# FALSAFA YA MAGEUZI YA IMAM HUSEIN

**Kimeandikwa na:**
Sayyid Jawad Naqvi

04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 1 4/25/2018 11:01:26 AM

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 17 - 010 - 4

**Kimeandikwa na:**
Syed Jawad Naqvi

**Kimetarjumiwa na:**
Alhaj Ramadhani S. Kanju Shemahimbo

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Hajat Pili Rajab

**Toleo la kwanza:** Juni, 2011
**Nakala:** 1000
**Toleo la Pili:** Septemba, 2018
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701
Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640
**Simu/Nukushi:** +255 22 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv.com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info/ebooks/

ILI KUSOMA QUR'ANI MUBASHARA
KWA NJIA YA MTANDAO,
TEMBELEA www.somaquran.com

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ............................................................1

Dibaji ya Mchapishaji ..........................................................3

Dibaji...................................................................................4

Utangulizi ............................................................................7

Historia na Falsafa ..............................................................16

Machimbuko mbalimbali ya kifalsafa ................................20

Kuielewa Falsafa ya Mageuzi ya Husein (a.s.) –
Qayam-e-Husein ................................................................23

Fafanuzi Ishirini tofauti za Kusimama
kwa Husein (a.s.)................................................................32

Matatizo Katika Kulichanganua Tukio la Karbala.............46

Tatizo la Kwanza – Maoni binafsi .....................................47

Tatizo la Pili – Silika ovu...................................................54

Tatizo la Tatu – Maono Finyu ya kiakili ............................63

Matokeo ya Uchambuzi wa akili Finyu .............................71

Husein (a.s.) – Mfasiri bora wa Karbala ............................75

Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s.)........................78

Husein (a.s.) – Mfano wa Kuigwa .....................................82

Kufungua Pazia la Karbala ................................................84

Kupumbaa kwa Ummah – Tatizo la Urithi ........................85

Kupumbaa – Silaha ya Madhalimu....................................88

Mwanzo wa Kupumbaa ....................................................94

Kupumbaa – Gonjwa la Mlipuko la Kijamii......................98

Kupumbaa juu ya Yazid ..................................................103

Lengo la kisimamo...........................................................107

Karbala – Kimbunga cha Mzinduko ................................115

Wito wa Karbala ni wa Kudumu Milele ..........................119

Ni Mwanzo – Sio Mwisho ...............................................124

Maswali na Majibu ..........................................................128



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 4 4/25/2018 11:01:26 AM

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, *Philosophy of Qayam-e-Hussain (a.s.)* kilichoandikwa na Sayyid Jawad Naqvi. Sisi tumekiita, *Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husain ('Alayhis 's-Salaam).*

Kitabu hiki kinaelezea falsafa ya mageuzi ya Imam Husain *('Alayhi 's-Salaam)*. Mageuzi ya Imam Husain (*'Alayhis 's-Salaam*). yalianzia mjini Madina na kukamilika tarehe 10 Muharram 61 Hijria katika ardhi ya Karbala. Mapambano haya ya mageuzi yalichukuwa takriban miezi sita, kuazia mwezi aliotoka Imam mjini Madina mpaka Makka na kuishia Karbala katika siku ya Ashura.Ujumbe wa Ashura na Karbala ni pigo kubwa kwa watawala madikiteta, wakandamizaji, madhalimu na mafisadi.

Kila siku zinavyokwenda, madhalimu hawa hujitokeza katika sura mbalimbali na kufanya ufisadi mkubwa katika ardhi. Lakini kama alivyosema Allah katika Qur'ani Tukufu: *"Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu amekataa isipokuwa kuitimiza nuru Yake, ijapokuwa makafiri wamechukia." (Qur'ani Tukufu*



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 1 4/25/2018 11:01:26 AM

*Sura at-Tawba;* 9:32). Allah anasema kweli, kwa hakika hawatafanikiwa katika njama yao hii

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukitarjum kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru Alhaj Ramadhani S. Kanju Shemahimbo kwa kukubali jukumu hili la kukitarjum kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa na changamoto kubwa kwa wasomaji wetu.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation.**



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 2 4/25/2018 11:01:26 AM

# DIBAJI YA MCHAPISHAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam.

Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 3 4/25/2018 11:01:26 AM

# DIBAJI

**MATAB** Publications wanayo furaha kuwasilisha kazi nyingine ya Ustadh Sayed Jawad Naqvi. Maudhui iliyoko kwenye mjadala ndani ya kitabu hiki ni "Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s.). Maudhui hii ni ya umuhimu wa hali ya juu sana katika zama hizi wakati ambapo mfumo wa utawala sawa na ule wa Yazid kama ule wa zama za Imam Husein (a.s.) umeenea katika sehemu nyingi za dunia leo hii, na hususan katika ulimwengu wa Kiislamu. Leo hii, majaribio yanafanyika ili kuyageuza malengo na madhumuni ya kule kusimama kidete kwa Imam Husein (a.s.). Mageuzi ya Imam Husein (a.s.) ni shule ya itikadi na harakati ambazo zinawahimiza wale watu waadilifu na wapenda kweli kusimama kwa ajili ya haki na wasivumilie dhulma na uonevu. Kuna baadhi ya walinganiaji wasiojua kitu na pia baadhi ya mawakala wa maadui waliopandikizwa ndani ya ummah wa Kiislamu ambao kwa kurudiarudia wanahalalisha utu wa Yazid bin Mu'awiyah na kujaribu kubadilisha kusudi la kusimama huku kwa ki-mungu kuwa ni mapambano ya maslahi ya kifamilia na kibinafsi yenye mwelekeo wa kisiasa baina ya pande mbili. Kitabu hiki kinatumika kama jibu kwa mashaka kama



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 4 4/25/2018 11:01:26 AM

hayo yaliyojengeka kwenye akili za watu, na baada ya kuelewa kwa kiasi fulani lile lengo la mageuzi ya Husein (a.s.), wasomaji wenyewe wanaweza kuchambua na kufikiri kuhusu ni sababu gani watu na vikundi kama hivyo ambao wanageuza utukufu wa kisimamo hiki na kuwathibitisha watu madhalimu kama Yazid kama mtu ambaye Mwenyezi Mungu atakuwa radhi naye.

Kitabu hiki kimesimama kwenye msingi wa semina ya hotuba nne zilizotolewa mara tu baada ya mauaji ya kikatili ya Shahid Muzaffar Kirmani (r.a.). Huyu Shahid Muzaffar alikuwa miongoni mwa wale wachache walioielewa falsafa ya harakati za Husein (a.s.) na alitiwa msukumo nazo. Safari yake juu ya njia ya Imam Husein (a.s.) ikawa ndio sababu ya risasi kupenya kwenye kifua chake.

Katika kitabu hiki, kwa mara nyingine tena Ustadh Sayed Jawad Naqvi anaiendelea maudhui hii nyeti katika njia ya kimantiki na kiuanachuoni. Anawasilisha maoni ishirini tofauti kuhusiana na lengo la mwamko wa Imam Husein (a.s.) na kisha anaelezea lengo halisi la kusimama huku kupitia kwenye maneno ya mwasisi wa mwamko huu mwenyewe, ambaye ni Imam Husein (a.s.).

Kitabu hiki kinatumikia kama utangulizi wa kuchokonoa wazo la mchakato wa suala muhimu sana



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 5 4/25/2018 11:01:26 AM

na lililobadilishwa na kugeuzwa sana. Kitabu hiki sio chenye upana sana ambacho kinaelezea maudhui hii kutoka kwenye vipengele vyote, kitabu hiki kimelengwa katika kulianzisha suala hili na watumiaji chakula cha sawa cha mawazo, ambapo wanaanza kufikiri, kuchunguza, kuchambua na hatimaye kuitekeleza dhana ya mwamko huu katika maisha yao wenyewe na jamii.

Kitabu hiki kimetafsiriwa (kwenye Kiingereza) na Bethat Islamic Reseach Center (B.I.R.C) ambayo inaendeshwa chini ya usimamizi mzima wa Ustadh Sayed Jawad Naqvi. Na kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Taasisi ya al-Itrah Foundation, Dar es Salaam. Kwa taarifa zozote za ziada juu ya kitabu hiki na mambo mengine yoyote yanayohusiana nacho, wasomaji wanaweza wakaangalia kwenye mtandao wa B.I.R.C. at www.Islamimarkaz.com



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 6 4/25/2018 11:01:26 AM

# UTANGULIZI

Maudhui iliyoko kwenye mjadala ni "Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s.)." Huu ni wakati mgumu kwetu sisi kuchukua juhudi kubwa hii kwa kutokuwepo kwa muasisi wa mlolongo huu wa semina – Shahid Muzaffar Kirman. Yeye na wale Mashahidi wote ambao waliitika "Labbayk" juu ya mwito wa Imam Husein (a.s.)

هَلْ مِنْ نَاصِرٍ يَنْصُرُنَا

**"Je, wapo wa kutunusuru sisi?"**
*Mausuwati Kalimati Imam Husein (a.s.)* – uk. 506.

Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za watu kama hawa katika amani.

Maudhui hii inaweza kuelimishwa kupitia vipengele mbalimbali. Ukweli ni kwamba waliokufa kishahidi wote katika historia ambao walitoa maisha yao kwa ajili ya Uislam waliuelewa wito huu na walitambua uhalisi wake, kwa kweli walifikia vina vyake na kugundua roho yake.

Utakutana na watu ambao wana wahaka, wasio na subira, wako tayari kuuliwa kishahidi, kwa mfano shahidi mheshimika Muzaffar Kirman; alikuwa ni nafsi



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 7 4/25/2018 11:01:26 AM

iliyoamka na isiyo na subira. Hakupata utulivu, hakuwa na amani, hakuna ukimya mahali popote. Wako wengi kama Shahid Muzaffar ambao bado hawajatambulika.

Tunapaswa kujaribu na kutambua tofauti kati yao na sisi; sisi ni watu tunaofurahia usingizi mzito, tulio na utulivu na amani na tunaishi maisha ya anasa bila ya kuwa na wasiwasi juu ya lolote, ambapo watu hawa kwa upande mwingine vilevile wanaishi katika dunia hii hii na kama wangefanya juhudi kwa ajili ya anasa hizi wangezipata zote kwa urahisi kabisa na wangeweza kuishi maisha ya starehe sawa na yetu; hata hivyo wao walipendelea kupata shida katika njia ya haki.

Kundi la idadi ya akina Muzaffa katika historia na leo hii ambalo hatulijui bado linaendelea kuishi. Sababu kubwa ya tofauti hii ni kwamba wao waliitambua falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s.). Bila shaka sisi pia tulichukua kitu kutoka kwenye falsafa hii lakini je, ni kweli kwamba tulichukua kile kilichohitajika sisi kukichukua? Kama kiini chake cha kweli kilipuuzwa na mtu fulani na kueleweka kwa mtu mwingine basi ni dhahiri kwamba kutokana na tofauti hii katika ufahamu, athari itakazokuwa nazo juu ya watu wawili hawa zitakuwa tofauti. Ni dhahiri kabisa kuna tofauti katika hali za yule ambaye ameiendea maana yake ya wazi na ambaye aliingia kwenye vina vyake na ameelewa kiini chake halisi.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 8 4/25/2018 11:01:26 AM

## MIHEMKO NA KUELEWA

Ulimwengu mzima bila ya kutofautisha kati ya waumini na wasioamini na madhehebu tofauti za Kiislam umetambua ile maana ya kisimamo cha Imam Husein (a.s.) angalau kwa kiasi fulani hivi na vilevile wamejaribu kuonyesha kuelewa kwao na utambuzi wa tukio hili kupitia taratibu maalum. Wala sio Waislamu tu bali pia na vikundi tofauti kama Wakristo na Ma-Hindu wanaonyesha heshima zao juu ya Imam Husein (a.s.).

Heshima na upendo wao ni msingi hivi kwamba mnamo tarehe 10 ya mwezi wa Muharram, India inatoa siku ya mapumziko ingawa sio nchi ya Kiislamu, Pakistani, ambayo ni nchi ya Kiislamu inatoa siku mbili za mapumziko kama ilivyo kwa nchi nyingine za Kiarabu. Wasio Waislamu kwa kusherehekea mapumziko ya siku moja huwa wanaonyesha shukurani zao ambapo Waislamu huifanya kwa siku mbili. Wale kati yetu sisi ambao kiulinganishi tunahusika zaidi, tunatoa heshima zetu kwa kuomboleza kwa muda wa siku kumi (10).

Haijalishi ni siku ngapi za mapumziko zinazotolewa lakini tunaweza kuelewa kule kupenda na kujihusisha kwao na Imam Husein (a.s.). Kumwaga machozi, kupiga vifua, kuhadithia mateso yao, kusikiliza juu ya taabu zao, yote haya yanaonyesha dalili ya namna fu-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 9 4/25/2018 11:01:26 AM

lani ya upendo na kwamba kuna heshima kwao juu ya Imam Husein (a.s.)

Hata hivyo, kwa upande mwingine, hapa kuna baadhi ya watu ambao kwao wao mwaka mzima unakuwa kama tarehe 10 Muharram (Ashuraa) kwa sababu sio kwamba wametambua tu ule ukweli kuhusu ujumbe wake bali pia wanaelewa kwamba inakuwa na maana gani pale inaposemwa: **"Kila ardhi ni Karbala na kila siku ni Ashura."** Wao wanaomboleza mwaka wote mzima kama siku ile ya mwezi 10 Muharram, kwao wao kila siku ni Ashura. Vichwa vyao viko makini juu ya Imam Husein (a.s.) kipindi cha mwaka wote mzima na sio ile mwezi 10 ya Muharram tu. Inawezekana vipi kwamba wale ambao wameelewa kile kiini na wamejenga imani yenye nguvu thabiti walale pembeni na kutenga siku chache tu za Muharram kwa ajili ya maombolezo na kisha kuzitumia siku zilizobakia kwa ajili yao wenyewe tu? Hapana, mara kile kiini kinapokuwa kimeeleweka basi hali haiwezi kuwa hivyo kamwe. Wachache wao wanakwenda mbali zaidi kiasi kwamba wanayageuza maisha yao yote kwenye Ashura.

Mihemko na kuguswa hisia kunaathiri kuenea dunia. Baadhi ya watu huishi maisha yao ya kawaida hata katika ile siku ya mwezi 10 ya Muharram. Kuna watu ambao



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 10 4/25/2018 11:01:26 AM

hubadili hisia zao kirahisi na kulingana na mazingira yanayowazunguka. Kwa wakati mmoja wanatiririsha machozi na katika sekunde tu inayofuatia huwa wanacheka. Wanaweza kudhibiti mihemko yao. Hizi ni kama zile hali ambazo mtu anaweza kuzitwaa kwa urahisi.

Ni mihemko ile ambayo inakuja kutoka ndani kabisa hadi nje, mihemko ambayo inakuja kutokana na kuelewa kuliko mazingira tu ndio viashirio kwamba kupo kuelewa. Macho ya mtu, uso na mwili mzima viko katika udhibiti wa nafsi na wakati nafsi inapouelewa huu ukweli halisi wa ujumbe wa Karbala, basi hapo na mwili pia unaathiriwa roho na hili haliruhusu mabadiliko ya haraka na ghafla ya hisia za mtu (kutoka katika hali ya kulia na kwenda kucheka) ambayo yanaweza kutokea tu iwapo mihemko hii ilikuwa ya kijuujuu tu.

Baadhi ya watu walimuuliza Imam (a.s.) kwamba, wakati tunapokuwa mbele yako hisia zetu zinakuwa sio za kawaida, lakini tunapokuwa tuko mbali na wewe tunahisi hali tofauti, ni nini sababu ya mabadiliko haya? Hii ni kwa sababu, pale mtu anapokuwa na ukaribu sana na kitu au jambo, huwa anajenga uhusiano na muambatano ambao umeegemea kwenye msingi wa uelewa wa juujuu na kwa kweli huo ni wa muda wa mpito tu.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 11 4/25/2018 11:01:26 AM

Hivyo tunaweza kusema kwamba, miongoni mwetu ambao kwamba kila siku imo ndani ya mipaka ya Karbala tu, tumefikia roho ya Karbala na tumeweza kuielewa kupita kiwango cha juujuu. Matukio yana mguso wa kihisia mzito juu ya wanadamu. Katika siku nzima kabisa mara kwa mara hisia na mihemko yetu hubadilika kulingana na hali lakini mabadiliko haya ni ya mpito tu na yanategemea juu ya ile hali tuliyomo ndani yake.

Lile tukio la Karbala lina mandhari mbalimbali za kimhemko na hivyo bila kujali mtu kuwa ni Shi'ah au Sunni au asiyeamini anazindukana kutokana na simulizi ya Karbala na anaonyesha hisia fulani kuhusiana nalo. Lakini hii haina maana kwamba mtu huyo ameipata maana halisi ya Karbala. Ukweli ni kwamba Karbala inayo mambo mengi ya kimhemko ambayo kwamba hata wale ambao walimpinga Imam (a.s.) waliathiriwa na hisia hizi.

Umekwisha kusikia kwamba katika ule usiku wa mwezi 10 wa Muharram, wakati hawa waporaji walipokuja kwenye mahema ya Imam Husein (a.s.) walilia huku wakiwa wanapora! Wakati mmoja wao alipofika karibu na Bibi Fatima Sughra (s.a.) yule binti mdogo kabisa wa Imam Husein (a.s.), Bibi huyo aliuliza: "Ewe muuaji, mimi sikuweza kuelewa kwamba unapora vitu vyangu na huku unalia pia?"



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 12 4/25/2018 11:01:26 AM

Kisha akajibu kwamba, “Mimi ninalia kwa sababu watu ninyi hamna hatia, hamna cha kulaumiwa, mnatokana na familia tukufu, familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na sababu ya kwa nini ninawinda vitu vyako ni kwamba, iwapo mimi nitaacha kuvipora basi mtu mwingine atalazimika kuja kuvifuata hivyo.”

Hayo yalikuwa ndio maneno ya adui huyo.

Kama muuaji kisaikolojia amevutika na anaanza kulia machozi, haina maana kwamba tuanze kumsifia eti kwa sababu tu ameelewa ile maana halisi. Umesikia kwamba wale watu katika mapaa ya nyumba za al-Kufah walikuwa wanalia wakati msafara huo ulipokuwa unapita kwenye mitaa ya Kufa, watu hawa walikuwa wakiwarushia mawe na vilevile huku wakilia kwa sauti kubwa.

Bibi Zainab (a.s.) hakuwauliza kwamba ninyi watu mlikuwa mnatambua ukweli wenyewe na licha ya kuwa sehemu ya sababu ya msiba huu bado mnalia? Lakini badala yake alianza hotuba yake kwa kuwalaani akisema:

“Natamani Mwenyezi Mungu ayaendeleze machozi yenu milele kwa sababu machozi haya sio machozi ya huzuni, haya ni machozi ya watazamaji tu.”



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 13 4/25/2018 11:01:26 AM

Je, umewahi kuwaona watazamaji? Watazamaji wanatekeleza mara moja, kwa mfano wakati baadhi ya watu wanapokuwa wanacheza mchezo, na ile timu wanayoiunga mkono inashindwa, basi wanakuwa na huzuni, na kama timu hiyo ikishinda basi wanakuwa na furaha.

Pale watu wa Kufa walipoyaona kama matukio yale; wanawake, mabibi, wasichana wadogo, vile vichwa kwenye mikuki ….. wao pia waligusika kihisia na matukio hayo kwa kiasi fulani kwamba hata Yazid alipatwa na mhemko na akasema: "Mimi sikumwambia Ubaidullah kufanya tendo la kikatili kama hili na yote haya ni matendo yake mwenyewe." Alisema yote haya kwa sababu alijua kwamba endapo angekiri makosa yake watu wangempinga.

Kuhitimisha juu ya hili ni kwamba msisimko wa kimihemko ni uakisi tu wa silika za mwanadamu na kutangaza mapumziko ya siku mbili au tatu kunaonyesha tu namna ya upendo kwa Imam (a.s.) kwa wale wanaopatwa na hisia hizi.

Lakini wako tofauti; wale ambao wameunganishwa na roho ya Karbala, ukweli halisi wa Karbala, wale ambao wanajua ile falsafa ya kisimamo cha Imam Husein (a.s.) – "Qayam-e-Imam Husein (a.s.)" wale ambao kiungo chao sio cha kimhemko tu hivi basi, au kiungo



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 14 4/25/2018 11:01:26 AM

cha juujuu. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba hawana muambatano wa kihisia; bali wanao mwambatano huo na kadhalika uelewa wa Karbala kwani watu hawa nao ni binadamu.

Haitoshelezi kule kuonyesha hisia tu basi; bali unapaswa kuambatana na ile maana halisi na ya kweli ya Karbala katika msingi wa huu muambatano wa kihisia. Unapaswa kuchukua hatua hii moja mbele katika kuelewa kiini chake cha kweli.

Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s.) ndio falsafa ya Karbala, falsafa ya kifo cha kishahidi, kiini cha dini na moyo wa Uislamu na Qur'ani. Uhusiano wa kimhemko ni mawasiliano tu yaliyowekewa mipaka na hisia tu na kamwe hauonyeshi njia ya kwa mtesekaji kwa ajili ya jambo hilo. Mihemko kamwe haitufikishi kwenye vina, hata hivyo inatengeneza msingi wa muambatano ili kukuza uelewa wetu wa ukweli ulio nyuma ya matukio au kwa maneno ya wazi kama Imam (a.s.) alivyosema katika siku ya mwezi 10 Muharram: "Mimi ni mtoa mfano wa kuigwa kwa ajili yenu, jaribuni kujifanya wenyewe kama mimi, twaeni mtindo wangu, fikra na muonekano wangu. Hali yangu leo hii ni picha wakilishi kwa ajili yenu; mazingira yangu ya sasa ni alama kwa ajili yenu." Wakati mwanadamu



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 15 4/25/2018 11:01:26 AM

atakapoipata ile maana yake ya kweli, basi kila siku inakuwa kama mwezi 10 ya Muharram kwake na kila sehemu ya dunia inakuwa kwake ni ardhi ya Karbala.

Hii ina maana kwamba, ni juu ya utambuzi wako, kuelewa kwako kwamba ima hutatengeneza Karbala moja katika uhai wako au utaipitisha kila siku ya uhai wako kama Ashura.

Mashaahid kwa kweli ni watu ambao kwamba wameelewa hii maana ya kwamba Imam Husein (a.s.) alikuwa ni alama (ya kigezo) kwa ajili yao. Hivyo, hata baada ya muda mrefu kama huo, alama hii bado ingali hai kwa ajili yao na kwamba sio wakati wala ardhi ambavyo vimewazuia wao kuthibitisha kwamba wao ni wafuasi wa kweli wa Imam Husein (a.s.) kwa kuweza kuikamata sawasawa ile maana ya kweli halisi ya falsafa hii.

## HISTORIA NA FALSAFA

Ni madhumuni gani juu ya kuielewa falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s.)? Sura zake za dhahiri ni lazima ziangaliwe ili kwamba wakati tutakapoijadili baadae, akili zetu hazitakuwa na shaka juu yake.

Inawezekana kwamba mpaka sasa umeifikiria ile elimu kuhusu historia ya Karbala kama falsafa yake.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 16 4/25/2018 11:01:26 AM

Utambuzi wa kihistoria kwenye tukio la Karbala unaweza kuwa ni hatua moja kuelekea kwenye falsafa hiyo, lakini kwa hali yoyote ile historia ya tukio hilo inakusudiwa kuelezea falsafa yake.

Nadharia za kifalsafa kuhusu Karbala sio historia ya Karbala na lengo la "Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein" sio kusimulia ta'arikh kuhusu Karbala kwa mtazamo wa kihistoria.

Falsafa ya Karbala ni kujaribu kuelewa kwa nini kulikuwa na mageuzi katika Karbala? Nini sababu zake, vyanzo na vipengele ambavyo vimesababisha kuchukuliwa kwa hatua kama hizo na Imam Husein (a.s.)?

Kama tukijumuisha kwa mukhtasari sababu zote, vipengele na vyanzo na kuelewa jinsi hivi vilivyopelekea kusimama huko basi itakuwa ni mkusanyiko huu ambao utaitwa Falsafa ya Karbala.

Maelezo ya jinsi Imam Husein (a.s.) alivyochukua kisimamo hiki (mageuzi) kwa mfano, katika tarehe kama hiyo safari ilianza, katika tarehe hii Makka ilifikiwa hiyo ndio historia ya Karbala. Tunaijua historia hii kwa kiwango fulani lakini ni jambo la kusikitisha kwamba wakati mwingine ile historia kiasi kidogo tunayoijua ni ya kubuniwa vilevile. Sababu ya hili ni kwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 17 4/25/2018 11:01:26 AM

sababu watu ambao hawana uhusiano na kiini chake sasa hivi wameanza kuisimulia.

Chukua mfano wa mama wa mtoto mgonjwa na muuguzi ambaye analipwa kwa ajili ya kumuangalia mtoto huyo mgonjwa. Kama muuguzi huyo atachoka na mtoto akaanza kulia, basi atamkaripia mtoto huyo. Hata hivyo, hata kama mama huyo mwenyewe akiwa mgonjwa na mtoto akawa mgonjwa wakati wa usiku, basi mama huyo atapuuza adha yake mwenyewe na kumshughulikia mtoto. Kwa muuguzi huyo ni kazi yake kumwangalia mtoto huyo na analipwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, na kama utamwambia muuguuzi huyo amsimulie mtoto hadithi, atafanya hivyo pia kwa sababu analipwa ili kufanya hivyo.

Hivyo tunapowalipa watu ili wasimulie hadithi ya Karbala basi wanafanya kazi yao. Hivi kweli watajali kuhusu kile wanachokisema, iwapo imebuniwa au laa, madhali wao wanalipwa?

Baadhi ya watu wanasema kwamba "Maimam" hao waheshimika walikuwa wakifanya vivyo hivyo na kwamba wasimulizi wa Karbala walizawadiwa na Maimam lakini huku ni kuelewa vibaya, Maimam wetu hawakuwazawadia tu mtu yeyote aliyesimulia hadithi ya Karbala katika namna ya mtindo ambayo msikili-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 18 4/25/2018 11:01:26 AM

zaji alikuwa akidhania wangeweza kuwa na tamaa ya Karbala. Maimam walitaka kueleza kwamba sisi sote lazima tujaribu kuiangalia Karbala na kuisimulia kwa usahihi. Zawadi hizo hazikuwa mishahara; huwezi kulipwa kwa kazi hii.

Hivyo wakati msimuliaji anapoanza kusimulia historia hii kile kinachokuja akili mwake kinakuwa ni historia ya Karbala kwa vile watu wanaomsikiliza wanaichukulia kwamba ni kweli, huenda mtu huyu hakusoma hata kitabu kimoja kuhusu Karbala. Hivyo ni jambo la muhimu kwetu sisi kuona kwamba historia ya kweli na halisi kwa kweli itapotea.

Na hili sio kosa lake tu, na sisi tuko vivyo hivyo, tunaweza tukawa tumesoma vitabu vingi sana vya silabasi ya Chuo Kikuu chetu na vitabu vinginevyo lakini kamwe hatukujaribu kusoma kitabu juu ya Karbala. Hivyo chochote atakachokisema mtu huyo kwa jina la Karbala kinakuwa ni sahihi kwa msikilizaji vilevile. Huyo msikilizaji na msimuliaji wote wako sawa kwa sababu hakuna mmoja kati yao ambaye amesoma chochote.

Lakini kila mtu hayuko hivyo. Karbala ina wataalamu na wanahistoria ambao wameandika na kusimulia ile historia sahihi. Hata hivyo, sio lazima kwamba baada ya kuisikiliza historia hiyo mtu anaweza akaele-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 19 4/25/2018 11:01:26 AM

wa madhumuni ya Karbala, kwa ajili ya hili ni lazima kusoma ile falsafa ya historia, falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s.).

Nimewaambieni yote haya kwa sababu mnazingatia akilini kwamba historia ya Karbala ni mada nyingine na kusimama kwa Imam Husein (a.s.) nayo ni mada nyingie tofauti. Simulizi ya hadithi hiyo ni historia; ambapo uchunguzi na upimaji juu ya kwa nini matukio maalum kama hayo yalitokea na matokeo yake ambayo yalikuwa kwamba Karbala ni falsafa.

## MACHIMBUKO MBALIMBALI YA KIFALSAFA

Kadhia ya Karbala inahitaji maelezo sawa sawa na aya za Qur'ani. A ya vilevile yenyewe ina historia kwamba wakati iliposhuka maudhui yake ilikuwa ni tofauti kabisa. Utambuzi juu ya Karbala unategemea juu ya kuelewa, ni kwa nini kadhi hii ya Karbala ilitokea? Nini kilichosababisha itokee? Sasa, tunapaswa tu kutafuta jawabu la hii "kwa nini."

Maelezo mbalimbali yanatolewa. Baadhi ya watu wanadai kwamba utawala wa wakati huo ulikuwa ukimdai kiapo cha utii Imam Husein (a.s.) kwa ajili ya Khalifa (Yazid), hivyo kama majibu, yeye alianzisha



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 20 4/25/2018 11:01:27 AM

mageuzi (*Qayam*) haya. Sasa swali linalojitokeza lenyewe ni "Ni vipi kama kiapo hiki kisingedaiwa na utawala huo? Je, Imam (a.s.) asingepanga mageuzi haya na hivyo kwamba sababu pekee ya kusimama kwake kidete ilikuwa ni haya madai ya kiapo cha utii? Zaidi hasa watu wanadhani kwamba maelezo haya na fikira hiyo ni uakisi wa ukweli.

Maelezo ya namna nyingine ni kwamba kwa sababu watu wa al-Kufa waliandika barua kwa Imam na kumualika ndio maana alianzisha mageuzi hayo kama matokeo ya barua hizi. Watu walimualika yeye kwa ajili ya mapinduzi na yeye akachukua msimamo huo. Tena swali hilo hilo kwamba ni vipi kama barua hizo zisingeandikwa na watu hao wa al-Kufa, hivi basi kusingekuwa na haja ya mapinduzi haya?

Maelezo mengine ni kwamba hata ingawa kama alitakiwa kiapo cha utii na barua hizo ziliandikwa, ilikuwa ni majaaliwa ya Imam kwamba alipaswa kukumbwa na yote haya. Au kwamba lengo la msingi nyuma ya mageuzi haya lilikuwa ni kifo cha kishahidi, yaani, Imam (a.s.) alitaka kuuliwa kishahidi hivyo alitimiza matakwa yake kwa tukio hili.

Baadhi ya watu wanasema usilihusishe tukio la Karbala na Imam Husein (a.s.). Imam alikuwa ni



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 21 4/25/2018 11:01:27 AM

muathirika wa Karbala, usiliite ni kisimamo (*Qayam*) cha Imam Husein. Hivyo wao wanasema; watu waliosababisha ya Karbala walikuwa ni Umar-e-Saad, Shimri, Ubaidullah au Yazid. Wao walikuwa ndio waandaaji wa Karbala. Watu hawa wamejaribu kuibadili Karbala ya Husein kuwa Karbala ya Yazid.

Uwezekano mwingine juu ya sababu ya Imam Husein (a.s.) kuanzisha mageuzi haya ilikuwa ni kwa sababu yeye alitaka kusimamisha haki, serikali ya utendaji wa ukweli halisi na kwa sababu aliiona serikali ya wakati ule kuwa ya kidhalimu, hivyo alianzisha mageuzi haya kwa ajili ya kufanikisha haki yake.

Sio tu kwamba kila kundi lilifikia maelezo yake tofauti, bali pia waliijenga historia kulingana na maelezo hayo.

Maelezo mengine ni kwamba yeye alichukua njia hii ya kisimamo cha mageuzi ili kuirekebisha jamii. Kuingia madarakani hakukuwa ndio lengo lake, ilikuwa ni umma ndio uliokuwa umeharibika. Yeye alitaka kurekebisha machafu yao. Kadhalika katika maelezo mamoja sababu ya Karbala ilikuwa ni: "Kuamrisha mema na kukataza maovu."

اَمْرَ بِالْمَعْرُوفِ وَ اَنْهى عَنِ الْمُنْكَر

**Kuamrisha mema na kukataza maovu.**



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 22 4/25/2018 11:01:27 AM

Kama tunataka hasa kujua “falsafa ya kusimama kidete kwa Imam Husein (Qayam-e-Husein), kwa kweli tunapaswa kueleza ile siku ya Ashura kwa taswira chambuzi ili kuelewa ni zipi zilikuwa ndio sababu halisi za kwa nini Imam Husein (a.s.) alilazimika kuanzisha mageuzi haya ndani ya Karbala.

## KUIELEWA FALSAFA HALISI YA MAGEUZI YAIMAM HUSEIN (A.S.)

Falsafa yenyewe ni Ujumbe wa Kihistoria ambamo masuala mengi yanajadiliwa na yanaweza kujadiliwa. Kama ilivyoelezwa mapema, ufahamu juu ya historia ya Karbala ni muhimu lakini unaanzwa kwa masikitiko kwamba ile historia ya kweli halisi inaweza isielezwe. Sisi kama wasikilizaji hatuutambui usahihi wa matukio yaliyotokea huko kwa vile tunatosheka na kusikiliza tu. Ni dhahiri kwamba wakati wazungumzaji wenyewe hawana utambuzi, basi ni vipi tunaweza kutarajia hali ya wasikilizaji kuwa na uzuri wowote?

Vyanzo vinavyofaa vya historia ni vitabu. Hivyo, wasikilizaji wanapaswa angalau kuchunguza kitabu kimojawapo cha historia katika maisha yao ili kupata mtazamo sahihi kwenye historia. Hicho kisiwe ni mkusanyiko wa hotuba au mahubiri ya mtu yoy-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 23 4/25/2018 11:01:27 AM

ote kwa sababu hayaelezei historia kama yanavyotoa taswira ya mtu yule. Ili kupata umaizi halisi kwenye mambo ya kihistoria baadhi ya vitabu sahihi vinapaswa kusomwa.

Ingawa kusoma historia peke yake tu kunazidisha elimu ya mtu, kama vile ambavyo kuna wanahistoria wengi ambao wana utambuzi mzuri wa historia ya Karbala na matukio mengine ya kihistoria vile vile, lakini utambuzi wa mambo sahihi ya kihistoria hautoshi kuunda msingi wa uelewa halisi. Kama iliwezekana kwa mambo ya historia kutoa uwepo halisi wa Karbala basi kuna wasiokuwa Waislam wengi na Waislam pia wa madhehebu tofauti ambao wanafahamu historia hasa ya Karbala. Watu wa zama zile, wale waliokuwepo mnamo mwaka wa 61 Hijiria pia wanafahamu yale maelezo ya uhakika, lakini licha ya kujua uwasilishaji sahihi wa historia bado hakukuwa na faida. Kwa kweli, maadui wa Imam Husein (a.s.), wauaji wa Bwana wa Mashahidi (*Syed-Us-Shuhadaa*) walikuwa wanatambua kikamilifu historia hiyo kwa sababu walikuwa ni wao walioitengeneza historia hii.

Hivyo inaonekana kwamba kule kuijua tu historia ya kweli hakutoshi kupata umaizi kwenye kadhia na kuendeleza uelewa wa kweli juu yake.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 24 4/25/2018 11:01:27 AM

Historia ni kipengele kimoja tu cha Karbala na sio uelewa mzima kamili wa Karbala, bali inaelezwa kwa huzuni kubwa kwamba sisi hatulitambui hili. Kama tunataka kufanya uchanganuzi wa maelezo sahihi ya kihistoria basi tunapaswa kujifunza kitu fulani na hicho ni falsafa ya Karbala, ile falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s.) – Qayam-e-Husein (a.s.). Kule kulielewa hili kuna maana kubwa kabisa na ni muhimu mno kabisa.

Kwa kifupi ili kuliweka wazi hili, linaweza kuonyeshwa kuhusiana na vitendo vyetu vya ibada. Kuna baadhi ya vipengele vya wazi vya ibada, kwa mfano, Udhuu, Tayammam na kadhalika na vingine vingi vyenye idadi ya wazi ya maelekezo. Kwa swala za kila siku kuna shuruti, misingi, vifungu na wajibat ambazo zinahitaji kukamilishwa katika swala. Wanachuoni wameelezea kanuni za sharia za Kiislam (fiqhi) za kila kimoja ya vipengele hivi na sisi kwa mujibu wa hizo kanuni tunatekeleza swala zetu. Tunaswali swala sahihi, tunafanya udhuu sahihi na kutekeleza taratibu zote ipasavyo lakini baadae tunakuwa na shaka bado iwapo swala zetu zimekubaliwa au hapana. Wakati ambapo tunaziswali kwa mujibu wa kanuni hizo, sasa kwa nini tunakuwa na hofu? Hatimae tunaliacha hilo juu ya Allah kwa kusema "Insha'Allah (Mungu akipenda) ataikubali swala yetu.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 25 4/25/2018 11:01:27 AM

Sasa swali linajitokeza kwamba je, kuna kigezo chochote cha kuweza kujua iwapo swala zetu zimekubaliwa au hapana? Jawabu ni "Ndiyo" kipo kigezo, yaani kuna athari fulani za Swala zilizotajwa ndani ya Qur'ani na Maimam Ma'sum. Athari moja inayojulikana sana ni:

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ

**"Bila shaka swala inazuia maovu na machafu." (Qur'ani Tukufu Sura al-'Ankabut; 29:45)**

Hii ni athari, lakini hii ni athari ya kukubaliwa swala tu. Kama baada ya swala hadi wakati wa swala inayofuatia au katika maisha yako yote ukawa hufanyi upungufu wowote au dhambi kutoka kwenye ulimi, mkono, macho au kiungo chochote basi ni dhahiri kwamba swala yako imekubaliwa kwani imekufanya wewe ujiepushe na upotofu. Hii ni sawa na kukagua usahihi wa viza ya nchi. Kama utaweza kuingia kwenye nchi hiyo ina maana kwamba viza yako ilikuwa ni sahihi na halali, vinginevyo isingewezekana. Kadhalika endapo mtu atazitekeleza swala zake lakini akawa ni mpotovu inaonyesha kwamba swala zake hazikukubaliwa kama aya hiyo hapo juu inavyothibitisha. Hivyo, kukubaliwa kunawezekana kama badala ya kufikiria vipengele vya taratibu za swala tu, tunajaribu kutambua dhati ya swala.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 26 4/25/2018 11:01:27 AM

Kumwaga maji juu ya mkono hakumzuii mtu kutokana na uovu kwa sababu mtu anaweza akachukua udhuu hata kwa kupora maji kutoka kwa mtu mwingine au kama ukiingia kwenye nyumba ya mtu mwingine bila ya kukaribishwa na ukatumia maji ya udhuu bila ruhusa. Kama huyo mtu hakufurahia kuhusu kuingia kwako kwenye makazi yake ataridhika vipi na kuchukua kwako udhuu kwa kutumia maji kutoka kwenye nyumba yake? Ni dhahiri, kama wewe ni mgeni, katika hali hiyo inaruhusika. Hata kama nia yako ni kwa ajili ya udhuu lakini udhuu huu haukubaliwi na Mwenyezi Mungu. Hivyo mtu anapaswa atambue dhati ya swala pia, sambamba na maelekezo yake.

Swala ina sehemu mbili; vitendo vya kanuni za kiada na dhati iliyofichika na tunapaswa kuzitambua zote kwani uhalisi, na moyo wake, unatokana na hii dhati iliyojificha. Tatizo la kawaida linalokabiliwa na wengi wetu ni kukosa umakinifu katika swala zetu na tunavurugwa kirahisi na hata kama tumehifadhi kikamilifu taratibu zote kwa usahihi kutoka kwenye *Tauziihal-Masail* (kitabu cha kanuni) bado tunavurugwa kimawazo kwa urahisi kabisa. Sababu ni kwamba kile kipengele ambacho kinaweka mazingatio yetu kwa Mwenyezi Mungu wakati wa swala, hakimo katika maelekezo ya taratibu za kiada, badala yake kimo katika ile dhati iliyofichika,



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 27 4/25/2018 11:01:27 AM

na kuwa na uwezo wa kuelewa uhalisi wa swala kutatufanya sisi tuwe makini kumwelekea Mwenyezi Mungu sio tu ndani ya swala bali pia hata wakati tunapokuwa nje ya swala.

Hivyo unaweza ukaiona tofauti iliyo kubwa sana kati ya mtu pale anapokuwa anatambua tu zile dalili za dhahiri za kitu fulani na pale anapotambua ile dhati yake. Kama ilivyoelezwa kabla kuhusu yule shahidi ambaye ndiye alianzisha mfululizo huu wa mijadala (semina), tendo lililobarikiwa, na ambaye kwa masikitiko makubwa sana hatunaye miongoni mwetu leo hii, Marhum Shahid Kirman (Mola amuweke pema peponi), yeye aliielewa dhati au kiini cha Karbala na hicho ndicho kilichomfanya awe tofauti. Hizi ni sura mbili (dhati ya dhahiri na ile iliyofichika) ambazo kwazo jambo linaweza kuangaliwa ambako kunatusaidia sisi kuonyesha kwa mfano ile tofauti kati ya Marhum Shahid huyu na sisi.

Tunaweza kuielewa tofauti hii endapo tu kama tunaelewa kwamba Karbala vilevile ina sura mbili, kama vile ambavyo Qur'ani ina sura mbili, na swala nayo ina sura mbili; moja ya dhahiri na nyingine iliyofichika. Yule ambaye anatambua vipenegele vya wazi vya taratibu za swala yake atakuwa tofauti na yule ambaye



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 28 4/25/2018 11:01:27 AM

anatambua pia na zile siri zake zilizofichika. Kadhalika Karbala pia ina sura mbili; moja ni kutokeza kwa Karbala, yaani ile historia ya Karbala (ambayo vilevile imegeuzwa na kubadilishwa na haikunukuliwa kwa usahihi hasa), na nyingine ni kiini cha Karbala, ule ujumbe hasa wa Karbala, ambao ndio ule ukweli uliofichika katika tukio hilo la Karbala.

Sasa swali linaibuka hapa la ni namna gani ya kufikia hicho kiini, kwa mfano ni namna gani ya kukifikia kiini cha Qur'ani, kiini cha swala, kiini cha Karbala na ni muhimu kutambua kwamba kwa lengo kama hili kusoma tu aya, kufuata idadi ya maagizo au kule kusoma tu maelezo ya kihistoria hakutoshelezi. Unaweza kuwa umewaona Wahifadhi wa Qur'ani (*Hafidh al-Qur'an*) wengi ambao hawaielewi hata ile maana ya "Bismillah," hivyo kutambua dhati hiyo tunahitaji maelezo, tunahitaji ifunuliwe, tunaihitaji inyanyuliwe kutoka nyuma ya pazia ya ibada. Swala inahitaji maelezo, Qur'ani inahitaji kutafsiriwa (Qur'ani wala haihitaji kuelezwa, sio kwamba yenyewe inahitaji kuelezwa bali ni sisi tunaohitajia maelezo ya Qur'ani). Qur'ani iko dhahiri na wazi lakini sisi hatuielewi mpaka atokee mtu aifafanue. Kadhalika historia ya Karbala iliyonukuliwa haitoshelezi, inahitaji kufafanuliwa ili kwamba sisi tuweze kuanza kuielewa.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 29 4/25/2018 11:01:27 AM

Kwa mfano, mimi nataka kuhubiri Qur'ani na kama nitaisoma sura nzima ya al-Baqarah mbele yako hilo litakufanya uchoke tu na hata kukufanya usiifurahie Qur'ani yenyewe. Hivyo kama Surat-al-Baqarah ikisomwa mbele yako kwa masaa mawili hadi matatu, matokeo yake ni kwamba wakati mwingine hutafika karibu yangu au karibu na Qur'ani au Suratul-Baqarah! Bali kama aya moja au aya chache tu zikisomwa mbele yako pamoja na maelezo na ufafanuzi, basi kwa vyovyote utavutiwa kwenye Qur'ani kwani utakuwa unafikiria kwamba ikiwa idadi ndogo ya aya zinaweza kuwa na kina kikubwa kiasi hiki, basi kina cha Qur'ani nzima na maana yake kitakuwa chenye kuvutia na kuchochea sana. Hivyo maelezo, ufafanuzi hudikiza kupenda na mvuto. Hali kadhalika ile kadhia ya Karbala; kama ilivyoelezwa hapo kabla na kwa muendelezo (sio ile Karbala iliyosimuliwa kwetu), inahitaji kuangaliwa kwa ujuzi wa kina kirefu zaidi.

Tunayo hadhara bora na waumini wazuri kabisa, lakini waumini hawa wameshughulika sana katika mambo yasiyo ya kisomi kwa kiasi kwamba hawapati nafasi ya kutimiza matakwa yao ya kisomi, hivyo watu wanaitumia fursa kutokana na ujinga wetu lakini hawajaribu kuuondoa. Sishuhudii kwamba hawa watu waliochukulia



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 30 4/25/2018 11:01:27 AM

ujinga wetu kwa kawaida na hiba wameinakili ile historia sahihi, na kama tulivyoeleza kabla, tunapaswa kusoma na kuchunguza angalau kitabu kimoja juu ya historia ya Karbala. Bali kama historia sahihi imenakiliwa, inawezekana kwamba watu wanakuwa wamechoka kwani inaweza ikaelekea kuwa kama hekaya tu. Matukio fulani ambayo yamekuwa yakisikika ndani ya kadhia ya Karbala yanaweza yakawa hayapatikani katika historia ya kweli endapo tunaisoma hivyo tunavunjika moyo na kukerwa nayo. Lakini kutakuwa na watu ambao hawachoki kwa sababu ile historia ya kweli yenyewe inavutia sana, na pale tu unapoanza kusimulia baadhi ya matukio ya kihistoria watu wanakuwa wanahusika nayo, kwa sababu historia ina nguvu ya mvuto bali wakati mwingine huwafanya wasikilizaji wake kuchoka hususan kama hii mojawapo kwa vile haina mabadiliko ya matokeo ambayo yanaweza kuwavutia wasikilizaji.

Hivyo historia ya Karbala inahitaji maelezo na ufafanuzi kwa sababu bila hivyo hakuna atakayeweza kulielewa zinduko la Karbala, na hii ndio sababu kwamba wale watu ambao wanaweza kulielewa zinduko la Karbala wana tofauti kubwa kabisa na watu wa kawaida kama akina sisi. Wao hawachukui siku moja, mbili au kumi za mapunziko au kujigamba kwa thawabu ambazo zinaweza kupatikana kwa kushiriki ka-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 31 4/25/2018 11:01:27 AM

tika kukumbuka tukio la Karbala. Kama mtu atapata kuuelewa moyo wa Karbala na ukweli wa Karbala basi atakuwa amechanganyikiwa na kuguswa kuhusu ni vipi namna ya kutekeleza wajibat zake kuhusiana na haki za Karbala. Hivyo tofauti hii chimbuko lake linaanzia kwenye kule kuelewa kile kiini cha Karbala.

## FASILI (MAELEZO) ISHIRINI TOFAUTI JUU YA MAGEUZI YA HUSEIN (A.S.)

Sio kwamba hakuna hata mtu mmoja ambaye amewahi kuelezea Karbala kamwe, wengi wameeleza kadhia ya Karbala na kila mmoja amefanya hivyo kwa mujibu wa maoni yake mwenyewe. Ningependa kutaja orodha ya maelezo ambayo yanajulikana zaidi na ambayo yanastahili kuitwa maelezo. Ingawa kuna takriban maelezo kama hamsini yanayowezekana, kuhusiana na mageuzi haya ambayo yanapatikana kutoka kwenye vyanzo tofauti lakini sisi tutachukua ishirini tu ambayo ni maarufu sana. Aya moja tu ya Qur'ani imeelezewa katika njia mbalimbali, kadhalika kadhia ya Karbala pia inaweza kuelezwa kwa namna na njia mbalimbali.

Baada ya orodha hiyo tutatafuta maelezo ya ni kanuni gani kwa ajili ya maelezo ya Karbala, ni vipi tutakavyoielewa Karbala, ni vipi tutakipata kiini cha Karbala



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 32 4/25/2018 11:01:27 AM

ili tuweze kupata ujumbe wa mageuzi hayo - Qayam-e-Imam Husein (a.s.) na kisha tuone matokeo yake.

Kama vile tu ambavyo swala inavyomzuia mtu na upotovu, Karbala nayo pia inamkataza mtu upotofu. Inawezekana vipi kwamba mtu anayeielewa Karbala na wakati huohuo akawa ni mpotofu, haliwezekani hilo. Kama kugusa aya ya Qur'ani bila ya udhuu kunavyokatazwa, kugusa aya ya Karbala bila tohara pia kunakatazwa. Kwa madhumuni haya utakaso wa nafsi, hisia za upenda starehe, akili na tabia unahitajika. Sasa kila mtu anafanya lile analotaka kwa jina la Karbala, ambavyo ni kuvunja heshima na ufedheheshaji wa Karbala. Karbala ni tukio lisilo na hatia la mja Ma'sum. Kama Qur'ani inavyojisemea yenyewe kwamba ni wale waliotakaswa tu wanaoweza kuigusa, kadhalika ukaribu na wahusika hawa kunaweza kupatikana tu kwa utakaso.

**Fasili ya Kwanza:** Kama ilivyoelezwa kabla, watu waliuliza ni kwa nini kadhia hii ya Karbala ilitokea, kwa lengo gani. Ukweli na malengo ya Karbala yalikuwa ni yapi? Walipochungulia kwenye historia walikuta kwamba ilikuwa ni kwa matokeo ya madai ya kiapo cha utii. Wanafalsafa wengi wana maoni ya kwamba sababu ya msingi ya Karbala ilikuwa ni yale madai ya



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 33 4/25/2018 11:01:27 AM

kiapo cha utii. Wao wanadhani kwamba kama Yazid asingetoa madai ya kiapo cha utii kutoka kwa Husein ibn Ali (a.s.), ngano hii ndefu juu ya Karbala isingetokea.

**Fasili ya Pili:** Ilikuwa ni mwaliko wa watu wa Kufa. Kama watu wa Kufa wasingemualika, Imam Husein (a.s.) kamwe asingekuja, ilikuwa ni watu wa Kufa waliomchochea Imam Husein (a.s.), vinginevyo angebakia kujishughulisha katika maisha yake.

Baadhi ya watu wamesema kwamba hicho kiapo cha utii hakikuwa ni jambo la muhimu sana hivyo. Imam Husein (a.s.) alitoka Madina kwenda Makka hivyo angebakia Makka ama kurejea mara baada ya Hijja, au wakati ambapo hali ingetulia angeweza kurejea kama mahujaji wengine wote, lakini wakati Imam Husein alivyotoka Makka kuelekea Kufa, sababu ya msingi ya safari hii ilikuwa ni mwaliko ule wa watu wa Kufa kwa Imam Husein (a.s.) na halafu wakajitoa kwenye mwaliko huo. Huu mwaliko na huku kujitoa kwao kulikuwa ndio sababu ya kuanza kwa tukio hili la msiba.

**Fasili ya Tatu;** kama ilivyoelezwa mwanzo, ambayo siku hizi imekuwa ndio maoni ya kawaida kabisa, kwamba hii ilikuwa ni jaala, ilikuwa ni majaliwa ya kiungu na Imam Husein (a.s.) alikuwa hana jinsi mbele



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 34 4/25/2018 11:01:27 AM

ya matakwa ya Mwenyezi Mungu na ilikuwa afanye kama ilivyoagizwa, Yazid pia alikuwa anahusika kwa kitendo hiki, haya ni matokeo yaliyokuwa yamekwishapangwa. Kama tulivyokwisha kusikia mara nyingi kutoka kwenye mimbari zetu kwamba Imam Husein (a.s.) alimwambia dada yake; "Dada yangu sasa ni majaliwa yako," na dada akasema, kaka yangu, haya sasa ni majaliwa yako, maneno haya yamechukuliwa kutokana na fasili au maelezo haya vinginevyo hayamo katika historia kwa kweli. Fasili hii ilikuwa ya kawaida sana katika siku zile hususan Bani Umayya walikuwa wakisema kwamba haya sio makosa yetu na kwamba hawakupaswa kulaumiwa kwani yalikuwa ni majaaliwa ya kiungu yaliyobeba tukio zima, na hili lilisimuliwa maalum hasa na watu walilipwa kuyatangaza maoni haya kwamba ilikuwa kadara ya Imam Husein (a.s.) kuuawa. Tangu hapo maoni haya yalienezwa na hivyo bado yapo hai. Yalienezwa kupitia washairi, wanahistoria, wanachuoni, wanafalsafa ambao walilipwa vizuri kabisa kwa ajili ya lengo hili ili kwamba kusiwe na yeyote wa kuchukuliwa kuhusika, na sasa baada ya miaka 1400 maoni haya bado yanaendelea kushikiliwa.

**Fasili ya Nne:** Hii ni kwamba, Imam (a.s.) alikuwa na tamaa ya kupata Shahada, kwamba Imam (a.s.) aliyafanya yote haya kwa sababu alitaka kuwa Shahid na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 35 4/25/2018 11:01:27 AM

washairi wamelithibitisha hili, maoni haya ndio chanzo cha udanganyifu katika imani ya Imam (a.s.):

"Kifo cha kishahidi ndio madhumuni na lengo la mu'mini, wala sio zile ngawira za vita ama ukaliaji wa nchi."

Kifo hiki cha kishahidi kilikuwa ndio madhumuni ya msingi kwa sababu kwa hili, mtu anapata cheo cha kiungu kinachotamanika kimawazo, hivyo Imam (a.s.) alijitwalia njia hii ili kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, kuachana na ulimwengu huu na ili kuwa makini katika kumuelekea Allah alichukua njia hii.

**Fasili ya Tano:** Ni kwamba Imam hakukubaliana na mfumo wa utawala wa wakati ule, hivyo ili kupata madaraka, ili kukamata utawala huo yeye alileta mapinduzi haya ya kisiasa, kwani liko wazi kutokana na hotuba na mahubiri yake kwamba hakufurahishwa kabisa na mamlaka hayo kwa hiyo alichukua hatua ili kuushinda utawala huo. Ilikuwa ni kwa ajili ya kupata mamlaka tu na ili kutekeleza haki ndipo akachukua njia hii. Rai hii ni maarufu katika kundi la watu wasomi linganishi ambao wanajiona wenyewe kama wenye elimu ya kuweza kuelewa kiini cha Karbala.

**Fasili ya Sita:** Ni mageuzi ya ummah, hii ilikuwa ndio sababu ya msingi kwani watu walikuwa wamejiingiza



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 36 4/25/2018 11:01:27 AM

katika shughuli zisizo za kimaadili mno, hivyo ili kuwaongoza Imam (a.s.) alitwaa njia hii. Hii ni imani inayojulikana sana miongoni mwa watu wa zama hizi wakiwa na elimu sahihi na ya kweli. Sababu ikiwa ni hiyo katika ulimwengu wa sasa, mageuzi ya jamii ni jambo muhimu sana, na matendo yote mema na hata mabaya yanafanyika katika jina la mageuzi ya jamii, hivyo rai hii inakubalika sana siku hizi.

**Fasili ya Saba:** Falsafa ndio lile tukio la Karbala linamotegemea katika kipengele kimoja muhimu nacho ni:

أَمْرَ بِالْمَعْرُوْفِ وَ أَنْهَي عَنِ الْمُنْكَر

**"Amrisha mema na kataza maovu."**

Kadhia yote nzima ililenga kwenye lengo hili; muundo halisi wa *Amr bil Maaruuf wa nahi anil munkar* – kuamrisha mema na kukataza maovu, sio lile lililopo sasa hivi, hivyo Imam (a.s.) alijaribu kulifanyia kazi.

**Fasili ya Nane:** Ni yenye kupendelewa sana miongoni mwetu sote nayo hiyo ni kwa ajili ya kusamehewa kwa Ummah, Imam Husein (a.s.) aliona kwamba wahenga wangu hususan Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wamepata shida nyingi sana kwa ajili ya Ummah na kila wakati alipoulizwa juu ya sababu yeye alikuwa akisema ni kwa hali bora ya Ummah wangu, hata pale alipokwen-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 37 4/25/2018 11:01:27 AM

da Miraaj, yeye alimuomba Mwenyezi Mungu kupunguza uzito wa ibada juu ya Ummah kwa sababu alijua kwamba wakati utakuja ambapo Ummah utahisi kuelemewa na Swala hivyo alimuomba Mwenyezi Mungu kupunguza idadi ya swala za kila siku.

Kadhalika Imam Husein (a.s.) alidhani kwamba sasa kwa vile Ummah umo ndani ya kuelemewa na mizigo mingi, yeye alijua kwamba watu hawawezi hata kuswali swala mara tano, hivyo Husein (a.s.) alifikiri kwamba kwa nini asitoe muhanga ili kwamba Ummah wangu usiadhibiwe kwa ajili ya kutomuabudu Mwenyezi Mungu kama inavyotakikana. Hebu natudhanie kwamba kama vile tu Imam Ali (a.s.) alivyosema: "Ummah huu umenifedhehesha sana kiasi kwamba wameanza kunilinganisha na wengine;" je Imam Husein (a.s.) hatasikitika kwamba tumemfedhehesha kwa kiasi kwamba tumeanza kumchukulia yeye kama kafara kwa ajili ya dhambi!!!!!!! Fidia kwa utendaji maovu wetu!!!!

Maelezo kama hayo yalikuwa yakizushwa wakati wa nyuma kuhusu mitume wengi kutoka kwenye Ummat zao. Hivyo kwa hili tunasema sasa kwamba Imam (a.s.) amelipia matendo yetu, sasa tuko huru kufanya lolote tunalotaka na hakutakuwa na vizuizi juu yetu!



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 38 4/25/2018 11:01:27 AM

Sasa hebu tuiangalie ile "*Ashra Mubashira*" (ufunuo kwa ajili ya watu kumi). Ashra Mubashira, kwa mujibu wa riwaya ndani ya vitabu vya ndugu zetu Sunni ni tukio ambapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliorodhesha majina ya watu kumi kati ya masahaba zake kama waliohakikishiwa kuingia Peponi. Sisi hatukubali wala kuamini juu ya wazo hili kwa vile Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwapa hati na wao walilidai hilo wao wenyewe, na haiwezekani kwa mtu (mwenye kuweza kukosa) kutangazwa duniani humu kama mtu aliyebarikiwa. Kwa upande mwingine, sisi wenyewe tunasema kwamba kila mtu wa kawaida miongoni mwetu (Shi'ah) amebarikiwa na kuhakikishiwa kwa ajili ya pepo kwa sababu Imam (a.s.) ametoa kafara kwa ajili ya matendo yetu, hili sio sahihi, kwani kama tunajichukulia wenyewe kama tuliothibitishwa kwa ajili ya pepo, basi tunapaswa kuwafikiria hivyo na wale Ashra Mubashira vile vile.

**Maoni ya Tisa:** Ni pale watu wanaposema kwamba Imam (a.s.) hakulifanya hili, hivyo kwa nini kumhusisha nalo, yeye alikuwa ni muathirika tu, tukio lile liliIetwa kwake na watu wengine; hivyo msiseme kwamba aliuawa kishahidi. Hii pia ni imani potovu kwani ni jaribio la kuibadilisha Karbala ya Husein na kuwa Karbala ya Yazid.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 39 4/25/2018 11:01:27 AM

Akili inahitajika hapa ili kuelewa yote haya, kuwa mhusika wa Karbala (Karbalaai) sio kazi rahisi; walikuwepo mamillioni ya Waislam wakati ule lakini walipatikana Karbalaai 72 tu, na tofauti hii (ya kiidadi) inapatikana hata leo hii pia na itakuja kuwepo pia wakati wa kudhihiri kwa Imam-e-Hujjat (a.t.f.s.). Hivyo haja ya saa hizi ni kuelewa kwa akili, ufahamu na utambuzi. Mu'mini anazo sifa zote hizi na hawezi kughilibiwa. Imam Ali (a.s.) anasema ndani ya Nahjul-Balaghah: "Mimi sijiingizi mwenyewe kamwe kwenye hali ya kutuhumu au matatizo wala kufanya hilo liwezekane kwa wengine kufanya hivyo." Sisi ni wafuasi wa huyu Imam Ali (a.s.) na hatupaswi kufanya jambo lolote la makosa wala kusababisha hali kama hiyo kwa wengine ambayo inafanya kuwa rahisi kwao kutudhuru sisi.

**Fasili ya Kumi:** Hii inafahamika vizuri miongoni mwa ndugu zetu Sunni kwa sababu wanaamini katika wale makhalifa wanne, baada yao ni wachache tu wanaoamini kwa Imam Hasan (a.s.) kama khalifa wa tano, wengine wanamchukulia Amiir-e-Shaam kama khalifa wa tano, bado kuna wengine wanasema kwamba Khulafaur-Rashidun ilikomea baada ya Khalifa wa nne, halafu ikaanza zama ya ufalme. Mfumo wa utawala ulikuwa umebadilika kwa kulingana na wao. Katika Ushi'ah, mfumo wa utawala, ama iwe ni katika kip-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 40 4/25/2018 11:01:27 AM

indi cha uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au baada ya hapo; katika nyakati zote mfumo ulikuwa ni uleule na utabakia huo huo, unafahamika kama "Mfumo wa Imam na Ummah" yaani Kiongozi na Ummah. Ndugu zetu Sunni wanaamini kwamba mpaka wakati wa Khalifa wa nne, mambo yalikuwa yakienda vizuri na mfumo ulikuwa umesalimika kutokana na makosa lakini akaja Khalifa wa tano na akavuruga mfumo huo. Alifuata mfumo ule wa zamani lakini kidogo kidogo alileta mabadiliko ndani ya mfumo huo na hatimae mwishoni pale alipomfanya mwanawe kuwa mrithi wake, nia zake zikaeleweka wazi, hivyo hapa Imam Husein (a.s.) akachukua nafasi yake kufuta kosa hili na kurudisha ule mfumo wa "Imamat-wa-Ummah," – yaani "Mfumo wa Kiongozi na Ummah."

**Maoni ya Kumi na Moja:** Ni kwamba Bani Umayyah walianza desturi ya mauwaji ya kinyama ya halaiki ya Shi'ah; hili lilianza wakati wa utawala wa Amir-e-Sham Muawiyah na likaendelea kuongezeka siku hadi siku. Imam (a.s.) alimuonya Yazid wakati ule wa kusimamisha mauaji haya. Kuna barua kutoka kwa Imam (a.s.) zilizowasilishwa kwa Yazid ambamo majina ya Mashahidi wachache yanatajwa, kwa hiyo Imam (a.s.) hakuvumilia jambo hili na hivyo alisimama kulipiza kisasi. Kwa maneno ya siku hizi inaweza kusemwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 41 4/25/2018 11:01:27 AM

kwamba aliandaa maandamano marefu kutoka Madina hadi Karbala, kuonyesha kwamba kile kilichokuwa kinafanyika kilikuwa ni makosa, na ili kuyazima maandamano haya, kwa vile yalikuwa ni tishio ambalo lingeweza kuiangusha serikali, walizingirwa ndani ya Karbala na kila unyama ulioweza kutendwa ulifanyika hapo kumsimamisha Imam Husein (a.s.) dhidi yao. Wengi waliuawa kishahidi na waliobakia wakachukuliwa mateka, ingawa picha hii haijulikani vizuri sana kiulinganishi lakini bado imenukuliwa na wanahistoria wajuzi na wanafalsafa.

**Wazo la Kumi na Mbili:** Ni kwamba Muawiya alikuwa akitumia kutoa hotuba za kumshutumu Imam Ali (a.s.). Wazungumzaji wanaofahamika vyema wa daraja la juu kabisa walitumika kwa lengo hili. Imam Husein (a.s.) alifikiri kwamba kwa hili jina la familia ya Mtukufu Mtume litapotea kwa haraka sana. Hili lilikuwa kwa kiasi kwamba wakati Hadhrat Ali (a.s.) alipopigwa dharuba mnamo mwezi 19 Ramadhani, watu walishangaa kwa kiasi kwamba kuwepo kwake Imam pale msikitini kulikuwa ni mshituko.

Kwa hiyo ili kulizuia hili na kudumisha hadhi ya familia yake, Imam Husein (a.s.) alichukua hatua kali madhubuti.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 42 4/25/2018 11:01:27 AM

**Wazo la Kumi na Tatu:** Linaeleza kwamba, baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) watu walianza kwenda kuelekea pande za upotovu. Wakati wa Imam Husein (a.s.) mwelekeo wa dini ulikuwa ni mgeni kabisa, na yeye alipata hofu kwamba dini ya Uislamu itakwisha mara tu. Hivyo ili kuiweka dini hai aliamua kufanya mageuzi haya.

**Maelezo ya Kumi na Nne:** Yalikuwa pale Imam Husein (a.s.) alipoona kwamba; huu ni wajibu wangu wa kisheria, hivyo alilitekeleza tendo hili la Karbala. Hakukuwa na lengo jingine nyuma yake.

**Wazo la Kumi na Tano:** Linasema kwamba Imam (a.s.) alifanya hili kwa ajili ya kukamilisha wajibu wake. Kwa ajili ya ukamilishaji wa uthibitisho (Hoja), ili kwamba vizazi vijavyo viweze kwa mara nyingine tena kupata mamlaka yale yale ya zamani katika Makka ambayo Bani Hashim walikuwa nayo hapo mwanzoni. Bani Umayyah walitaka kuchukua kisasi, hivyo Karbala ilikuwa ni kulipiza kisasi tu kwa Yazid kutoka kwa Bani Hashim, kwa vile babu zake waliuawa katika vita vya Badr.

Hili linafanywa na wale wanaojaribu kuua mwelekeo wa kidini wa Karbala na kuuwasilisha tu kama mgogoro baina ya makabila mawili. Na kama ushahidi



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 43 4/25/2018 11:01:27 AM

wa kuthibisha maoni yao walisema kwamba wakati wowote Ali (a.s.) alipopigana, yeye alipigana na Bani Umayyah, hakuwahi kamwe kupigana na mtu mwingine yoyote. Hili lilikuwa ni kiasi tu cha kudunisha akili zisizo na hatia.

**Wazo la Kumi na Sita:** Hili ni la ajabu, linalopendwa na wasiokuwa Waislamu; linasema kwamba Imam Husein (a.s.) alifeli katika kutafsiri hali ya kisiasa kwa usahihi na kwa maneno mengine, ilikuwa ni uborongaji wa kisiasa uliofanywa na yeye. Hivyo aliuawa kishahidi. lakini yeyote yule aliyetoa maelezo haya ni mjinga kwa sababu hajui kwamba Imam Husein (a.s.) alikuwa akitambua Shahada yake kabla ya kuanza safari yake yenyewe.

**Wazo la Kumi na Saba:** Ni kwamba Husein (a.s.) aliona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliuonyesha Ummah wake njia nyingi za kupatia thawabu, lakini zote zilikuwa zipatikane kwa kupitia taabu na matatizo, hivyo yeye alitwaa njia kwa ajili yao kupata thawabu kwa urahisi sana, yaani: "Mimi nitauawa kishahidi nanyi mtapaswa kuomboleza juu ya kifo changu ili muweze kulipwa thawabu."

Ma'asumin (a.s.) wamesema: "Kama chozi moja litadondoshwa juu ya Husein (a.s.), basi Jahannam



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 44 4/25/2018 11:01:27 AM

itaharamishwa juu ya jicho hilo." Usemi huu umetafsiriwa vibaya na wanafalsafa na walilifanya hili wazo la kwamba kuomboleza tu peke yake kunatosha juu ya kupata thawabu.

**Wazo la Kumi na Nane:** Ni kwamba kusimama huku kulikuwa na idadi kadhaa ya malengo, ni mkutano, mkusanyiko, ni hatua pana yenye sababu chungu nzima na zote zilikuwa yeye amezipata. Kwa kifupi Imam alilengea hatua yake hii juu ya "Haki."

Hamasa yake ilikuwa ni kuweka hai uadilifu. Hivyo maelezo yote yale ambayo hayapo karibu na sababu hii yanaweza kufutiliwa mbali. Yeye alionyesha pia kwamba haki haina ukomo, mtu lazima aifuate kwa kiasi kwamba asiweze hata kujali juu ya maisha yake binafsi.

Haya ndio yale maelezo yote yanayofahamika vema, lakini kuna mengine mengi zaidi ya hayo. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani Ashuraa imezungumziwa. Kuwa na athari juu ya Ashuraa mtu lazima atengeneze mtazamo kuhusu Ashuraa ili kwamba tuweze kupiga mbizi kwenye bahari ya Karbala, tunatoka kwenye maisha haya tulivu na ya anasa na kujitosa kwenye awamu ya uhangaikaji kama Shahiid Mudhafar Kirman ambaye maisha yake yalikuwa ni kigezo cha uhangaikaji



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 45 4/25/2018 11:01:27 AM

kwa sababu yeye aliielewa ile falsafa halisi ya 'Qayam-e-Imam Husein' – Mageuzi ya Imam Husein (a.s.).

## MATATIZO KATIKA KULICHANGANUA TUKIO LA KARBALA

Kutokana na maelezo yaliyopita, ni dhahiri kwamba kuna umuhimu kwa sisi kuchanganua yale mageuzi ya Imam Husein (a.s.). Sio kwamba mageuzi yenyewe yanahitaji uchanganuaji wetu, bali ni sisi ambao tunahitaji kuyachanganua mageuzi haya. Bila ya uchambuzi huu sisi hatuwezi kukifikia kina chake, hiyo iwe ni leo ama kesho. Ni jambo ambalo haliwezekani kwamba bila ya uchambuzi huu mtu anaweza kwa kweli kuifahamu hoja ya kimantiki kwa ajili ya mageuzi haya. Umejionea mwenyewe kwamba tangu wakati ule wa mageuzi yenyewe hadi leo hii kila mtu ametoa maelezo tofauti juu ya sababu ya mageuzi haya kutegemeana na mitazamo na uelewa wao. Vile vile hatuwezi tukadai kwamba bila ya kujali juhudi zote hizi za kielimu na kitafiti, sisi tumeelewa sawasawa ule uhalisia wa mageuzi haya. Kwa upande mwingine ni muhimu kwamba tuwe tunatambua baadhi ya uchambuzi wake na kwamba tuna uelewa fulani kuhusu uhalisia wake na ule moyo ambao kwawo huo hili lilitokea. Hata hivyo,



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 46 4/25/2018 11:01:27 AM

kwa upande mwingine tena tunakabiliwa na matatizo kadhaa makubwa katika kutafsiri matukio ya namna kama hii.

## TATIZO LA KWANZA – MAONI BINAFSI:

Nitawasilisha mbele yako la kwanza kati ya matatizo kama hayo ambalo kwa kweli lenyewe ni msiba mkubwa kwa haki yake. Tatizo ni kwamba kwa tukio kama la Karbala, ambalo lilikusudiwa kuwa la hadhara na limekuwa maarufu miongoni mwa watu, linakuwa ni muathirika wa maoni ya watu. Wakati tukio linapokuwa la wazi kwa kiasi kama hicho, basi linakuwa limeanikwa kwenye uchunguzi wa ummah na linakuwa ni eneo la maoni ya ummah na mitazamo ambayo huongezwa kwenye tafsiri yake.

Hebu tuliweke pembeni tukio la Karbala na tuangalie jambo jingine ambalo pia ni maarufu na ni somo la uchunguzi wa ummah, ambalo matokeo yake nalo pia linapatwa na matatizo hayo hayo. Mfano unaweza kuwa ni dini yenyewe kwa sababu dini ni kwa kila mtu na wala sio kwa kundi maalum, ama la mtu binafsi, bali ni kwa ajili ya watu wazima na vijana, wanaume kwa wanawake; kila mtu, kizazi kilichopita, kile kilichopo sasa na kizazi kijacho baadae. Inahusiana na kila kitu



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 47 4/25/2018 11:01:28 AM

na kila mtu, hivyo ni jambo la kawaida. Hii ndio sababu ya kwa nini pale panapokuwepo na kazi ya kidini ambayo inatakikana basi tunatumia maneno "mimi sio mmiliki wa dini." Au "Yeye sio mmiliki wa dini." Hili ni sahihi pia, ukweli ulivyo ni kwamba dini ni kwa ajili ya kila mtu na hakuna mtu mmoja anayeweza kuwa ndiye mmiliki wake na mwangalizi wake.

Qur'ani pia inatumia maneno haya هُدًى لِّلنَّاس "*Huda lil-Naas*" yenye maana ya 'muongozo kwa wanadamu wote,' lakini inategemea juu ya juhudi na uwezo wa kila mtu binafsi juu ya ni kiasi gani cha muongozo anachoweza kujipatia na kutimiza wajibu wao wa kidini. Kwa vile dini ni kwa ajili ya kila mtu, ni kawaida na sote tunatambua kwamba imekuwa ni muathirika wa mambo chungu nzima. Kama isingekuwa ni ya kila mtu basi huenda pengine isingekabiliana na matatizo yote haya. Kuna taaluma nyingi na ujuzi mwingi ambao sio kwa ajili ya kila mtu, na kwa vile sio za kawaida, basi hazikabiliani na matatizo yoyote. Kwa mfano kuna kule kusomea hisabati, ambako sio kwa kila mtu, ni kundi maalum tu linalojifunza hisabati na ambalo lina upendeleo na somo hilo.

Kwa hiyo utaona kwamba hakuna mabishano wala ugomvi wowote. Kuna madhehebu katika Dini lakini

hakuna madhehebu katika Hisabati. Profesa wa hisabati kamwe hatatoa hukumu juu ya kuuawa kwa profesa mwingine kutokana na tofauti katika nadharia fulani au kwa kusema kwamba nimeiandika fomyula hii kwa njia hii na yeye ameiandika kwa njia ile na hivyo yuko nje ya mzunguko. Hili halikufanyika siku zilizopita na kama halitokei katika siku zijazo basi watu watafikiria kwamba profesa huyo amepagawa. Madhehebu hayawezi kukubalika katika Hisabati, Fizikia, Kemia na katika mambo mengi mengine.

Sasa katika siasa kuna makundi na madhehebu pia, na yale matatizo ambayo Dini inakabiliana nayo vilevile siasa inakabiliwa nayo kutokana na sababu zile zile kwamba siasa nayo ni jambo la kawaida na kwa watu wote. Hisabati ni namna nyingine, ambamo watu binafsi wanaojitaalimisha kipekee ndani yake wanakuwa na uwezo wa kuelewa hisabati hizo na wanaelewa jinsi ya kupata ujuzi kwa ajili yake, jinsi ya kuitumia na kama kuna tatizo linalojitokeza basi wanajua jinsi ya kulitatua tatizo hilo. Hata hivyo, mtu wa dini au mwanasiasa hafikirii namna hiyo, hii ni kwa sababu hakuna ujuzi katika hili bali tofauti pekee ni kwamba haya mambo mawili yanahusiana na ummah wote na ummah pia ni mshiriki katika hayo. Sasa kama kitu kinahusiana na ummah basi vipengele kadhaa vinabidi kutazamwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 49 4/25/2018 11:01:28 AM

na mambo kadhaa yanahitaji kujadiliwa. Ummah ni mshiriki wa namna kwamba haufikirii kitu chochote, ule upande mwingine unaangalia kila kipengele cha manufaa kwa ajili ya ummah lakini ummah haufikirii lolote kati ya malengo yake. Matokeo yake hili, jambo ambalo ni la ummah au la kawaida kwa kweli kabisa litapitiwa na mabadiliko, ugeuzaji, na mabishano kwa sababu maoni na mtazamo wa ummah vinabadilika wakat wote kutoka rangi moja kwenda nyingine. Hivyo kuwa la ummah tu kunaweza kuwa ni hatari kwa mambo fulani. Kama unataka kuhifadhi kitu basi ni bora kuhakikisha kwamba ummah hausikii chochote chenye kukihusu kitu hicho. Lakini kwa upande mwingine lazima kwa siasa na dini kuwa za ummah.

Haiwezekani kuiweka dini kwenye pembe ya chumba, ndani ya maficho au ndani ya chuo cha kidini. Hata hivyo, juhudi zimefanyika za kuiondoa dini mbali na ummah na kuikomeshea kwenye mipaka ya shule za kidini au misikitini na sio kuiruhusu kuingia mitaani kwetu na kwenye nyumba zetu lakini hili halikufanikiwa. Kumekuwepo na juhudi kubwa za kujenga majengo makubwa na halafu kuiwekea mipaka dini ndani yake hivyo hakuna anayeingia kwenye majengo haya, lakini dini ina nguvu na uwezo wa kuvishinda vihunzi hivi na kufikia moyo wa watu. Ingawa hili ni zuri lakini basi



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 50 4/25/2018 11:01:28 AM

linasababisha tatizo vile vile. Dini ni jambo la ummah kwa kila, chanzo cha muongozo kwa ajili ya kila mtu. Sasa dini imekuja kwa ajili ya kila mtu lakini haiwezekani kwamba watu mmoja mmoja hawawezi kuiathiri. Dini inaathiri watu lakini pia watu nao huiathiri dini. Siasa nayo vilevile ni hali kadhalika, inamuathiri mtu wa kawaida naye mtu wa kawaida anaiathiri siasa. Sasa kama ukichunguza utaona kwamba matatizo makubwa yaliyoibuka kwenye dini ni kwa sababu ya yenyewe kuwa ya ummah na haiwezekani kuupuuza ummah kirahisi tu. Maoni ya ummah, manufaa, furaha ni mambo muhimu wakati mwingine kunakuwa na migogoro baina ya dini na ummah na matokeo yake washiriki wote wanahitaji kuonekana kwamba ni watu wa dini na wa ummah halikadhalika.

Kuna mifano kadhaa katika historia ambamo utaona kwamba dini imekubaliwa kwa ajili ya ummah na wakati mwingine ambapo ummah umekubaliana kwa ajili ya dini. Hii ilikuwa ni namna tu ya sampuli ya kuthibitisha kwamba kama ukiangalia ndani ya dini basi utagundua kwamba kuna matatizo mengi yanayoibuka kwa sababu tu ya kuwa dini ni ya ummah. Kadhalika, Qur'ani pia inakabiliana na matatizo. Vitabu vingine vilivyofanya maalum ambavyo sio vya ummah huwa havina matatizo. Kwa mfano kwa vitabu vya



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 51 4/25/2018 11:01:28 AM

kompyuta hakuna ubishani navyo kwa sababu ni vya kushughulika na kundi maalum la watu. Kundi hilo la watu linafikia hatua ambapo wanaelewa vitabu hivi, hivyo kunakuwa hakuna migogoro.

Hata hivyo, dini sio tu kwa ajili ya mtu ambaye yuko tayari kuikubali lakini vile vile ni kwa ajili ya mtu ambaye hayuko tayari kuikubali. Mtu ambaye anayo haki ya kueleza maoni yake kuhusu dini anafanya hivyo, lakini kadhalika asiyekuwa na haki ya kufanya hivyo bado anafanya hivyo.[1] Hata hivyo, kwa kweli kungekuwa na sheria kwamba ingawa dini ni kwa ajili ya kila mtu, lakini ili kutoa maoni kuhusu dini lazima kuwe na sifa maalum za kiuwezo. Unaweza kutoa maoni yako lakini ni pale tu unapokuwa na ujuzi na uwezo wa kuyaelezea kama katika taaluma nyinginezo.

Katika dini na siasa hili huwa halitokei, hakuna hata mmoja anayeangalia endapo kama wanayo haki ya kutoa maoni yao au hapana. Tunayatoa maoni haya, tunahukumu masuala, sisi sote tunajifanya kuwa Mujtahidi (wataalamu wa utafiti wa masuala ya kidini) na

1. Mfano wa hili unaweza kuonekana wazi katika mtandao wa Intaneti. Kuna mabaraza ya maongezi ya wazi kabisa, makundi na tovuti ambamo watu kutoka kila mahali ulimwenguni pote wanakaa na kupitisha maoni yao juu ya mambo ya kidini. Wale ambao wala hawajui misingi ya dini wanakaa hapo, wakitoa mawazo na maoni yao na kuwashutumu wanachuoni, mafaqihi na wale viongozi wakuu wa masuala ya kidini.

Mafaqihi (wanasheria wa kidini). Kila watu wana dini yao. Hivyo jambo lolote ambalo ni ummah lina matatizo hayo hayo, kama yale ya Karbala.

Mageuzi haya pia ni ya ummah na kwa hiyo kwa kuwa kwake ni ya ummah vile vile yamehatarishwa kwenye matatizo kadhaa. Karbala ni kwa ajili ya kila mtu, haina mwenyewe maalum na Imam Husein (a.s.) yeye ni kwa ajili ya kila mtu na kwa hivyo hili tukio la Karbala pia linahusishwa na kila mtu. Sasa suluhisho sio kulifanya ni la baadhi ya watu tu ili kuepuka maoni yasiyo sahihi, linapaswa libakie ni la ummah lakini lazima kuwe na kigezo cha sifa stahilifu na taratibu za ni lini mtu anakuwa na uwezo wa kutoa maoni. Hii ndio sababu k Kila mmoja wao alishangazwa kuhusu wamba matukio kama la Karbala yamelengwa na kauli, maoni na utambuzi. Kila mmoja ana mtazamo na maoni tofauti. Mtu ambaye ana jazba ameiangalia Karbala kutokana na mtazamo wa kijazba. Wengine wenye mtazamo wa kifalsafa wameiangalia Karbala kwa falsafa. Muelekeo na maelekezo yoyote yawayo ya mtu, basi mtu huyo ameingalia Karbala kwa muono huo.

Hivyo tatizo kubwa sana ambalo linajitokeza ni kwamba, pale mtu anapojaribu kuelewa jambo, la kidini au lisilo la kidini, katika hatua ya kuelewa huwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 53 4/25/2018 11:01:28 AM

yeye anapata uwezo wa kufanya au kufikia maoni yake mwenyewe pamoja na hitimisho.

## TATIZO LA PILI – SILIKA MBAYA - ZA KIOVU

Mwenyezi Mungu ameweka uwezo ndani yetu wa unyambuaji, utambuzi na mahitimisho, ambao kimsingi sio wa kimachafuko, hata hivyo kwa sababu uwezo huu haukuzoeshwa na kulelewa vizuri unafanya kama mtoto mtundu, shetani mdogo. Hakuna mtoto aliyeumbwa mtundu, kila mtoto alikuwa msafi, lakini kila mtu amewahi kuwa mtoto, hata wale ambao kwa sasa wako makini sana nao walikuwa watundu. Watoto wote leo hii watakua na kuwa makini na wakweli, wanakuwa wa kishetani kutokana na kukosa muongozo kutoka kwa wazazi, na mazingira ya kifamilia kutokuwa ya kufaa. Sio kwamba mtoto aliumbwa na tabia mbovu lakini kutokana na sababu kadhaa mtoto huyo hugeuka kuwa mnyama. Sio huyo mtoto kwamba kwa kweli ni mtundu bali mazingira yake ndio yamemfanya kuwa hivyo, na mtoto huyo huyo kama atalelewa vizuri anaweza pia kuwa mwema.

Halikadhalika ndani yetu sisi sote kuna mazingira ambayo yamo ndani. Allah swt. ameumba mazingira safi halisi kabisa ndani yetu na mazingira haya yanatu-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 54 4/25/2018 11:01:28 AM

saidia sisi kwa uwezo wa kuelewa na uwezo huu unatusaidia sana sisi kwa kiasi cha kufikia hatua ya kufanya maamuzi na uvumbuzi. Angalia karibu yako utaona kwamba kuna mambo mengi sana ambayo yalikuwa hayajavumbuliwa na ambayo kwa sasa yamevumbuliwa. Haya yote ni matokeo ya uwezo wa ubunifu ambao umewekwa ndani yetu sisi. Vinginevyo tungekuwa bado tunasafiri kwa ngamia, na bado tunakula wanyama wa porini. Huu vile vile ni uwezo wa uumbaji, ambao kwa hali halisi ni uwezo wa kufikiri, uwezo wa ufahamu. Hivyo kuna uwezo wa uvumbuzi uliowekwa ndani yetu.

Hata hivyo hii ni kwamba tu pale unapokomaa ndipo basi unavumbua, lakini usipoongozwa, badala ya uvumbuzi wa kujenga, unaanza kufanya uovu. Uwezo huu uko ndani yetu sote, maasum na wasio maasum, wasomi na wasiosoma, mtu anayekaa mjini na mtu aliyeko kijijini, mtu wa wakati uliopita ama wa zama hizi za sasa, mtu wa dini na asiye na dini, kila mtu anao uwezo huu. Kama ukipewa muongozo sahihi unaofaa unaanza kuvumbua, vinginevyo utakwenda upande potovu wa kimakosa. Matatizo yote yanakuja kwa sababu ya hili na tatizo la kwanza ambalo hili huliibua liko ndani ya hatua ya uelewaji wa jambo. Pale tunapojaribu kulielewa jambo, uwezo huu

unakuwepo na huwa unaanza kufanya uovu. Inasemekana kwamba Shetani wakati wote anatafuta fursa. Mtoto anahitaji mazingira kuonyesha fitina zake; yeye mwenyewe peke yake asingeweza kufanya hivi ndani ya chumba kitupu kwa sababu hamna starehe. Uwezo huu wa uvumbuzi na kufikiri ambao haukuendelezwa vyema nao pia unatafuta fursa, haufanyi uovu wakati wote, unapata wasaa wakati unapojaribu kuelewa jambo fulani. Unakusubiri wewe uanze kufahamu na kutambua, mara unapofungua kitabu kizuri nao unajiandaa kufanya kazi yake ya uovu. Kama ukisoma mistari miwili na unachoka na unaanza kuitafuta rimoti ya **TV** ili kuangalia picha ya sinema. Mawazo haya yanaibuka kutoka ndani na tunakuwa hatujui ni wapi mawazo haya yanakotokea. Kwa kweli hizi ndizo kazi za Shetani, lakini ni shetani yupi? Shetani yule aliyeko nje ama yule aliye ndani? Glasi hii imevunjika, je ni nani aliyeivunja? Je, ni yule shetani aliyeko nje – Ibilisi au shetani aliyeko ndani – mwanao? Glasi imevunjwa na shetani lakini shetani huyo ni mwanao mwenyewe aliyelelewa visivyofaa, shetani ambaye ulimfanya kuwa shetani.

Kadhalika inasemekana kwamba shetani alinishawishi mimi kufanya hili, lakini hakuwa ni ibilisi bali ni yule shetani aliyeko ndani yako, ambaye ameku-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 56 4/25/2018 11:01:28 AM

zwa kama matokeo ya kukosa muongozo na mafunzo yanayofaa. Hili ndio tatizo kubwa la pili katika hatua ya uelewa na ufahamu, ambalo linaonyesha uovu wake. Sasa uovu, wenyewe ni tofauti, watoto wanaotoka vijijini watafanya uovu kwa namna ya kishamba ambapo wale walioko mjini watafanya kwa namna na njia tofauti. Sasa uwezo huu unafanya kazi yake katika fikra, unakufanya wewe ufikiri kimakosa, na matokeo yake mawazo ya kiovu huibuka upande wako kutoka ndani. Hili ndio tatizo katika kutafsiri jambo kama Karbala.

Wakati wote tunapofikia hatua katika kuielewa dini, Qur'ani au kitu chochote kinachohusiana, na tukaanza kutafakari; moja ya njia ambayo unaitumia katika kufanya kazi yake ya uovu ni kutuzuia sisi kutafakari hasa na kulifanya jambo lenyewe kuwa lenye kusumbua. Hata hivyo, sio mbinu ile ile inayotwaliwa kila wakati na shetani huyu wa ndani, wakati mwingine inaweza kukutaka wewe kusoma pia. Kama ilivyosikika kwamba mtu mmoja alikuwa amelala wakati shetani alipokuja kumwamsha kwa ajili ya swala ya Al-Fajr. Mtu huyu alishangazwa kwa sababu inafahamika kwamba shetani anakutaka wewe ulale usingizi. Alimuuliza shetani kwamba kwa nini unaniamsha, najua kuwa kuna namna ya uovu ndani yake! Ingawa silielewi hili, ni dhahiri linaonekana kama ni tendo jema. Shetani anasema,

usijali, mimi ninafanya jambo zuri kwa ajili yako, vinginevyo ungeikosa swala yako. Mtu huyo anasema hapana, ingawaje ni tendo jema, lakini kwa sababu ni kazi ya shetani, basi kuna kitu cha kutilia mashaka ndani yake. Imam Khomeini (r.a.) alikuwa kila mara akisema kwamba wakati wowote Marekani itakapoanza kuwa na wema juu yetu, basi uiangalie kwa msimamo wenye mashaka, wakati wowote unapopokea ujumbe wa wema kutoka kwa bwana huyu wa mashetani, basi usiwe na furaha moja kwa moja bali uwe umechanganyikiwa sana kwa sababu kuna uhakika wa kutokea kuwa na jambo la kiovu sana kuhusu wema huo. Kama kukiwa na ujumbe wa uovu kutoka kwao, hapo wewe tulia kuhusu hilo na kuwa na uhakika kwamba ni uovu wao ambao umepata mwonjo. Kwa hiyo yule mtu ambaye alikuwa ameamshwa na shetani anasema kwamba sitahitaji tena swala yangu hadi utakaponieleza sababu ya ni kwa nini umeniamsha kama hivi. Shetani anasema kwamba sababu ilikuwa kwamba wewe ni mtu unayewahi sana kuhusiana na kutekeleza swala zako kwa wakati. Una fahari juu ya hili pia kwamba wakati wote wewe unatekeleza swala zako kwa wakati na unawaangalia watu wengine kwa kujigamba kwamba wao wanachelewa na kuziswali baadae kidogo. Unajiona wewe mwenyewe kuwa mbora juu ya wengine.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 58 4/25/2018 11:01:28 AM

Sasa, leo ulikuwa unachelewa na kama ungekuwa uamke baadae, swala yako ingekuwa imechelewa, na kwa sababu ya hilo fahari yako ingeumia na mimi sikutaka kiburi hiki kitoweke. Siku zote nilikuwa nikitaka wewe uwe na kiburi.

Unaona kwamba kuna maovu mengi sana yanayofanya kazi kiasi kwamba mwanadamu anapaswa kumuuliza shetani mwenyewe juu ya uovu wenyewe katika kitendo hicho. Hii inatokea, hakuna mtu ambaye ni mchamungu zaidi kuliko Mitume au Maimam hata hivyo, na wao wakati wote walikuwa wakizungumza na watenda makosa kwa upole na kamwe sio kwa kiburi. Kama umebarikiwa kwa muongozo basi mshukuru Mwenyezi Mungu swt. na usiwe na kiburi. Hiki ndio kiburi cha mwanzo. Shetani anawapenda sana watu kama hao ambao wanaufikia muongozo lakini bado wanakuwa na kiburi, yeye mwenyewe alikuwa kiburi. Ndani ya Qur'ani, Allah swt. anazungumza na shetani na anamuuliza kwa nini yeye hamsujudii Khalifa ambaye Allah swt. amemuumba na yeye anajibu kwamba yeye ni bora kuliko huyo Khalifa. Hivyo yeyote anayetamka maneno haya kwamba mimi ni bora kuliko wengine waliobakia basi huyo ni shetani. Unapaswa kuwa mnyenyekevu. Malaika hawakusema kamwe kwamba wao ni wabora bali wakati wote walimwambia Al-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 59 4/25/2018 11:01:28 AM

lah swt. kwamba – Wewe unajua vizuri zaidi. Hivyo Shetani huwa anafanya maovu mengi ya kutatanisha sana ndani yetu. Mmoja wa Shetani kama huyo ni ule uwezo wa kufikiri usioendelezwa na unaanza tu uovu wake wakati unapotaka kutafakari juu ya jambo fulani. Ameahidi kuhakikisha kwamba sisi hatupati kuelewa jambo vizuri kiasi inavyostahili.

Kama yule Ibilisi ambaye ameahidi kwamba atatushawishi sisi kufanya makosa, kadhalika nguvu hii imeahidi kuhakikisha kwamba hutaelewa jambo sawasawa. Kwa hiyo pale tatizo hili linapojitokeza linabadilisha yasiyo halisi kuwa ndio kweli na kuwasilisha hilo. Kuna tofauti kati ya mawazo.

Kuna mambo mawili unayoyajua ya maoni au masimulizi. Kuna tofauti kati ya maoni na masimulizi, wakati wowote nguvu hii inapoibuka ndani yetu inatengeneza fikra potovu ndani yetu. Unaweza kuwa umeona vitabu vya kihistoria ambavyo kwa hakika ni simulizi; historia imewasilishwa kwako kama simulizi. Historia ni uhalisia wa matukio lakini maoni na mawazo yameibadilisha kuwa simulizi. Mtu ambaye anaipenda simulizi anaweza akaifanya kuwa tamthilia, picha ya sinema. Wakati tunapoiangalia drama hiyo hatusemi kwamba hii ni simulizi ya kihistoria bali tunase-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 60 4/25/2018 11:01:28 AM

ma hii ndio historia yenyewe, hakuna tofauti. Dunia ya imani, dini na siasa iko namna hii, wakati wowote kunapokuwa na hatua kwa ajili ya kutafakari, wazo hili la kiovu linaonyesha kazi yake. Unaweza kuangalia kwenye milango mingi ya Uimam na Utume na utaona kwamba maisha ya watukufu hawa yamegeuzwa kuwa ni masimulizi, na ni watu wa dini na wanachuoni ambao wameongeza simulizi karibu na watu hawa kama ni historia. Hili limewapa kisingizio watu wengine kuijadili dini yetu kwa msingi wa simulizi hizi. Kwa mfano Imam al-Hujjat (a.t.f.s.), Imam Ma'sum, Khalifa wa Allah swt. amegeuzwa kuwa ni kioja na simulizi na simulizi za aina mbalimbali zinazosimuliwa kwa watu, wao wanafurahia kuzisikiliza.

Ni kupitia uwezo huu wa kufikiri kwamba Karbala nayo pia imeguswa, kwa vile historia sasa imegeuzwa kuwa simulizi na hili limefunguliwa kwa kila mtu kuingia ndani na kuelezea maoni yao. Kama mshairi aliyekuja kuandika shairi lake kuihusu Karbala kuonyesha mawazo yake nasi tuliyakubali kuwa ni historia. Sasa, kama tunakuja kutoa ufafanuzi, basi tayari mbele yetu kuna haya mawazo yaliyoundwa kibinafsi, ubunifu ambao unakuwa ni kikwazo kikubwa katika uchambuzi sahihi wa jambo lenyewe na hapo kuweza kufikia uhalisia wake. Ni vipi tutaweza kuufikia ukweli? Hili



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 61 4/25/2018 11:01:28 AM

ndilo tatizo kubwa kuhusiana na maoni ya ummah. Ni kusudio la msiba na balaa. Hatuwezi kuepuka kirahisi mwelekeo wa ummah kwa sababu haya yamekusudiwa kuwa ya ummah, lakini hii haina maana kwamba tunaweza kumpa mtu yoyote haki ya kuelezea hadithi kuhusu hilo, na kuelezea mawazo yake binafsi juu yake.

Kuna njia ya tatu, ambayo ndio njia sahihi na hii ni kuhakikisha kwamba ukweli unabakia kuwa ukweli kwa ajili yetu. Utaona kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) akiwa ni maasum, ambaye ni mwenye kutokukosea katika mawazo na kuelewa pia na sio katika vitendo tu. Yeye hawezi kuelewa jambo lolote kwa makosa, lakini bado katika du'a zake (s.a.w.w.) yeye anasema: "Rabbi Arinil ashyakimaha" – nionyeshe haki jinsi ilivyo. Kwa nini anamuomba Mwenyezi Mungu swt. amuonyeshe haki kama ilivyo? Ili kutoa uelewa wa mambo kama mambo yenyewe yalivyo na sio kama yanavyoonekana kuwa, sio yaonekane kuwa kama yako hivi kumbe yako vingine tofauti kabisa. Hii ni du'a kubwa sana ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambamo kuna somo kwa ajili yetu kwani yeye mwenyewe ni ma'sum na anayaona mambo kama yalivyo hasa na sio kama yanavyoonekana, lakini sisi tunayaona mambo kwa utofauti kama ni mambo mengineyo, ambapo kwa hali halisi yako tofauti na tuyaonavyo. Yeye



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 62 4/25/2018 11:01:28 AM

anatufundisha sisi kwamba, angalieni historia kama historia ilivyo, yaangalieni matukio kama yalivyo hasa, angalieni Qur'ani kama ilivyo, msiongeze maoni yenu binafsi, mawazo na dhana ndani yake.

## TATIZO LA TATU – MAONO YA MAWAZO FINYU

Tatizo la tatu katika tafsiri ya jambo kama Karbala ni kule kutojulikana. Kwa Karbala kuna kina kirefu sana juu yake kwamba hata kama tukichukulia kwamba kuna akili iliyo huru kutokana na uovu wa mawazo, bado kuna mawazo safi yanayohitaji kulinganishwa na kina cha tukio lenyewe vilevile. Wakati mtu anapokuja kuliona hili, basi kufikiri vilevile lazima kuwe kupana kama tukio lenyewe.

Kama ukiangalia kwa akili yenye hali ya kufungika kwenye tukio pana sana, basi hilo jambo pana litaonekana kufungika vilevile. Hili ni dhahiri, wala haihitaji ufafanuzi kama unaangalia kwenye mandhari pana sana kupitia kwenye tundu dogo, basi mandhari hiyo pana sasa itaonekana kuwa ndogo sana. Allah swt. ameuumba ulimwengu kuwa mkubwa sana, mkubwa kiasi kwamba haieleweki. Kilimia yetu (mkusanyiko wa vijinyota vingi kama wingu jeupe) ni sehemu tu ya mamillioni ya



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 63 4/25/2018 11:01:28 AM

kilimia. Katika kila kilimia kuna mamilioni ya nyota na sayari na mifumo na mfumo wetu wa jua na sayari zake ni mmoja tu wa mifumo kama hiyo. Dunia ni sehemu ndogo tu ya mfumo huu, ni ipi nafasi ya dunia katika kuilinganisha na ulimwengu? Juu ya ardhi hii hatuishi kila mahali, utakapomuuliza mtu kwamba wanaishi wapi, hatakutajia dunia, watatoa jina la sehemu wanayoishi, na mtaa wao. Kama mtu mmoja mtaani anakuuliza juu ya anuani ya makazi yako, utamtajia namba ya nyumba yako. Ndani ya nyumba hiyo tunaishia kwenye kitanda. Hebu sasa linganisha uwepo wako kwenye ulimwengu wote. Ili kuuelewa ulimwengu huu, sisi tunayo sehemu ndogo kama hiyo, na tunaagizwa kuuangalia ulimwengu. Yeye ameumba ulimwengu mkubwa kama huu, mimi nitawezaje kuuangalia ulimwengu huu, uchunguzi wangu utakuwa wa akili iliyofungika. Wakati tunapoangalia kitu kipana kwa hali ya akili iliyofungika, na kitu hicho basi nacho huonekana kuwa ni kidogo, lakini kama tutaangalia kitu kidogo kwa akili iliyopanuka basi hicho nacho kitaonekana kuwa ni kikubwa.

Karbala nayo ni kubwa na pana kama ulimwengu na ili kuiangalia tunahitaji mtazamo mpana sana, vinginevyo tutakapoingalia kwa akili finyu, basi itaonekana kuwa ndogo. Hivyo mtu anapokuja kuielezea Karbala, Qur'ani au dini basi anahitaji kupanua mtazamo wake.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 64 4/25/2018 11:01:28 AM

Hivyo ndani ya Qur'ani, Mwenyezi Mungu swt. anamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atazame kwenye ulimwengu huu lakini kwanza aendeleze upeo katika utambuzi. Je, Mwenyezi Mungu hakuumba akili pana huru ndani yetu?

Hata kwa mtu wa kawaida, Mwenyezi Mungu swt. anasema kwamba anapotaka kumuongoza mtu basi anaumba akili timamu huru ndani ya mtu huyo. Hali ya akili finyu itaongozea kwenye upotovu. Haiwezekani kwa mtu mwenye akili iliyofungika kuielezea Karbala, kwa hiyo ni muhimu kuongezea kwenye shaksia na mawazo yako huu upana wa maono kabla ya kujiandaa kuielezea Karbala na halafu utaona baadhi ya ukweli ndani ya Karbala, kisha utaiona falsafa ndani ya Karbala na kisha utauona ujumbe ndani ya Karbala. Kama unaungalia ukweli wa Karbala basi tengeneza ufahamu mpana.

Ufahamu kama huo ulikuwepo wakati ule Karbala ilipotokea. Wakati Ubaidullah bin Ziad alipoongea na Bibi Zainab (s.a.) na kushindana hapa, mtu mwenye akili iliyofungika anazungumza na mtu mwenye akili huru ya wazi, hivi ndivyo watu wenye akili zilizofungika wanavyofanya, wanashindana tu, hakuna upole ndani ya ndimi zao? Alisema katika namna ya kukashifu mbele yake na akamuuliza ulimuona vipi Allah swt.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 65 4/25/2018 11:01:28 AM

hapo Karbala? Jibu la Bibi Zainab lilikuwa vipi? "Nilimuona Allah kuwa ni Mzuri, Mzuri zaidi kuliko siku zote kamwe." Huu ndio ufahamu unaotakikana wakati wa kuiangalia Karbala, halafu kama Bibi Zainab (s.a.) tunaweza kuuona utukufu (*Jamaal*) wa Mwenyezi Mungu. Nini wanachokisema watu wenye akili zilizofungika?

Kama ukisikiliza visomo vya maombolezo (*marsiya* na *nauha*) vya watu wenye akili finyu, mara nyingi sana utakutana na maneno haya: "Hapakuwa na mtu wa kumpa Husein (a.s.) na familia yake maji, Mwenyezi Mungu hakumpatia maji, hapakuwa na mtu wa kukuokoa wewe, Mwenyezi Mungu hakukuokoa, ulikuwa wapi ewe Mwenyezi Mungu wakati ule?"

Vifungu hivi vya maneno vinamuumiza kila mtu ikiwa ni pamoja na hao Mashahidi wenyewe wa Karbala na hata lengo lenyewe la Karbala. Angalia lugha yenyewe, halafu sasa angalia lugha ya mtu mwenye ufahamu mpana. Alhamdulillah, yeye Zainab (s.a.) anamshukuru Mwenyezi Mungu swt. kwa kuwachagua wao kwa jukumu hili, asimpe mtu mwingine yeyote fursa (*Tawfiiq*) hii ya kulitimiza hili. Bila ya utambuzi huu huwezi kuiona Karbala na kuuona Utukufu wa Mwenyezi Mungu. Je, umewahi kulisikia hili likisem-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 66 4/25/2018 11:01:28 AM

wa kamwe? Lakini hivi ndivyo anavyosema Bibi Zainab (s.a.)! Yeye aliiangalia vipi Karbala? Kwa utambuzi gani? Yeye atasema: "Mimi ni binti ya nani? Ni kwa ajili ya nani ilishuka aya hii ya Qur'ani? Mimi natokana na familia ile ambayo kwayo Mwenyezi Mungu swt. aliumba upana ndani yao." Kama ikiangaliwa kwa mtazamo huu, basi utauona Upweke wa Allah (*Tawhiid*) ndani ya Karbala, na huu unawasilishwa kila mahali. Hivyo utauona tu ukweli wa Karbala kwa utambuzi mpana kama huo. Karbala ni bahari yenye kina kirefu sana na iliyochafuka kwa mawimbi makubwa sana ambayo kwa kupiga mbizi mara mbili au tatu hawakuweza kuzipata zile tunu zilizofichikana humo. Bahari hiyo inazo hazina nyingi na haiwezekani kwa kila mtu kuzama kwenye kina cha bahari hii na kupata hazina hizi kutoka chini ya kina chake. Hivyo utaona kwamba wale ambao wameisoma Karbala, wakajifunza falsafa yake; mwenendo na kanuni zake, wao wanaweza kufanya hivyo.

Wakati ule pia, watu walikuwa wanachukua vitu kutoka Karbala, mtu mmoja akichukua kilemba cha Imam Husein (a.s.), mwingine akichukua pete yake, mwingine viatu, na wengine walikuwa wanachukua vitu kutoka ndani ya mahema. Mtu mwingine aliwapa watoto maji na akajipatia tendo jema, mwingine alim-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 67 4/25/2018 11:01:28 AM

saidia mtu mwingine na akapata baraka. Na wezi nao walipata chochote kitu; wauaji walipata chao kitu na hata watazamaji nao pia walipata kitu chao. Wafuasi wa Karbala vilevile walipata chochote, wengine walipata kuomboleza, wengine walipata baraka kwa ajili ya ulimwengu ujao, kwa kutegemea uwezo wa mtu mhusika, walichukua hayo kutoka Karbala.

Vilevile katika karne hii mtu fulani, kwa kuelewa kuhusu Karbala naye pia amechukua kitu fulani pamoja naye. Utaona kwamba kurukia ndani ya bahari hii yenye kina kirefu pia kunahitaji ujasiri na mtu huyu mashuhuri Imam Khomeini (r.a.) amesema tunacho kitu, hii dini, huu utawala, huu udhibiti, hii Wilayat, sisi ni kitu cha maana mbele ya mataifa makubwa, na hayo mataifa makubwa sasa wametuchoka. Tumelipata wapi hili? Yeye anasema: "Kutoka Karbala," kutoka kwa wale waliokuwa Karbala, sio taifa la Irani au mtu yoyote bali ni Karbala iliyotupatia sisi, Sio kwamba milango ya Karbala iko wazi kwa wachache na imefungwa kwa wengine, unaweza kupata kila kitu kutoka Karbala, ikiwa utakuwa na moyo uliojaa mapenzi utapata hazina.

Chochote unachokitaka unaweza kukipata kutoka pale; inategemea tu juu ya yule mtu anayeomba



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 68 4/25/2018 11:01:28 AM

kwamba anaomba kitu gani. Unaweza kuona kwamba hata wale waporaji walipata kitu fulani, na wale wezi vilevile, hakuna aliyerudishwa mikono mitupu, wanahistoria, wanachuoni, yeyote aliyeingia katika kutafuta alipata kitu. Imam Khomein (r.a.) naye pia alipata kitu kutoka Karbala.

Katika karne hii mapinduzi makubwa kama hayo yametolewa. Madhali kuna mtu wa kuchukua kutoka kwao, kutakuwa na mfano ambamo mtu yeyote atakataliwa. Kama mtu anataka kuitafsiri (karbala) basi anapaswa kuongeza muono wake. Wakati nguvu ya macho yetu ya kuona inapodhoofika, hapo tunatumia mawani kuiboresha. Kwa mfano mawani ya jua, lengo lake pekee ni kupunguza mwanga, popote pale penye kuzidi kwa mwanga basi mawani ya jua yatapunguza mwanga huo. Sababu ya kwa nini tunatumia mawani ya jua ni kwamba hatuna uwezo wa kuvumilia mwanga. Kadhalika utambuzi wetu unaweza ukapofushwa na kuzidi kwa mwanga kutoka kwenye tukio kama la Karbala. Hivyo unashusha pazia mbele ya macho yako ili kwamba ule mwanga wa Karbala usije ukakupofusha. Hivyo kwa uoni huu wenye mipaka utaona nini basi ndani ya Karbala? Utaionaje Karbala kupitia uoni huu? Utaelewa nini kupitia uoni huu? Kwa hiyo ni nani atakayeielewa Karbala? Ni



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 69 4/25/2018 11:01:28 AM

watu wangapi waliokuwepo pale kuiona Karbala kwa wakati ule?

Watu wa al-Kufa walimwandikia barua za kumwalika Imam Husein (a.s.), lakini je, waliielewa Karbala? Wakati ule kulikuwa na idadi ya watu ya mamia ya maelfu waliokuwa wameizunguka Karbala, katika msafara wa askari wa Umar bin Saad walikuwepo maelfu ya wapiganaji. Wale ambao hawakuja Karbala, watazamaji wa Kufa na Shaam (Syria) walikuwa pia ni maelfu lakini kwa ukweli ni watu 72 tu waliofika Karbala pamoja na Imam Husein (a.s.), hivyo ukweli ni kwamba walikuwa ndio wao tu waliokuwa muono wenye uwezo wa kuielewa Karbala. Waliweza kuona kila kitu na walikuwa na uelewa sahihi. Katika mawanda hayo hayo walikuwepo wale ambao uoni wao ulitiwa ukungu, macho ya watazamaji pia yalikuwa na ukungu. Hebu jaribu kukisia hesabu ya watu wa wakati ule, kutoka kwenye idadi yote ya watu hao, ni watu 72 tu walioweza kuitafsiri Karbala kwa usahihi kwa sababu mara watu wanapokuwa wameielewa Karbala, basi hawawezi kusimama pembeni au hawawezi kuwa watazamaji.

Kadhalika hivi ndivyo hali ilivyo leo, idadi ile ile ya watu ndio ambao kwa kweli wanaoielewa Karbala leo hii. Ushahidi ni kwamba, kama watu wengi wangeweza



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 70 4/25/2018 11:01:28 AM

kuielewa Karbala basi kusingekuwa na uchelewaji huu wa Kutokeza kwa Imam al-Hujjat (a.t.f.s.). Kipindi hiki kisingekuwa kirefu namna hii kama ukweli ungelikuwa umeeleweka. Inashangaza kwamba tunasema Karbala, Karbala kwa wingi sana lakini bado inahitaji kutafsiriwa. Hili ni tatizo moja; jingine ni kwamba hakuna uwiano kati ya mfasiri na tafsiri ya somo lenyewe. Yeye ni mtu mwenye uoni wenye ukomo na Karbala ni bahari pana mno. Isipokuwa atakapo endeleza utambuzi wake, sio rahisi kwamba ataweza kuitafsiri Karbala. Hili pia linahusika kwa Ghadiir na matukio yote kama hayo. Ni muhimu juu yetu sisi kuomba kwamba tupate uoni wa namna ambayo kwamba tunaweza kufanya uadilifu kwenye uchambuzi huo.

## MATOKEO YA UCHAMBUZI WA AKILI FINYU

Kama inavyosemekana, mada ya Ashura na Karbala na mwenendo (*siirah*) ya Imam Husein (a.s.) inategemea juu ya ufafanuzi kama ilivyo kwa mada zinginezo. Hakuna mtu anayeweza kutoa changamoto juu ya hilo bila ya fasili kuwa ameielewa mada hiyo. Katika zama zile, na katika zama za sasa pia na katika zama zijazo vilevile, inahitaji ufafanuzi. Nimezungumza juu ya maoni kadhaa na kuorodhesha ishirini kati yao ambayo



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 71 4/25/2018 11:01:28 AM

yanafahamika mno na fasili au maelezo juu ya mada hii, ambayo ilikuja katika akili za baadhi ya watu wazima na wanachuoni. Halafu vilevile nimesema kwamba ufafanuzi wa Karbala au tukio kama Ashuura, mageuzi haya matukufu na matukio kama haya ni magumu sana kuyafanyia ufafanuzi, sio lazima kwa watu wote kutoa ufafanuzi. Hii ni kwa sababu uwepo wa ushirikiano wa karibu sana kati ya somo lenyewe na yule anayelitolea ufafanuzi ni kigezo muhimu sana katika kutoa ufafanuzi. Yule mtu anayechambua tukio na lile tukio lenyewe lazima kufanana katika upana wao. Uono mfinyu hauwezi kufanya ufafanuzi wa tukio zito kama hilo, na tumeona matokeo ya mtazamo kama huo.

Maulana Ruumi ametoa mfano mzuri kabisa wa mtazamo kama huo, wakati tukio linapokuwa kubwa sana na muono ni mfinyu, matokeo ya uchambuzi yanayopatikana yanageuka kuwa ni mzaha wa kimawazo, maoni na mawazo. Hii ni kwa sababu mawazo yanaundika pale tu muono unapolitazama tukio. Wakati muono unapoangukia kwenye tukio hapo maoni yanajitokeza kuwepo. Hivyo mipaka ya maoni haiishii kwenye tukio, inaishia kwenye muono na utambuzi wa tukio. Jinsi muono unavyokuwa mkubwa ndivyo mawazo yatakavyokuwa makubwa. Matukio wakati mwingine yanakuwa makubwa zaidi kuliko muono wenyewe,



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 72 4/25/2018 11:01:28 AM

hivyo mawazo yanayoundwa kutokana na matukio kama hayo yanaweza kuwa mengi mbalimbali, kama yale juu ya ulimwengu. Kwa vile ulimwengu ni mkubwa sana, kuna maoni mapana sana kuhusu ulimwengu vile vile. Maoni yako chini ya udhibiti wa muono na sio chini ya udhibiti wa tukio.

Mfano ambao Maulana Ruumi aliuwasilisha ulikuwa kwamba, ndani ya chumba kilichofungwa chenye giza aliwekwa tembo, halafu wachambuzi wengi na waona mbali wengi katika utaratibu ulioandaliwa waliingizwa ndani ya chumba hicho kwenda kuona kilichokuwa humo ndani ya chumba hicho. Ni jambo la kawaida kwamba kwa vile kile chumba kilikuwa na giza hawawezi kuona chochote; hivyo walipapasa tu kwa mikono yao ndani ya chumba hicho ili kutengeneza maoni. Hapa ni muhimu kutaja kwamba kuna baadhi ya watu ambao wakati wote husema kwamba hatuna wakati, tunashughulika na taratibu za kazi zetu za kila siku, na wanataka matokeo katika sentensi chache tu. Lakini hili halifanyi kazi katika hali nyingi, katika sehemu fulani fulani unahitaji kusimama, kuwa na subira na kuchukua muda katika kuelewa mambo. Katika hadithi hii ya mfano pia, wengi waliingia ndani ya chumba hicho kwa haraka na ndani ya muda mfupi tu wakajaribu kukusanya elimu kuhusu kilichokuwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 73 4/25/2018 11:01:28 AM

ndani ya chumba hicho. Mmoja aligusisha mkono wake na akatoka nje, mwingine akafanya hivyo hivyo, wa tatu vilevile akafuata njia ile ile ya wenzie. Chochote walichoweza kugusa kwa haraka waligusa, kama vile tu tunavyosema kwamba tuna muda wenye ukomo wa mwaka mmoja au miaka miwili tu ya kusoma kwenye shule za kidini (Hawza), ndivyo katika muda huu mfupi yule tembo aliweza kueleweka kwa namna yenye ukomo mfinyu tu.

Upatikanaji wa elimu unategemea juu ya kiasi gani cha muda na fursa tunayotumia katika kuipata. Pale mtu atakapoingia kwa haraka na kuigusa tu, mikono yake inagonga kwenye mkia, na anapotoka nje kila mtu anamuuliza kuhusu alichokiona ndani humo, yeye anajibu kwamba kuna fagio linaloning'inia humo chumbani, ni kwa vile aligusa mkia tu. Kwa sababu ya haraka zake na kwa sababu ya uoni wake finyu yule tembo na ukubwa wake amegeuka kuwa fagio. Hii ndio sababu yeyote anayeuangalia ulimwengu huu kwa haraka haraka, kwake yeye ulimwengu utaonekana kama mpini wa fagio tu. Lakini yeyote yule anayeuangalia kwa welekevu na subira atapata maoni tofauti kabisa kuhusu ulimwengu huu. Hivyo wengine walisema hii ni nguzo, kiti cha kifalme, na kwa mujibu wa mwingine ilikuwa ni pangaboi ndani humo. Kila mmoja aliwasilisha maoni yake, lakini yey-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 74 4/25/2018 11:01:28 AM

ote aliyetazama na kugusa sehemu zote za mwili mzima wa tembo huyo aligundua kwamba huyo alikuwa ni tembo hasa.Hivyo uono wa kawaida ni ule ambao ni mpana na sio ulioundwa kwa haraka, ule ambao unafanywa kwa kuchambua kila kipengele cha suala zima kwa utulivu na subira. Kwa hiyo lazima tuweke muda kwa ajili ya kutafuta elimu. Lazima tuokoe muda kutoka kwenye sehemu nyingine na kuutumia kwa mambo kama hayo. Isije kuwa kwamba tulazimike kuokoa muda kutoka kwenye mikusanyiko ya kidini, misikitini, Madrassa na kisha tuupoteze kwenye maeneo ya madukani, masokoni, sherehe na kwenye safari zisizo na manufaa kwenye mabarabara. Hii ni shughuli ya hasara ambapo tunaokoa muda kutoka kwenye maisha yetu na kuutumia kwenye mabarabara. Ni muhimu kuokoa muda, lakini vilevile ni muhimu juu ya ni wapi na vipi tunautumia ule muda wetu tuliookoa. Tunapaswa kuokoa muda unaotumika barabarani na kuutumia kwa mambo kama hayo yenye manufaa na sio kinyume chake, vinginevyo ni kitendo cha kibadhilifu katika maisha yetu.

## HUSEIN (A.S.) – MFASIRI BORA WA KARBALA

Maelezo na ufafanuzi wa tukio la Karbala ni mgumu sana na unaofika mbali sana. Ni bahari ya kina kirefu

na yenye tufani ambamo mawimbi makubwa huibuka humo na kuzamisha ndani yake wale watu wanaoangalia humo. Wengi wamezama kwenye bahari hiyo na kujifisha maji wao wenyewe, na hawakupata manufaa yoyote; wengine wanachukulia kwamba wamepata manufaa kutoka kwenye bahari ya Karbala kwa kujimwagia matone yake juu ya vichwa vyao kwa kukaa ufukweni mwake. Hii ni namna ya hisia nzuri tu na si kingine chochote. Kuufikia uso wa bahari hiyo, maandalizi na ridhaa vinahitajika. Vyovyote iwavyo, hii ilikuwa ni namna ya kisingizio tu iliyowasilishwa. Swali sasa ni kwamba ni ipi kati ya tafsiri au ufafanuzi tutakayoichukulia kwamba ndio halisi na ambayo tuipendelee, ni tafsiri ipi ambayo ni yenye kufaa kiasi hicho, ni maelezo yapi yanayoweza kutuchukua na kutupeleka kwenye kiini hasa cha tukio hili.

Kama tukiangalia ndani ya kauli za Imam Husein (a.s.), yeye mwenyewe ndiye mwelezaji mzuri na bora wa tukio hili. Ingawa wafuasi wa Imam Husein (a.s.) nao pia wamefanya hivyo, na wale ambao waliokoka kutoka Karbala vile vile walitoa maelezo juu ya lile tukio la kutisha. Lakini mtu bora zaidi, katika hili, ni Imam Husein (a.s.). Hii ni kwa sababu kwamba vilevile yeye anatimiza yale masharti muhimu kwa ajili ya kutoa ufafanuzi, na njia ya kuyapangua matatizo yale. Moja ya matatizo, kama ilivyo-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 76 4/25/2018 11:01:29 AM

tajwa hapo kabla, lilikuwa ni zile silika za kishetani zilizoingia ndani ya wanadamu wakati wanapokaa ili kuchambua matukio ya ki-Mungu. Tatizo hili linakuwa halipo endapo kama tutamrejelea Imam Husein (a.s.) mtangazaji wa tukio hili kwa sababu yeye ni Ma'sum. Maasum ni mtu asiyewaza kukosea kamwe katika kulielewa jambo na pia kulipitisha mbele zaidi. Tatizo jingine na hali juu ya uchambuzi lilikuwa ni kuwa na maoni mapana kama lile tukio lenyewe lilivyo pana.. Kwa hiyo hapa, kiasi lile tukio la Karbala lilivyopana na kubwa, kadhalika na muono wa Imam Husein (a.s.) ni mpana na mkubwa kiasi hicho hicho. Kwa hakika Imam Husein (a.s.) ndiye mwasisi wa Karbala, mvumbuzi wa Karbala. Kwani Karbala ilikuja kuwepo kupitia mikono ya Imam Husein (a.s.), na wale waliojaribu kuibadili kuwa ni Karbala ya Yazid wameshindwa. Na angalau dunia yote iliona kwamba lile lilikuwa ni kitendo cha Imam Husein (a.s.). Na inatajwa katika kurasa za historia kwamba hii ni Karbala na Ashuura ya Husein (a.s.). Hivyo tunapaswa kuiadhimisha hii kama Karbala ya Husein kwa kumbukumbu ya Bwana Mkubwa huyu. Tunapaswa kuliangalia tukio hili kupitia macho ya Imam Husein (a.s.) kama nilivyoelezea tayari hapo nyuma kwamba maelezo yote na tafsiri ya tukio hili sio halisi na sahihi, na kwamba baadhi yake hayana hata kiungo chochote cha uhusiano na shaksia hii tukufu ya

Imam Husein (a.s.), na ni matokeo ya wazi ya purukushani na utumbukiaji ndani ya giza nene.

Lakini baadhi ya yale yaliyotajwa mapema ni halisia. Ingawa hatuwezi kusema kwamba ni maelezo yaliyoshikamana sawasawa kwa uthabiti, kwa sababu kila mtu amechungulia katika tukio hili kwa uoni wenye mipaka na ameasisi mawazo yake na akayaelezea kwa kiasi fulani. Mambo yote haya yanayorejelewa katika maelezo haya halisia yalikuwepo Karbala, lakini endapo bado mtu ataangalia kwa uoni mpana zaidi anaweza kuona kitu kingine zaidi.

## FALSAFA YA MAGEUZI YA IMAM HUSEIN (A.S.)

Kwa nini Imam Husein (a.s.) alisimama? Kwa nini wito wa Karbala ulikuja kutokea? Kwa nini vuguvugu la Karbala lilianza? Ni lazima ijulikane na kuelezewa. Husein (a.s.) hakuacha hata kazi yake ya kuelezea na kuzungumzia juu ya lengo la wito huu kwa wengine. Aliuawa kishahidi mara tu baada ya kufanya kazi hii. Wengi wetu tuna tabia ya kazi zetu kwa ajili ya wengine kuja kuzifanya kwa kutoa visingizio. Yeye (a.s.) hakutegemea watu wengine kuifanya kazi hii, bali aliifanya yeye mwenyewe. Hakuiacha kwa ajili ya wengine kuja baadae na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 78 4/25/2018 11:01:29 AM

kufanya maelezo yasiyo sahihi juu ya tukio hili. Haikuwa kwamba pale muda wa kufa kwake kishahidi ulipokaribia aliomba muda zaidi na akafanya ufafanuzi wa tukio hili. Haikuwa hivyo, yeye kutokea mwanzoni mwa wito wenyewe alianza kufanya maelezo na ufafanuzi wa tukio hili. Mfafanuzi na mwelezaji bora ni yule anayeelezea lengo lake kabla ya kuanza kazi yenyewe, hangojei hadi kuelekea mwishoni ndipo abainishe lengo la kazi yake. Imam Husein (a.s.) katika hatua na nyakati tofauti za wito wake alieleza wazi, alibainisha na kuzungumzia juu ya lengo la wito wote kwa jumla.

Lafudhi tofauti ambazo Imam Husein (a.s.) alizitumia kwa kweli zilikuwa ni uthibitisho wa ile sababu ambayo aliitangaza katika siku ile ya kwanza hasa ya harakati hizi na akashikamana nayo hadi mchana ule wa siku ya Ashuura. Ni jambo gani hili ambalo lilimfanya Imam Husein (a.s.) kuanzisha mageuzi haya?

Imam Husein (a.s.) kwa kweli ni shaksia adhimu na tukufu, na amewasilisha mbele ya ulimwengu mandhari pana na ameelezea kwa ulingano sawa ule upana wake pia. Kuna tatizo moja ambalo linawafika Ma'asum wote, liliwakabili Mitume na baada yao, Maimam maasum, watu watakatifu na hata wawakilishi wa Maimam wanakabiliana na tatizo hilo hilo. Hata



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 79 4/25/2018 11:01:29 AM

wakati yule Imam) a.t.f.s.) wa mwisho anayengojewa atakapotokeza, yeye pia atakabiliana na tatizo hilo hilo la msingi, kila mtu ambaye Mwenyezi Mungu alimchagua/alimuweka au alimsimamisha kwa ajili ya ujumbe maalum kama vile Mitume, wote walikabiliana nalo.

Na kila mmoja miongoni mwao alijaribu kulitatua tatizo hilo. Imam Husein pia alifanya vivyo hivyo na kwa utatuzi wa tatizo hili ndipo tukio hili likaja kuwepo. Hii ndio sababu tunasoma *Ziarat-e-Waritha* kwa ajili ya Imam Husein (a.s.). Yeye ndiye mrithi wa Mitume. Katika hali halisi lile tukio la Karbala lilikuwa ndio wosia, urithi wa Mitume, kwa hiyo yeye anajulikana kama mrithi wa Mitume (*warithatul-Anbiyaa*). Hivyo imedhihirishwa kwamba liliunganishwa tangu mapema na lilikuwa ni uandamizi wa mitume. Kwa upande mwingine Husein (a.s.) vile vile ni Kigezo cha Mfano (*Us-wah*); ni maneno yake.

فلكم فيّ (بيّ) اسوة

**"Mimi ni kiigizo cha mfano kwenu." – *Mausuwat Kalimati Imam Husein (*a.s.) uk. 377.**

Kama tukiangalia maneno ya Maasumin kadhaa wengine (a.s.) hususan haya hapa:



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 80 4/25/2018 11:01:29 AM

إِنَّ الْحُسَيْنَ مِصْبَاحُ الْهُدَى وَ سَفِينَةُ النَّجَاةِ

**"Husein (a.s.) ni taa ya uongofu; ni safina ya wokovu." –** ***Uyunul-Akbar e Ridha (a.s.)*** **Jz. 1, uk. 59.**

Kama tukizifikiria kauli hizi tatu, za kuwa muandamizi wa Mitume (a.s.), kuwa kigezo cha mfano (us-wah) na kisha kiongozi na safina ya wokovu, tunaweza kufikia mawazo ya kupendeza na yenye kusababisha hitimisho.

Hivyo hebu tuiangalie ile kauli ya kwanza ambamo inasemekana kwamba Husein (a.s.) ni mwandamizi (mrithi) wa mitume, hii inamuunganisha Husein (a.s.) moja kwa moja na zama za nyuma. Ambapo ile riwaya kwamba Husein (a.s.) ni safina ya wokovu inamuunganisha Husein na zama zijazo baadae. Sasa tunaweza tukaona mielekeo miwili ya shaksia ya Imam Husein (a.s.), mwelekeo mmoja ambao unamuunganisha na wahenga wake na mwingine unamhusisha yeye na Ummah baada ya Karbala. Mrithi (*Warith*) na kigezo cha mfano (*Us-wah*) ni mada mbili. Hawezi kuwa Kigezo cha mfano kwa wale waliotangulia, yeye ni *Us-wah* kwa kizazi kijacho na ni mrithi wa wale waliotangulia; wahenga wake. Husein (a.a.) ni mrithi – mwandamizi wa mtu na ni kigezo kwa mtu mwingine. Siri zote na ukweli vinaweza kupatikana kutokana na vipengele



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 81 4/25/2018 11:01:29 AM

hivi viwili kwamba kwa nini Husein (a.s.) alifanya mageuzi (*Qayyam*) haya. Kama endapo, na Mungu aepushilie mbali hilo, hatukuwa na maelezo yoyote ya Karbala kutoka kwa Imam Husein (a.s.) mwenyewe hata hivyo hivi vipengele au mielekeo miwili ingekuwa inatosheleza kwetu sisi kuelezea tukio la Karbala. Kwamba Husein (a.s.) ni mrithi na Kigezo (*Us-wah*).

## HUSEIN (A.S.) – KIGEZO CHA MFANO

Us-wah maana yake ni mfano. Kigezo cha Mfano. Kama inavyoelezwa kwenye Qur'ani:

لَّقَدۡ كَانَ لَكُمۡ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٌ

**"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ….. (Qur'ani Tukufu Sura al-Ahzab; 33:21).**

Ingawa aya hii fupi inahitaji maelezo ya kutosha na uchambuzi, haikudhihirishwa kwa urahisi na wazi kabisa. Maana ya *Us-wah* bado haijaeleweka kwetu sisi na ushahidi wa hili ni kwamba hadi leo hii hatujawakubali wale watu maasum kama vigezo (*Us-wah*) vyetu vya mfano. Kusikiliza maamrisho na makatazo (*amr* na *nahyi*) ya mtu haimaanishi kwamba ni Kigezo cha Mfano kwetu. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akituzuia



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 82 4/25/2018 11:01:29 AM

kufanya jambo nasi tukaliepuka, haina maana kwamba Mtukufu Mtume aligeuka kuwa Kigezo cha Mfano kwa ajili yetu. Bali ina maana kwamba tulimfuata na kumtii na tumetiishwa kwake (*ita'at*). Lakini hatukumkubali yeye kama Kigezo cha Mfano juu yetu. Kigezo cha Mfano kiko hatua chache nyuma ya utii huu (*ita'at*); kwa hiyo inawezekana kwamba sisi ni wafuasi (Muti'i) wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lakini bado anaweza asiwe Kigezo cha Mfano kwa ajili yetu. Kama vile kwenye Qur'ani imezungumzwa kwa tofauti kuhusu:

أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ

**"….. Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume." (Qur'ani Tukufu Sura an-Nisaa'; 4:59).**

na

**"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ….. (Qur'ani Tukufu Sura al-Ahzab; 33:21).**

Imeelezea kwa mbalimbali, maneno yote yako tofauti, sio kitu kimoja kinachojadiliwa katika aya zote mbili. Lakini kwa kweli Qur'ani inashauri kwamba tunalazimika kumfuata na vilevile kumkubali Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama Kigezo cha Mfano kwa maisha yetu vilevile. Tunawatii watu wengi lakini sio Vigezo



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 83 4/25/2018 11:01:29 AM

vya Mfano juu yetu. Kwa mfano, je sisi hatuwatii wazazi wetu? Lakini sio wajibu kwamba watoto ambao wanawatii wazazi wao, basi wazazi hao pia ni Vigezo vya Mfano kwa ajili yao. Kigezo cha Mfano anaweza akawa yeyote yule, inaweza ikawa ni jirani, mwalimu, mtu mwanahistoria, lakini wao pia bado wanawatii wazazi wao. Hivyo inadhihirisha ile tofauti kati ya kumkubali mtu kama Kigezo cha Mfano na kule kumtii mtu. Athari ya Kigezo cha Mfano katika maisha yetu inakosekana na huu ni ushahidi tosha kwamba sisi hatujatambua maana yake. Hatuna nafasi kubwa ya kutosha ya kujadili kwa undani zaidi kuhusu Kigezo cha Mfano (Ushwa) hapa, hili linahitaji mhadhara wa kipekee ili kuelewa nini kinachomaanishwa na kigezo cha mfano, nani anapaswa kuwa kigezo cha mfano na kwa nini kigezo cha mfano ni muhimu katika maisha yetu.

## KUFUNUA PAZIA LA KARBALA

Hivyo hivi vipengele viwili vya shaksia ya Imam Husein (a.s.) ambamo yeye mwenyewe anasema kwamba: "Mimi ni Kigezo cha Mfano kwenu" na kwa upande mwingine wale maasumin wengine wanasema kwamba Husein (a.s.) ni mrithi wa mitume tofauti, na kwa kuainisha jina la kila mtume wao wamerejelea kwenye urithi wake. Hii inatosha kwa kuelewa ukweli na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 84 4/25/2018 11:01:29 AM

falsafa ya mageuzi matakatifu ya Imam Husein (a.s.). Sasa tunahitaji kulianika wazi lengo hili. Tafsiri kama neno ina maana ya kufunua jambo fulani (*Kashfi Qina*) ambalo limefunikwa na kufichika. Kwa sababu pazia la maneno limefunika ile maana ya Qur'ani na mfasiri anatokeza kuja kulifunua na kisha ni hapo tu ambapo tunaweza kuona basi ile maana yake halisi na ya kweli.

Sasa kwa kutumia mielekeo hii miwili ya shaksia hebu tujaribu kulifunua pazia, na tujaribu kuelewa ule uunganishaji wa uandamizi (urithi) na kigezo cha mfano pamoja na Imam Husein (a.s.). Yale matatizo yaliyowakabili mitume, Husein (a.s.) alipata mambo yote kutoka kwa mitume katika wasia, yeye alipokea mirathi kutoka kwa mitume pamoja na matatizo na misiba mikubwa ya Manabii. Namna ambavyo Husein (a.s.) ni Kigezo cha Mfano katika vitendo vyote, amali na maadili kwa ajili ya wengine pia yeye ni Kigezo cha Mfano katika nyanja hii vile vile. Matatizo yale yaliyowakuta Mitume, Qur'ani imeyataja matatizo haya.

## KUKOSA MANTIKI/UPUMBAVU WA MATAIFA (UMMAH) –TATIZO LA URITHI

Wa kwanza wao wa mitume wote ambaye kuhusu yeye Qur'ani imemtaja kwa usanifu sana na kuzungumzia juu



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 85 4/25/2018 11:01:29 AM

ya matatizo haya ni Hadhrat Adam (a.s.), lakini baada yake yeye, Mtume aliyekabiliana na matatizo kuhusiana na ummah wake kama ilivyotajwa kwenye Qur'ani ni Nabii Nuh (a.s.). Qur'ani imeelezea kwa kina sana kuhusu vitendo, harakati, malengo, ujumbe na matatizo yake yeye. Nabii Ibrahim, Nabii Isa, Nabii Musa na kisha kwa uainishaji hasa Mtume Muhammad (s.a.w.w.), matatizo yao yote yameelezewa na Qur'ani. Tatizo gumu kabisa ambalo liliwakabili mitume na ambalo linakuja kama kikwazo kikubwa katika kazi ya uongozi kuelekea kwenye ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na kwa sababu ya tatizo hilo watu wengi walibakia wameachwa bila uongozi, walizaliwa wakiwa wamepotoshwa na wakafa wamepotoka. **Tatizo hilo la msingi lilikuwa ni upumbavu au kukosa mantiki (*bihisi*) kwa watu** ambako kuliwakuta Mitume wote. **Upumbavu huu ulikuwa ni kuelekea kwenye haki (*Haqq*).** Uwanja wa haki ni mpana sana. Imam Ali (a.s.) anasema kuhusu haki hivi: "Haki ni pana sana kuizungumzia, lakini ni ngumu na finyu sana kuifanyia utekelezaji."

Hii ina maana kwamba unaweza kuongea na kutoa hotuba ndefu nyingi juu ya mada ya haki kwa sababu yenyewe ni pana sana. Lakini wakati unapoanza kutwaa au kufanyia kazi haki unaweza kuona kwamba ni ngumu sana kuifanyia kazi na kuitekeleza, huwezi kuweka



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 86 4/25/2018 11:01:29 AM

hatua yako mahali pote, na sio kwamba kila hatua tunay-ochukua basi ni hatua ya haki. Hatua zinazochukuliwa kuelekea kwenye haki ni maalum na makhsusi kabisa. Hii ndio tafsiri ngumu na sanifu sana ya haki iliyofanywa na Imam Ali, na zaidi kabisa ni kwamba Imam Ali (a.s.) amelithibitisha hilo katika maisha yake mwenyewe binafsi.[2]

2. Ali (a.s.) anasema ndani ya Nahjul-Balaghah, sio katika zile siku za kunyimwa bali ni katika siku za mamlaka yake makubwa, pale ambapo hazina ya Ummah ya dola kubwa kama hiyo ambamo jua kamwe halizami (hazina hiyo) ilikuwa mikononi mwa Ali (a.s.), ambaye hakunyimwa kitu chochote, yeye alikuwa ndiye mamlaka kuu, alikuwa na jeshi na upanga, na katika zama zile yeye anasema:

"Kama ningekuwa nimepewa matamanio ya hazina isiyo na mipaka na dunia yote hii ikageuka kuwa dhahabu, au kama ninatishiwa kuburuzwa nikiwa bila nguo katika miiba za jangwa (Khari-Mughaiila), na nikatakiwa tu kunyakua ganda la shayiri kutoka kwenye mdomo wa mdudu chungu, mimi nitapendelea kuburuzwa juu ya miiba za jangwani, lakini sitakuwa tayari kunyakua lile ganda la shayiri kutoka kwa mdudu chungu."

Unaweza kufikiria sasa, je Ali (a.s.) ni Kigezo cha Mfano *(Us-wah)* kwa ajili yetu ama laa? Lakini kwa ukweli halisi tunatekeleza utii wake lakini sio Us-wah kwetu. Wadudu chungu ni wadogo sana, tunaziponda haki za ubinadamu, na za Allah. Lakini Imam Ali (a.s.) hayuko tayari kunyakua ganda la nafaka kutoka kwa mdudu, kwa nini? Mdudu chungu huyo anaweza kuokota ganda jingine pia, lakini kwa Ali (a.s.) uzembe huu mdogo kiasi hicho unaweza kugeuka kuwa upumbavu na ukosefu wa huruma. Kwa hiyo Ali (a.s.) hawezi kulala mjini Kufa kwa sababu huenda kuna mtu amebaki na njaa huko Yemen. Lakini walikuwepo wengine ambao walilala usiku na mchana, na hawakuwa na habari ya kujali kuhusu njaa ya mtu mwingine.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 87 4/25/2018 11:01:29 AM

Haki ni kamilifu katika asili ya maumbile iwe ni kuhusu Mwenyezi Mungu ama kuelekea kwa mtu wa kawaida. Hii ina maana kwamba haitoshi kwa sisi kutoa haki zetu kuelekea kwa Mwenyezi Mungu tu, haki za watu, haki za jamii zinahusika kikamilifu kwetu sisi vilevile. Kukosa mantiki kuhusu haki hii ni tatizo la kijamii.

## UPUMBAVU – SILAHA YA MADHALIMU

Upumbavu huu unakuja kupitia hatua tofauti, sio kwamba mwanadamu ni mpumbavu kuanzia ile siku ya mwanzo. Upumbavu una maana ya kuwa katika hali ya akili kukosa fahamu. Kwa mfano, kama mtu anakuwa mgonjwa na anataka kufanyiwa upasuaji haraka sana, ambayo kwamba sehemu moja ya mwili wake inapaswa ikatwe, hivyo ili kumuokoa na maumivu mwili wake lazima ufanywe ukose fahamu. Ukosa fahamu huu unahusiana tu na maumivu, na wakati tunapokuwa hatusikii maumivu basi hapo daktari anaweza kufanya chochote akitakacho kwenye mwili wako, kuupasua, kuuponda, kuula, kuutupilia mbali, mgonjwa huyo hatasikia lolote kwa sababu hana fahamu. Kwa hiyo kuelekea kwenye jambo lolote ambalo mtu anafanywa kuwa hana fahamu, basi uwepo na kutokuwepo kwa jambo hilo kote kunabakia ni sawa sawa kuhusiana na hisia



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 88 4/25/2018 11:01:29 AM

na akili. Hivyo hata kama anakuwa na maumivu makali yanayopita ndani ya mwili wake, lakini kwa vile mwili wake umekuwa hauna fahamu hakuna hisia za maumivu hayo. Ni kawaida pale mtu anapopoteza fahamu ya kuhisi hayo maumivu, basi kuangamia kwake kuko karibu sana, kwa sababu maumivu ni dalili ya matatizo na maradhi, na kama mtu hahisi maumivu, anakuwa hajui juu ya maradhi ambayo hatimae yatamuua.

Unaweza ukaona katika mazingira yaliyokuzunguka, ni kawaida kabisa kwamba jamii zetu zimekuwa zimezimia kwenye machungu ya kijamii. Unaweza ukachunguza mwenyewe kwa kubinya sindano katika mwili wako na uone iwapo unahisi maumivu ama hapana. Kama unayahisi maumivu basi wewe ni katika wale wanaohisi maumivu na unazo hisia za kuyahisia maumivu. Lakini wakati mtu huyu huyu, anayehisi maumivu ya mwili wake, anaondoka nyumbani kwake akiwa ameshiba, na kisha kila mahali anaposhuhudia matumbo matupu, watu wenye njaa, wagonjwa, waliokandamizwa na wenye kuteseka kwa maradhi, yeye anapita tu katikati yao kana kwamba hajaona jambo lolote. Unaweza kuhisi maumivu ya sindano iliyochomwa kwenye mwili wako, haya ni maumivu yako ya kimwili, lakini huwezi kuhisi maumivu ya watu hawa waliokuzunguka. Hii ni kwa sababu mwili wako



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 89 4/25/2018 11:01:29 AM

uko hai lakini moyo wako hauna fahamu na hauwezi kuhisi maumivu hayo.

Ni mara ngapi tunakutana na mandhari ya kimaangamizi kama haya, lakini hakuna hata mojawapo linalosababisha maumivu japo kidogo sana ndani ya nyoyo zetu. Ni taarifa za habari ngapi tunazosikiliza kila siku? Tunapata habari za kadhia na matukio kadhaa kama hayo, lakini ni maumivu kiasi gani tunayoyahisi. Hatuhitaji kwenda mbali kumuona mtu mpumbavu, tunaweza kuuona upumbavu ndani ya nafsi zetu wenyewe. Wakati mwanadamu anapokuwa hawezi kuhisi maumivu, basi ni dhahiri kwamba kile chanzo cha maumivu yeye ataendelea kuzembea kuhusu hicho pia. Hususan wakati uzembe unapofikia kiwango ambapo mtu anapoteza hisia zake kuelekea kwenye maumivu ya haki pia. Halafu anashuhudia hisia za dhulma na maonevu lakini hawezi kuyahisi maumivu. Namna hii ya uzembe sio wa kimaumbile, mwanadamu hakuzaliwa bila mpumbavu. Zaidi ya hapo Mwenyezi Mungu amemuumba mwenye fahamu. Kwa hiyo mtoto hulia mara tu baada ya kuzaliwa kwake, na kama hakulia tunajaribu kumfanya alie. Mwanadamu anachukia kila aina ya maumivu na kulia, wakati mtoto huyo huyo anapolia baadae, wazazi wake wanapatwa na wasiwasi sana na kuhuzunika na kuomba aweze kuacha kulia.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 90 4/25/2018 11:01:29 AM

Lakini mnamo ile siku ya kwanza ya kuzaliwa kwake, wazazi wenyewe wanajaribu kumfanya alie. Ina maana kwamba huu ni wito wa uhai. Katika kulia huku tunaweza kuona uwepo wa uhai. Na kama mtoto huyo hatalia basi inaonyesha kwamba hana hisia. Na mtu asiye na hisia hawezi kuishi muda mrefu. Hii ni kwa sababu kukosa hisia kunampeleka mwanadamu kuelekea kwenye kifo. Kwa hiyo tunamshitua mtoto na kibao kidogo, kumfinya na sindano ili aweze kwa namna fulani kulia na kutoa sauti, ili tuweze kujua kwamba mtoto huyo anazo hisia ndani yake. Hivyo kila aina ya kilio sio uzushi (*biddah*). Kuna aina fulani za maombolezo ambazo ni dalili ya uhai ndani ya mwanadamu, yanaeleza kwamba mtu huyu yuko hai na hisia na fahamu vimo ndani yake. Na kama hakulia, basi mfanye alie. Na kama hatalia bado, basi angalau ufanye uso wako kama unalia ili tujue kwamba bado ungali hai na kwamba hutakufa haraka.

Upumbavu unajitokezaje ndani ya mwanadamu? Upumbavu ni mada muhimu sana na kwa ukamilifu tunahitaji kiasi cha siku chache za majadiliano kiasi cha kuelewa tu jinsi upumbavu unavyotokea kuwepo ndani ya mtu na kisha kwenye jamii. Leo hii kuna teknolojia ya kiuganga ambayo kuna baadhi ya madaktari wanaojifunza kufanya upasuaji, na kuna mganga anayeeleza



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 91 4/25/2018 11:01:29 AM

njia ya namna ya kumfanya mgonjwa akose kujifahamu. Mganga huyu anajulikana kama "Mtuliza maumivu – *anesthetic.*" Wakati mwingine hata mtaalamu wa upasuaji – surgeon anakuwa hana ujuzi wa kumfanya mgonjwa akose fahamu, anamtegemea mtulizaji huyu. Mtaalamu huyu anafundishwa kwa kiasi tu kwamba anaweza kuwafanya watu wakose fahamu na kuwafanya wasihisi kitu ili baadae yule mpasuaji anaweza akafanya lolote na mgonjwa, hata kuchanachana mwili wake. Katika njia ya namna hiyo hiyo kuna watu ambao wamepewa kazi ya kuyafanya mataifa kuwa wapumbavu, wao ni wataalamu wa upumbazishaji. Wapasuaji makatili na waonevu ambao wanafanya upasuaji huo wa mataifa wanakata, kuchana chana na kuyatafuna kuyala, lakini kwenye upasuaji na uchanaji huu, ni lazima kuyafanya mataifa yawe hayana fahamu, yapumbae.

Kwa ajili ya upumbazaji huu wao wanatuma wataalamu hawa, aina hii maalum ya upumbavu inatengenezwa ndani ya mataifa kupitia ndimi zao, kalamu zao na majukwaa, vitabu na vyombo vya habari. Kwa hiyo wanatumia njia zote hizi na vyombo kuunda upumbaaji huu katika mataifa (ummah). Kwa nini? Kwa sababu watawala hawa katili wanapopasua matumbo na vifua, wakati wanapoharibu sura ya ummah, basi mataifa na

ummah wasiweze kuhisi operesheni hii. Wataalamu wao waliobobea, wa upumbazaji ni mastadi sana na walioelimika hasa. Na wanayafanya mataifa kuzembea kwa namna ambayo ummah hauwezi kuhisi kule kuchanwa vipande vipande kwa sababu wataalamu hao ni mahiri sana. Zaidi ya hayo, mataifa yanahisi kama yanapata maendeleo na kusonga mbele na kuingia kwenye ulimwengu mwingine tofauti.

Wakati mwingine watu wasio makini huzungumza upuuzi; kwa kweli katika hali hii watu huzungumza upumbavu zaidi. Kama mtu anaandika na huku anaongea katika hali ya kutomakinika isisemwe kwamba yeye anatoa hotuba, bali sema kwamba anapayuka. Lolote linalosemwa kwa wakati huo wa kutojitambua ni upuuzi mtupu na mazungumzo yasiyo na maana. Kwa hiyo mataifa mapumbavu huzungumza yasiyo na maana, ambapo mataifa yaliyoamka yanatenda zaidi. Hii ni aina mojawapo ya uzembe kwamba wanazungumza upuuzi. Sio kwamba kila asiye makini macho na ulimi wake vimefungwa, kwa kiasi upumbazaji huu ulivyo na kina zaidi, uzembe huu huongezeka zaidi. Kwa hiyo usiseme kwamba upumbazaji ndio ushahidi wa maisha. Mingi ya mijadala kutoka kwenye mimbari na misikitini ni mikusanyiko ya mazungumzo yasiyo na maana yanayozungumzwa na watu katika hali ya kutojitambua. Hivyo kuufanya ummah kukosa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 93 4/25/2018 11:01:29 AM

fahamu na kutojitambua ni ustadi ulioonyeshwa kutoka kwenye nyingi ya mimbari zetu.

Ni vipi mataifa yanavyozembea? Kama tunavyoona kwamba wanadamu wanakabiliana na matatizo mengi sana kuhusiana na maisha yake ya kila siku, kama vile matatizo ya kiuchumi, ya kijamii na ya kifamilia. Kuyaondoa na kuyakwepa matatizo haya wananunua na kutengeneza upumbavu ndani ya nafsi zao. Wanakimbilia kwenye msaada wa madawa ya kulevya na pombe. Kwa kutumia njia kama hizo za upumbazaji, kwa kiasi cha muda mfupi tu wanapata namna fulani ya starehe. Na unaweza kuwa umeona kwamba hisia ya uzito wa matatizo yao unaondoka kwa muda, na sio kwamba matatizo hayo yametatuliwa. Madeni yao hayawi yamelipwa kwa kutumia madawa na kuingia kwenye hali ya kutojitambua. Wanapokuja kupata fahamu, wanagundua kwamba yale madeni hayakulipwa, kwa kweli na riba imepanda zaidi sasa. Huu upumbavu wa kujitwalia hauwezi kutatua matatizo.

## MWANZO WA UPUMBAVU

Upumbavu unaanza kutokana na uzembe (beaytnai). Uzembe ni neno jepesi; lina maana ya kuonyesha ku-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 94 4/25/2018 11:01:29 AM

tojali na kutomakinika kwenye jambo. Hii kwa kweli ni hatua ya awali kabisa kuelekea kwenye upumbavu. Mwisho na hitimisho la mtu mzembe ni upumbavu, upumbavu wa moyo.

Kwa mfano unamuona muombaji siku moja, na unamuangalia bila kujali kabisa na unaondoka zako. Unamuona muombaji yule yule kesho yake lakini humjali tena, lakini yule mtu anaye waangalia wenye kuomba kwa uzembe wa kutojali kwa siku nyingi, siku moja atakuja kuwa mzembe kabisa na mpumbavu katika suala la waombaji. Hisia za kuhusika kwenye uombaji zimekufa ndani yake yeye. Simulia kuhusu huzuni na wasiwasi mwingi wa mwanadamu na umasikini mbele yake, yeye hatojali hata kidogo, haitamuathiri yeye. Amekuwa mzembe. Kwa nini amekuwa mzembe? Kwa sababu tu ya kukosa kujali na mazingatio. Mambo madogo na hafifu wakati mwingine hugeuka kuwa mambo makubwa. Tabia zinakuwa ni kama kuzaliwa kwa mwanadamu. Ni vipi mwanadamu anavyozaliwa? Ni kwa tone dogo tu la manii. Kama ukijaribu kuyapima manii hayo ambayo yanamfanya mwanadamu kupatikana basi pengine hutaweza hata kupata mashine inayofaa kwa kupimia. Hiki ni kitu kisichokuwa na uzito na kidogo sana, ambacho hakiwezi hata kuonekana kwa macho. Lakini tone hilihili dogo la manii linapoingia kwenye mazingira ya-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 95 4/25/2018 11:01:29 AM

nayostahili na yaliyo salama, linakua na kulelewa hapo na linageuka kuwa kama mwili mkubwa.

Na wakati linapojitokeza kama mwili, bado linakuwa endelevu katika kukua kwake, na linakuwa mwanadamu mwenye mwili wenye afya nzuri kabisa. Tabia zinazaliwa na kulelewa katika njia na namna hiyo hiyo. Mbegu ya tabia nayo pia kwa asili iko vivyo hivyo. Mahali ambapo uhai wa mwanadamu umelelewa ni katika tumbo la uzazi la mama na kiuno cha mwanaume, lakini tumbo la tabia liko ndani ya wanawake na vilevile ndani ya wanaume. Kitendo kidogo kimoja kinaingia kwenye matumbo haya kama mbegu ya uzazi, halafu matumbo haya yanailea na kuidhihirisha siku moja kama tabia imara na madhubuti, inazalisha tabia. Na wakati maisha ya mwanadamu yanapozalisha tabia, basi tabia hii haikomi, bali inaendelea kukua. Hawa walevi wa madawa wakubwa ambao unawaona wakitumia madawa ya kulevya wakati wote huu, wao pia walianza siku moja kwa kipimo (dozi) kimoja kidogo.

Kama tunavyosema kila mara wakati tunapokwenda kwenye sehemu isiyopendeza au iliyoharamishwa kwamba tunakwenda mara moja tu, lakini hatutambui kwamba hii mara moja tu inaweza kugeuka kuwa tabia madhubuti. Hivyo dini inatuzuia tusifanye dhambi,



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 96 4/25/2018 11:01:29 AM

haina maana kwamba wakati tunapotenda au kuhusika katika dhambi basi wakati huo tunapaswa kuacha na kutoka kwenye dhambi hiyo, bali tunapaswa kukiua chanzo ufanya dhambi kabla kuzaliwa kwake. Wala tusiangalie na kuelekea kwenye dhambi; huu ni mshale wa shetani. Kama ile mbegu ya tabia ilikwenda kwenye tumbo lile na ikazaliwa kama tabia madhubuti basi huwezi ukaidhibiti. Kwa hiyo lazima ufanye uharibifu wa dhambi kabla haijazaliwa; ni lazima tufanye upangaji mikakati kama vile tunavyofanya mpango wa uzazi na familia siku hizi.

Sio kwamba uidhibiti baada ya kuzaliwa kwake kwa sababu huyu ni mtoto wa haramu, ambaye pale anapoingia kwenye maisha mara moja, hawezi kufundishika kwenye njia sahihi. Tumeliacha lile tumbo la tabia kuwa huru bila kuchukua hatua za udhibiti wa uzazi, lakini tunafanya uzazi wa mpango wa familia kwa ajili ya kuzaliwa kwa wanadamu.

Tabia mbaya ambayo inamuathiri mtu inaitwa kama ni ugonjwa, lakini ile ambayo inaikumba jamii inaitwa mlipuko na tauni. Kama mtu mmoja au wawili wanapata homa, tunasema kwamba ni homa, lakini endapo eneo zima la makazi likipata mahoma, hapo tunasema kwamba hiyo ni tauni. Up-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 97 4/25/2018 11:01:29 AM

umbavu wakati mwingine unakuwa kwa mtu mmoja au wawili, huo bado ni hatari lakini sio sana, bali pale upumbavu huu unapokuwa ni kawaida ya jamii nzima basi hapo inakuwa ni gonjwa la mlipuko. Na milipuko kama unavyojua, inaweza ikaangamiza na kuitokomeza jamii nzima. Kuna mambo ya kuogopesha kama hayo katika historia ambamo milipuko ya kipindupindu na malaria imesafisha kabisa miji mizima na jamii kubwa.

## UPUMBAVU – GONJWA LA MLIPUKO LA JAMII

Ugonjwa wa mlipuko mkali na hatari sana ni upumbavu, lakini vile vile na wakati mtu anapokosa fahamu kwenye masuala ya haki. Haki inakanyagwa mbele ya mtu huyo naye wala haonyeshi huzuni juu ya hilo. Sio kwamba yeye haingilii au kulinda haki, anakuwa hana fahamu kiasi kwamba haonyeshi uchungu, huzuni au kushusha pumzi japo mara moja kwa vitendo hivi vya kidhalimu. Upumbavu huu unazalisha mambo makubwa na unakuwa sababu ya matukio ya misiba mikubwa. Na tukio la balaa kabisa katika historia ya mwanadamu ni pale mlinganiaji wa haki na mwenye kuchochea haki na ukweli, aliyesimamishwa na Mwenyezi Mungu anapotengwa. Wakati jamii inapokuwa imezembea, Mtume



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 98 4/25/2018 11:01:29 AM

kama Nabii Nuhu (a.s.) anakuwa ametengwa na kuwa mpweke. Na kisha anasema:

رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا

**"….. Ewe Mola Wangu! kwa hakika nimewaita watu wangu usiku na mchana."**
**(Qur'ani Tukufu Sura Nuh; 71:5).**

Nimewalingania asubuhi na jioni, lakini ulinganiaji wangu haukuwaathiri hata kidogo, kwa kweli kuliwaweka mbali kabisa. Hii ni kwa sababu wakati daktari anapowaita wale walioathiriwa na ugonjwa wa mlipuko, huo mlipuko wenyewe hauwaruhusu wao kumsogelea daktari huyo, bali inawafukuzilia mbali. Mlipuko unaowadhuru wanajamii unawaweka mbali na madaktari siku hadi siku. Haya ndio yalikuwa machungu ya Manabii wote kwamba walishirikiana na jamii zisizojitambua. Sababu iliyowafanya wawe wapumbavu ilikuwa kwamba walikuwa wazembe kuhusu haki ndogo na hafifu na kwa hiyo wakawa wapumbavu kuelekea kwenye mambo makubwa yanayowahusu. Mfululizo huu wa Mitume uliendelea mpaka ukamfikia Mtume wa Mwisho (s.a.w.w.). Na umeona kwamba hata Mtume wetu wa Mwisho (s.a.w.w.) aliinuliwa pia na akatumwa katika ummah



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 99 4/25/2018 11:01:30 AM

mjinga wa Makka. Ni nini kilichosababisha kule kuhama kwa Mtume (s.a.w.w.) kutoka Makka kwenda Madina? Ingawa kituo kilikuwa Makka, Masjidul-Haraam ilikuwa Makka, Ka'ba ipo Makka, ndio mahali pa wahyi. Ikiwa Madina ilikuwa iwe ndio kituo baadae, basi yeye (s.a.w.w.) angepelekwa Madina tangu mwanzo wenyewe au angalau angeweza kuelezwa mapema kabla ya siku ya Bithat – siku ya kutangazwa – kwamba yeye (s.a.w.w.) angehamia Madina na kule kushuka kwa zile aya za kwanza kutaanzia pale. Ufunuo wa kwanza unakuja Makka na kisha baada ya muda fulani, Yeye (s.a.w.w.) anaambiwa aondoke Makka. Kwa nini? Kwa sababu Makka imekuwa pumbavu na hakuna wahyi utakaoshuka Makka sasa. Yeye (s.a.w.w.) alitakiwa kuondoka kwenda kwenye sehemu ya maana yenye ufahamu na nchi ya haki ya Madina.

Madina ilikuwa ni jamii inayojali na yenye kujishughulisha. Ingawa kulikuwa hakuna Waislamu, lakini wayahudi na makabila ya Aus na Khazraj hawakuwa wapumbavu. Na ingawa wakazi wa Makka walikuwa ni ndugu lakini walikuwa ni wapumbavu na walikuwa hawajihusisishi kuhusu hali ya uadilifu. Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuondoa Mtume Wake (s.a.w.w.) kutoka kwenye jamii ya kipumbavu. Uhamaji huu uli-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 100 4/25/2018 11:01:30 AM

kuwa ni uhamaji kutoka kwenye upumbavu kuelekea kwa watu wenye akili na ushughulikaji.

Huu ulikuwa ndio wasia ambao Imam Husein (a.s.) pia aliupata kama urithi. Unaweza kuona kwamba katika tukio la Ghadir, baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), katika tukio hili kubwa kilichotokea ni kile kile. Leo wote wanashangazwa na kutengwa kwa Imam Ali (a.s.) licha ya tangazo kubwa kama lile la tukio la Ghadir, kama ukiwauliza Ahlus-Sunna (madhehebu ya Sunni), hawako tayari kulikubali hili, kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alichagua mrithi wake mwenyewe, basi ni vipi, imekuwaje wale masahaba dhahiri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wachamungu, wana jihadi wanaotukuzwa sana waliweza kuyakataa maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Na wakati mwingine maswali kama hayo huibuka katika akili za Mashi'ah vile vile, hili linawezekanaje? Ndio, hili linawezekana, hili linatokea wakati mtu anapoonyesha kuzembea kuelekea kwenye uadilifu na haki, halafu uzembe huu siku moja unakuja kugeuka kuwa upumbavu. Na huu ulipogeuka kuwa upumbavu basi hata kama Mtume (s.a.w.w.) alitangaza uongozi wa Ali (a.s.) mnamo mwezi 18 Dhil-Hajj na akafariki mnamo mwezi 28 Safar, ndani ya miezi miwili na siku kumi uzembe huu uliishia kwenye upumbavu. Kwa hiyo katika ile siku



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 101 4/25/2018 11:01:30 AM

ambayo yeye (s.a.w.w.) alipofariki, hapakuwa na hata mtu mmoja aliyekuwa tayari kuilinda haki. Mtu pekee ndani ya Madina aliyesimama kutetea haki alikuwa ni Zahra (s.a.). Kwa nini mtu mmoja tu? Kwa sababu mtu huyu hajawahi kamwe kuonyesha uzembe juu ya haki. Yeye hakuwahi kupuuza japo haki ndogo kabisa. Yeye Zahra (s.a.) alikuwa mstari wa mbele katika masuala ya uadilifu na haki. Lakini wakati milango ya kawaida ilipobishwa hodi kwa ajili ya uungaji mkono kwa ajili ya Ali (a.s.) kulikuwa na watu wapumbavu nyuma ya milango hiyo. Hata leo hii hodi nyingi zinabishwa milangoni na tunaifungua tu kumwambia muombaji huyo ajaribu mahali pengine, hatujali juu ya shida za wenye kuhitaji. Kuna riwaya ndani ya Nahjul-Balaghah ambamo Ali (a.s.) anasimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

"Muombaji anayekujia nyumbani kwako, huwa haji mwenyewe, bali Mwenyezi Mungu ndiye anayemtuma. Yeye ni mjumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu anayekuja kwako wewe, lakini mnamnyima kila kitu." Ukataaji huu wa haki ndogo ndogo wa watu binafsi ni uzembe na unapoanza kuonyesha ukosefu wa kujali kwenye haki ndogo ndogo unaishia kuwa asiye na ufahamu juu ya haki kubwa za msingi.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 102 4/25/2018 11:01:30 AM

## UPUMBAVU JUU YA YAZID

Sasa huu ulikuwa ndio ummah na Imam Husein (a.s.) upande mwingine. Imam Husein (a.s.) aliona kwamba uzembe wa ummah huu umegeuka kuwa upumbavu. Dalili na ushahidi wa ummah huo kuwa wa kipumbavu ulikuwa kwamba mtu kama Yazid anakuwa Khalifa. Kama nilivyosema kabla kwamba unapaswa kuuliza falsafa ya mageuzi haya kutoka kwa Imam Husein (a.s.) mwenyewe, juu ya ni kwa nini ameharibu mapumziko na amani yake ya maisha, akawachukua wanawe, mke na ndugu zake kwenye uwanja wa vita na tukio la Karbala likatokea. Kwa nini mapinduzi haya ya damu, na mapinduzi haya matukufu yaliendeshwa na yeye (a.s.). Yeye mwenyewe anasema:

"Wakati mataifa (ummah) yanapoanza kuwafuata watawala kama Yazid, basi hiki ndio kifo cha Uislam na haki."

Jambo muhimu la kulielewa hapa ni kwamba ilikuwa ni Yazid ambaye ni mpituka mipaka na mtu dhalimu, lakini sio ummah. Lakini anachokisema Imam Husein (a.s.) ni kwamba kukubali na kuishi chini ya utawala wa mtu katili, mvuka mipaka na mtawala dhalimu kama Yazid ni ushahidi wa upumbavu mkubwa wa ummah na Husein (a.s.) hapendi upumbavu na uzembe kama



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 103 4/25/2018 11:01:30 AM

huo. Kumfanya Husein (a.s.) kuwa Kigezo cha Mfano (Uswah) ni vigumu sana. Imam Husein (a.s.) anasema katika *Du'a-e-Arafa*: "Ewe Allah ninakushukuru kwamba uliimaliza serikali ya waonevu, madhalimu kabla ya kuzaliwa kwangu, na ukaunda serikali ya haki ambamo mimi nilizaliwa ndani yake." Mtetezi madhubuti wa uadilifu na haki kama huyo ni Husein (a.s.). Hawezi hata kuvumilia kuzaliwa chini ya kivuli cha serikali ya madhalimu. Yeye alizaliwa chini ya utawala haki ya kimbinguni. Kwamba Husein (a.s.) anaichukulia serikali ya haki ya kimbinguni kama neema ya kuzaliwa huku, ni vipi Husein (a.s.) ataweza kukubali kwa uvumilivu kabisa serikali ya kionevu kama hiyo katika uhai wake?

فَإِنِّي لاارَى الْمَوْتَ إِلاَّ سَعَادَةً (شَهَادَةً) وَ الْحَيَاةَ مَعَ الظَّالِمِيْنَ إِلاَّ بَرَمًا

**"Mimi ninapendelea kifo cha heshima kuliko kuishi japo siku moja ya uhai wangu pamoja na madhalimu." (*Mausuwatu Kalimati Imam Husein (a.s),* uk. 356)**

Sababu ya yeye kusema hivi ilikuwa ni kwa sababu yeye hakuwa mpumbavu. Mtu mpumbavu hukaa pamoja na ukatili, anaweza kupitisha maisha yake yote katika ufalme wa waonevu na wakandamizaji. Mtu mpumbavu vile vile hukubali kuishi maisha yake ndani ya serikali ambamo haki inakanyagwa wazi wazi. Burudani, anasa amani, masikilizano, cheo, nafasi, mamlaka na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 104 4/25/2018 11:01:30 AM

mahitaji muhimu ya maisha, mambo yote haya huwatupa wanadamu kwenye giza na upumbavu. "Tunahusika nini na vitendo vya serikali" huwa unakuwa ndio miito ya uhalalishaji kutoka kwa watu wapumbavu kama hao. Wao wanapuuza kila aina ya dhulma ya serikali hizo.

Lakini Imam Husein (a.s.) kamwe hakufikiri au kusema kwamba anahusika nini na Yazid isipokuwa atakaponidhuru mimi mwenyewe binafsi? Alishughulisha kuhusu mtu kama Yazid kuingia kwenye madaraka. Yeye (a.s.) alihisi kwamba ni wajibu wake kwamba katika kuwepo kwake serikali ya madhalimu haipaswi kuanzishwa na kusimama. Yeyote yule leo hii anayechukia serikali ya haki na anakerwa na kuazishwa kwa serikali ya Kiislamu, wanapaswa kuacha kujihusisha na Imam Husein (a.s.). Madhehebu ya Husein (a.s.) ni madhehebu ya Serikali ya Haki. Ni vipi atakavyoweza mtu anayechukia kuanzishwa kwa serikali ya haki ya kimbinguni kujiita Huseini? Husein (a.s.) ndiye mtu ambaye hawezi kuvumilia kuzaliwa chini ya serikali kandamizi na wala hakubali kutumia japo siku moja ya uhai wake chini ya serikali katili na kandamizi.

**فَإِنِّيْ لاأَرَى الْمَوْتَ إِلاَّ سَعَادَةً (شَهَادَةً) وَ الْحَيَاةَ مَعَ الظَّالِمِيْنَ إِلاَّ بَرَمًا**

**"Mimi ninapendelea kifo cha heshima kuliko kuishi japo siku moja ya uhai wangu pamoja na madhalimu."**

Lakini huu haukuwa wito wa ummah. Ummah huu ulikuwa hausomi wito huu wa Imam Husein (a.s.)

Wito wao ulikuwa kwamba ilikuwa ni sawa kama serikali ilikuwa inatenda uhalifu na udhalimu, basi ilikuwa ni vitendo viovu vya serikali na halina chochote cha kuhusiana na sisi. Ummah ulikuwa haulizingatii hili kama ni fedheha kuishi maisha yao chini ya serikali kama hizo, kwa sababu walikuwa ni wapumbavu. Na juu ya yote haya walimuuliza Husein (a.s.) kuhusu lengo la mageuzi yake haya. Majibu ya Imam Husein (a.s.) lilikuwa ni usutaji endapo kwamba je, ni halali kuniuliza swali kama hilo? Je, hamuwezi kushuhudia hili lengo lenye upana la mageuzi haya? Kama nilivyosema kabla mahali fulani kwamba kama tukiishi kwenye ulimwengu uliopinduka juu chini, basi hata maswali yanakuwa juu chini. Hili sio swali la kuuliza, ati kwamba kwa nini umeanzisha mageuzi haya? Swali ambalo lingeulizwa ni lingekuwa ni kuhusu wale waliobakia kimya. Ni sawa kabisa na kile kinachotokea hata leo hii pia wakati mtu mmoja anapozungumzia juu ya haki, anashutumu dhulma na anaongea dhidi ya madhalimu, watu wanamuuliza juu ni nini kilichomkuta, kwa ubora zaidi, wale ambao hawaongei na wako kimya tu wangeulizwa. Hii ni kwa sababu dunia hii yetu iko juu chini, chini juu, na katika dunia ya namna hiyo ni maswali kama hayo tu yanayoweza kutarajiwa.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 106 4/25/2018 11:01:30 AM

Dunia hii ya kipumbavu iliyopinduka, maswali ni kuhusu, ni kwa nini Husein (a.s.) alianzisha mageuzi haya? Ambapo wanapaswa kuwa wanawauliza wale waliokaa kimya kwamba ni kwa nini hawakuanzisha mageuzi? Swali kama hilo liliulizwa kuhusu mageuzi ya Imam Khomein (r.a.). Kwa nini watu hawawaulizi wale ambao hawachukui hatua yoyote ile kuelekea kwenye haki, ambao hawaongei kamwe dhidi ya madhalimu? Kukaa kimya wakati dhulma inaendelea kunapaswa kutiliwa shaka.

## LENGO LA MAGEUZI

Imam Husein (a.s.) mwenyewe alielezea lengo lake mwanzoni kabisa. Huu ulikuwa ni ujumbe uliodhihirika wazi kabisa ambao haukuhitaji kuzungumziwa sana, lakini bado kwa wale watu wapumbavu wasio na fahamu, yeye Husein (a.s.) mwenyewe kwa uwazi kabisa alitangaza lengo la mageuzi yake. Alisema nini?

**الاَ تَرَوْنَ إِلَى الْحَقِّ لاَ يُعْمَلُ بِهِ وَ إِلَى الْبَاطِلِ لاَ يُتَنَاهَى عَنْهُ لِيَرْغِبَ الْمُؤْمِنُ فِي لِقَاءِ رَبِّهِ حَقًّا**

**"Hamuoni kwamba haki haitendeki, hamuwezi kuona kwamba uwongo haukatazwi?"**
***(Mausuwatu Kalimate Imam Husein (a.s.)*** **–** uk.356)

Lafudhi hii **"Je hamuoni,"** inatumika wapi? Hii inatumika wakati pale unapokuwa umeshughulika sana na jambo fulani na mtu mwingine anahoji juu ya kitendo hicho hicho, kwa mfano, kama hakuna taa na unajaribu kuwasha mshumaa, na mtu anakuuliza kwa nini unawasha mshumaa huo, hivi wewe utalijibu vipi swali hilo? Kwa kweli wewe utamuuliza kwamba, je wewe ni kipofu, kiasi kwamba huoni kwamba hakuna taa? Kadhalika wakati ule Imam Husein (a.s.) alichoma mshumaa wa uongozi katika giza la haki, kila mtu alimuuliza, kwa nini alikuwa anafanya hivyo? Hivyo Husein (a.s.) aliwauliza kama walikuwa ni vipofu. Walikuwa hawaoni kwamba watu wamekuwa wazembe na wapumbavu kwenye ukweli na haki (Haqq)? Hamuoni kwamba haki haitendeki?

Sasa swali ni, ni nani ambaye alikuwa mpumbavu kuhusu haki? Je, ilikuwa ni watawala tu pamoja na Yazid? Kama ilikuwa ni mtawala tu ambaye ndiye alikuwa mpumbavu basi angeweza kutengwa ili kwamba ugonjwa huu usienee na kuwafikia wengine. Lakini wakati ugonjwa unapokuwa ni wa mlipuko basi unahitaji dawa ya tofauti kabisa. Uzembe huu na upumbavu umekuwa ni ugonjwa wa mlipuko unaoenea kila mahali. Uislamu unatuvutia kwenye haki na uadilifu, Uislamu unatufundisha kuilinda haki na unatutegemea



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 108 4/25/2018 11:01:30 AM

sisi kuwa watetezi wa haki. Usiogope hata kufa katika kuilinda haki, Uislamu ule ule wenyewe umekuwa ni muathirika wa uzembe na upumbavu.

Licha ya Uislamu kuwepo, bado mbele ya Waislamu haki zinakanyagwa na wao hawaonyeshi kujali hata kidogo. Hiyo ndio sababu Imam Husein (a.s.) aliuuliza ummah endapo kama umekuwa pofu. Huu ndio ulikuwa ugonjwa wa mlipuko. Wewe na mimi hatuhitaji kufanya ufafanuzi wa tukio hili la Karbala, kwa sababu lilifanywa na Husein (a.s.). Yeye amekwisha kutoa maelezo juu ya lengo na madhumuni ya mageuzi haya kabla ya kuuliwa kishahidi. Yeye alisema:

إِنِّيْ لَمْ اَخْرُجْ اَشِرًا وَّ لاَ بَطِرًا وَّ لاَ مُفْسِدًا وَّ لاَ ظَالِمًا و إِنَّمَا خَرَجْتُ لِطَلَبِ الْاِصْلَاحِ فِی أُمَّةِ جَدِّی أُرِيْدُ اَنْ اَمُرَ بِالْمَعْرُوْفِ وَ اَنْهَی عَنِ الْمُنْكَرِ وَ اَسِيْرُ سِيْرَةَ جَدِّی وَ اَبِيْ عَلِيَ بْنِ اَبِی طَالِبْ

**"Mimi sikutoka ili kueneza shari wala dhuluma, bali nimetoka kwa ajili ya kurekebisha umma. Nitalingania kuamrisha mema na kukataza maovu ambapo ilikuwa ni tabia ya jadi zangu na baba yangu Ali bin Abi Talib (a.s.)."** ***(Mausuwatu Kalimate Imam Husein (a.s.)*** **– uk. 291).**

Kama ninyi (watu) mnaniuliza mimi lengo la Karbala, basi nawaambia kwamba, lengo na madhumuni yangu ni kufanya mageuzi. Sasa kuna swali, kwamba



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 109 4/25/2018 11:01:30 AM

ni nani anayehitaji kubadilishwa? Mabadiliko yanahitajika kwa wale ambao ni madhalimu. Ni nani aliyekuwa ni dhalimu, ni Yazid au ni ummah? Yazid alizaliwa kiharamu; udhalimu wake ulikuwa unatambulika vyema na ulimwengu wote. Lakini kulikuwa na udhalimu uliofichika ndani ya ummah ambao hakuna yeyote aliyeweza kuuona, ulihitaji macho mapenyevu ya Husein (a.s.). Imam Husein (a.s.) aliiangalia sababu ya kwa nini watu kama Yazid wanakuja madarakani. Hii ilikuwa ni kutokana na uzembe na upumbavu wa ummah uliofanya Yazid aingie madarakani. Uzembe huo ulizidi mno wakati Husein (a.s.) alipowalingania watu wa Madina kuungana naye, yeye pia aliuita ummah wa Mahujjaji huko Makka, lakini ni wangapi waliomuunga mkono Imam (a.s.)? Kumuabudu Mwenyezi Mungu na kwenda Hijja sio ushahidi wa mtu kuwa muadilifu na mkweli. Wakati uleule hasa wa hijja, Husein (a.s.) aliamua na kutangaza kwamba alidhamiria kuumaliza ugonjwa huu wa mlipuko, je ni kiasi gani mwaliko wa Husein (a.s.) uliwaathiri Mahujjaji hao? Katika Hijja yote, katika hali ya Ihraam, uzembe na upumbavu ulionyeshwa kuelekea kwenye wito wa kusimamia Haki. Ule ummah uliokuwa mzembe na pumbavu ulibakia kushughulika na kufanya Taratibu za Ibada ya Hijja.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 110 4/25/2018 11:01:30 AM

Husein (a.s.) alihisi kwamba kama upumbavu huu utaendelea kwa namna hii, basi maangamizi sio tu ya ummah pekee bali hata yale ya Uislamu pia yapo karibu mno, na Husein (a.s.) ndio jahazi la wokovu. Sasa wewe mwenyewe amua na ujibu, kama mtu anapokuwa mpumbavu na kukosa fahamu, na ukitakiwa kumuokoa, je utamuokoa vipi? Kwa kweli utajaribu kumrudisha kwenye akili zake timamu, utarudisha hisia zake kuwa hai, na utaondoa ukosa fahamu wake.

Sasa endapo jamii yote na ummah wakiwa hawana fahamu na wakawa wazembe, na jahazi la wokovu linakuja kuwanusuru, ni nini jahazi hili la wokovu litakalofanya kwanza? Atawarudisha kwenye fahamu zao, atajaribu kuwafanya wahisi, lakini vipi? Kama upumbavu huu utakuwa wa kina kabisa, kama ule wa kuwa mlevi wa heroini na pombe ambao unaweza kutibiwa au kumalizwa kwa kuwapa vitu vya chachu vya kula. Itakuwaje kama ulevi huu ni mzito sana kutokana na uzembe kwenye haki na upumbavu huu pia unafunikwa pazia chini ya vitendo vya dhahiri vya kiibada. Kama mtu anasoma utajo mtukufu – dhikr – katika hali ya ulevi, basi visomo hivyo haviwezi kuchukuliwa kama ni ibada.

Hivyo Imam Husein (a.s.) aliwaambia wale Mahujjaji kwamba katika sehemu hii ya ibada matendo yenu



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 111 4/25/2018 11:01:30 AM

ni kama ya yule mtu asiye na akili timamu ambaye anasoma nyuradi katika hali ya kutokuwa na fahamu na hii sio ibada. Kwanza amka wewe mwenyewe, kwa sababu katika hali ya ulevi chochote utakachozungumza kitakuwa ni upuuzi usio na maana. Kama unataka kutoa kauli za busara basi kwanza rudi kwenye akili yako timamu. Lakini ulevi huu hautaondoka kwa kutumia dawa zenye chachu tu, kwa kweli dawa kali kabisa zinahitajika. Mwanadamu ambaye ni mzembe na mpumbavu kuhusu haki ni kama aliye katika hali ya furaha kubwa, anakaa, anakula na kulala kwa starehe kabisa, na hivyo ulevi huu hauwezi kutoweka kwa kula vyakula vya chachu vya kawaida, kwa hili tunahitaji dawa kali sana na chungu. Maagizo ya dawa za kumrudisha mtu kama huyo kwenye akili zake timamu ni magumu sana na hasa pale inapokuwa ni ummah wenyewe, ummah unahitaji kuamshwa na kusimamishwa imara.

Hii ni kwa sababu kuzembea huku juu ya haki hauzaliwi leo kuwa ni mpya, bali umezeeka sana. Hadhrat Nuh anasikitika katika swala zake kwamba ninapaswa kushughulika na ummah usio na fahamu na wa kipumbavu. Nabii Ibrahim anaomba: Ewe Mola Wangu, ninashughulika na ummah mpumbavu. Nabii Musa anaomboleza kwa maumivu ya ummah huu mpumbavu. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ilibidi



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 112 4/25/2018 11:01:30 AM

ahame kwa ajili ya upumbavu huu. Ali (a.s.) aliachwa peke yake kwa ajili ya upumbavu huu. Hasan (a.s.) alitengwa kutokana na upumbavu huu. Husein (a.s.) hakutaka watoto wake nao wawe mawindo ya upumbavu na hataki dini hii kutumbukia kwenye shimo la upumbavu daima. Husein (a.s.) hakuwa tayari kukubali dini kuangukia kwenye ibada ya kutetemeka na mazungumzo ya kijinga ya ulevi. Yeye alitaka kuuondoa ulevi huu ambao ulikuwa umeenea kama gonjwa la mlipuko. Mlipuko huu umeingia kwenye mshipa hasa wa ummah, na kuutokomeza huu ummah ulibidi kuamshwa. Hauwezi kuamshwa kupitia vita na silaha, unaweza kushinda na kupata nchi na rasilimali kupitia madaraka, lakini huwezi kuyabadili mataifa na fahamu zao kwa nguvu. Majeshi na mabavu haviwezi kuamsha ummah kuelekea kwenye maadili (*Aqdar*). Husein (a.s.) anataka fahamu zilizoamka, anataka kuvunja mvuto wa uzembe, lakini kivipi? Unahitaji kuvunjwa kwa dhoruba nzito. Katika bahari hii iliyotuama, inahitajika kuanzisha tufani. Sio rahisi kuanzisha tufani hii katika ummah.

Kama unavyoweza kuona pale unapotupa kijiwe kidogo ndani ya maji kwamba kinasababisha mawimbi yanayosogea, mawimbi haya yanakwisha baada ya muda mfupi. Lakini unapotupa jiwe baharini hutaweza



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 113 4/25/2018 11:01:30 AM

kuona wimbi lolote. Ili kusababisha wimbi katika bahari kubwa, basi jiwe kubwa kabisa au mlima unahitajika kutupwa humo. Kadhalika, mpaka na isipokuwa shaksia kubwa kama Husein (a.s.) atakapoacha kuruka kwenye bahari hii iliyotulia ya ummah huu, basi hakuna wimbi litakalotengenezeka, na wimbi hili linapaswa kudumu hadi Siku ya Kiyama. Mtu mashuhuri kama Husein (a.s.) alitengeneza wimbi hili katika bahari iliyotuama ambamo mawimbi yake bado yamo hadi leo hii, na yatakuwepo hadi Kiyama. Wimbi hili litakuwa linaamsha dhamira za wanadamu hadi Siku ya Kiyama, litakuwa linaamsha watu wapumbavu hadi siku ya Mwisho.

Kwa hiyo je, mpaka sasa umeelewa kwa nini Husein (a.s.) alianzisha mageuzi haya? Imam Husein (a.s.) ameokoa juhudi na mitume wote; yeye ndiye mrithi wa mitume. Ni mrithi wa namna ambaye ametoa mali yote ya kizazi chake. Husein (a.s.) sio jahazi la wokovu kwa wenye dhambi tu bali yeye ni jahazi la wokovu kwa ajili ya dini, yeye ni jahazi la wokovu kwa matatizo ya mitume, ni jahazi la wokovu kwa ajili ya dhamira ya ubinadamu. Hii ndio falsafa ya mageuzi ya Mkuu wa Mashahidi (a.s.). Na ni mtu yule tu, anayeweza kuchukuliwa kuwa karibu na Karbala, yule ambaye amezinduliwa na Karbala, yule ambaye



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 114 4/25/2018 11:01:30 AM

anatikiswa na Karbala, yule ambaye kuwepo kwake Karbala kunasababisha dhoruba na tufani. Nimesema mwanzoni mwa mjadala huu kwamba isipokuwa pale roho na kiini cha mageuzi ya Husein (a.s.) kisipoeleweka sawa sawa, inaweza kuwa kama kile kidonge ambacho hakipewi mazingatio ya sawa sawa ya kumuamsha mtu aliyekosa fahamu kinavyoweza kuwa chanzo cha kifo chake.

## KARBALA – TUFANI YA MZINDUKO

Karbala ni jina la kusababisha matufani katika maisha wa watu na sio kuwafanya watu walale usingizi. Azadari ni jina la mzinduko wa watu kutoka kwenye usingizi mzito. Ni dalili ya maisha na uhai; kuhuzunika na kuomboleza huku ni kule kwa fahamu, maisha, uhai na hisia za maumivu. Hii ni dalili ya maisha na uhai. Hivyo kama mtu atakuwa hakulia basi mlazimishe alie. Azadari hii ni kama yule mtoto mchanga anayezaliwa ambaye kama hakulia atachukuliwa kana kwamba amekufa. Mtoto huyu ni lazima apewe hisia za haki. Falsafa ya Husein (a.s.) ni falsafa ya mwenye heshima kubwa juu ya haki. Mtu anayeheshimu ukweli, haki na uadilifu. Karbala ni shule ya itikadi. Usiichungulie falsafa ya Karbala kupitia madirishani, bali uielewe kupitia mazungumzo ya Imam Husein (a.s.). Kila jicho ni dogo kwa Karbala isipokuwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 115 4/25/2018 11:01:30 AM

lile la Husein (a.s.) ambalo linaona peo zote za Karbala. Na ni Husein (a.s.) ambaye anasema:

الاَ تَرَوْنَ إلَى الْحَقّ لاَ يُعْمَلُ بِهِ وَ إلَى الْبَاطِلِ لاَ يُتَنَاهَي عَنْهُ

**"Je, hamuoni kwamba haki haitekelezwi? hamuwezi kuona kwamba uwongo haukatazwi?"**

Husein (a.s.) anauliza kwamba hamuoni kwamba watu wamekuwa wazembe kuhusiana na ukweli, hawana ufahamu kwenye haki. Sio haki yangu kuwatoa kwenye lepe hilo la usingizi mzito? Je, nami pia nibakie kuwa mzembe na niseme kwamba mimi nifanye nini kuhusu hilo, na nikae kimya nikijishughulisha na mambo yangu binafsi ya maisha? Husein (a.s.) hawezi kuvumilia ukanyagwaji wa haki. Kutokea hapa tunaweza kuelewa, iwapo kwamba madai ya Yazid kwa kumtaka Husein (a.s.) akubali kiapo cha utii kwake yalikuwa ndio sababu ya mageuzi ya Husein (a.s.) au ni ule mwaliko wa watu wa Kufa? Watafutaji wa haki hawahitaji mwaliko wowote wa kusimama kwa ajili ya haki, bali wale ambao hawajitambui,wazembe na wasio na fahamu hawaji hata baada ya mialiko mingi.

Huhitaji kuwaalika wafuasi wa haki kwani wao wanalichukulia hili kama ni wajibu wao. Ni watu wa Kufa wanaopaswa kuamka kwa mwito wa Imam Husein (a.s) au ni Imam anayepaswa kuja kwa mwaliko



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 116 4/25/2018 11:01:30 AM

wao? Husein (a.s) ndiye anawaita wao na sio watu wa Kufa wamwite Husein (a.s).

Nabii Nuh (a.s) alisema. "Nimewalingania.´Husein (a.s) ni mrithi wa Nuh. Nuh anawaambia ummah wake. "Ninawaiteni ninyi, sio nyinyi muniite mimi. Niliwaiteni na nyinyi hamkuitikia "L!B!IK!" (Niko chini ya mamlaka yako) kwenye mwito wangu." Husein (a.s) alikuwa mlinganiaji. Yeye aliwalingania vizazi vyote hadi Siku ya Kiyama. Yeye ametoa somo la kuwa mfuasi wa haki. Yeyote anayemkubali Husein (a.s) kama kigezo cha mfano (Uswah) kwake, muonekano wake utakuwa vipi?

Wakati wanafunzi na wanatheolojia wote walipokuwa wakishughulika katika kazi ya uchambuzi, uchunguzi na utafiti wao, wakiwa wamekaa majumbani, mashuleni na maktaba, kulikuwa na mwalimu mmoja, faqihi na mwanatheolojia ambao walikuwa hawatulii. Kila mmoja wao alishangazwa kuhusu kutotulia kwake na kumuongoza yeye kuwa kama wao. Walikuwa wakimwambia, je hutuoni sisi? Kama watu wakubwa na mashuhuri wengine hawazungumzi, nini kimekutokea wewe? Kwa nini na wewe hunyamazi na kuwa kimya? Lakini kwa faqihi mkubwa huyu, yeye alikuwa amepoteza amani na utulivu wake. Anahisi kuwasiki-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 117 4/25/2018 11:01:30 AM

tikia wengine kwa vile hawakumuelewa Husein na Karbala, vinginevyo na wao pia wangehangaika kama yeye. Nafsi isiyotulia kama hiyo kisha inainukia na kusimama kuwa Khomeini (r.a), mtu ambaye aliielewa falsafa ya Karbala. Kuna mifano mingi ya watu ambao walimfanya Imam Husein (a.s) kuwa Kigezo cha Mfano kwao kama Shahiid Mudhaffar Kirmani; kuna tofauti gani kati yetu na Kirmani? Tofauti ni kwamba yeye alielewa ile falsafa ya Karbala na hivyo tufani ikaibuka kutoka ndani yake yeye.

Ndani ya bahari ya kimya cha upumbavu kwenye haki, Karbala ni jina la dhoruba, tufani ambayo inasababisha mawimbi ya uamsho. Tunayo Karbala kwenye midomo na ndimi zetu tu, bali sio kwenye uhai wetu. Tunaye Husein (a.s) kwenye ndimi zetu lakini hatuitambui falsafa yake. Karbala ni nini kwetu sisi? Kupitia Karbala tunayatimiza maombi yetu kwa ajili ya tamaa zetu za kidunia, tunajaribu kuomba kupata msamaha kwa madhambi yetu, tunaiona shifaa, tunapata kupitisha matakwa yetu, na tunaitumia kwa kila kazi ili kuikamilisha kwa mafanikio. Hapana shaka yoyote kwamba hizi hazifanyi kazi, yote haya yanatokea kwa sababu Karbla ni ina nguvu kiasi hicho, lakini hii sio falsafa ya Karbala. Si kama unakuja Karbala na kurudi baada ya kutafuta na kupata matamanio yako ya kidunia na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 118 4/25/2018 11:01:30 AM

wokovu tu. Ni lazima kuja kuelekea Karbala na kupata wokovu,lakini sio kwa kuigusa tu Karbala,wokovu huu unapatikana kwa kukuza akili ya utambuzi wa kutokuwa mzembe kwenye haki kwa kupata masomo juu ya ukweli,haki na uadilifu. Maimam Ma'sumin (a.s) wametilia mkazo sana juu ya Ziarat (heshima kuu) kwa Karbala. Walikwenda wao wenyewe Karbala. Kwa sababu Karbala ni somo la upendo na haki,Karbala inatuzuia sisi kuwa wapumbavu.Karbala inawaalika wanadamu kwenye kweli, haki na uadilifu. Mwaliko wa Karbala ni wa kudumu na upo hata leo hii.

## WITO WA KARBALA NI WA KUDUMU

"Je, wapo wa kutunusuru sisi" (Mausuwatu Kalimate Imam Husein (a.s.) –uk. 506).

هال من ناصر ينصرنا

Ni lini wito huu ulipotangazwa na Imam Husein (a.s.)? Ulikuwa ni wa kuja na kuokoa familia yake,jamaa,watoto na wafuasi? Kauli hii ilitangazwa wakati kukiwa hakuna hata mtu mmoja aliyebakia. Hivyo je, alikuwa akiomba msaada yeye mwenyewe binafsi? Kuokoa maisha yake mwenyewe? La hasha! Husein (a.s.) alikuwa ameamua kwa dhati kabisa kufa kishahidi na yeye (a.s.) yupo tayari



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 119 4/25/2018 11:01:30 AM

kuuliwa kishahidi, hivyo ni kwa ajili ya nani na kwa nini anahitaji wasaidizi sasa? Jibu la Husein (a.s.) litakuwa ni nini? Jibu lake litakuwa:

الاَ تَرَوْنَ إلَى الْحَقّ لاَ يُعْمَلُ بِهِ وَ إلَى الْبَاطِلِ لاَ يُتَنَاهَي عَنْهُ

**"Hamuoni kwamba haki haitendeki,hamuoni kwamba uongo haukatazwi?"**

Husein (a.s.) anasema. "Nimeleta jahazi la haki hadi Karbala. Nimeileta haki hadi siku hii ya !shura hapa Karbala. Je, somo hili juu ya haki liishie na kufungwa leo? Leo nimejaalia uhai kwenye hisia ya haki (katika siku ya Ashura). Leo nimezindua hisia ya mapenzi juu ya haki." Sasa Husein (a.s.) anahitaji wasaidizi watakao endelea kufanya jambo hilohilo,ambao watadumu katika kuamsha hisia za haki,kweli na uadilifu hadi Siku ya Kiyama.

Imam Sajjad (a.s.) alikuja baada ya kusikiliza du'a hii ya Husein (a.s.). Hakuwa ni Sajjad ambaye tunamchukulia kama mtu mgonjwa na dhaifu ambaye alikuwa hatambui kilichokuwa kikitokea katika uwanja wa vita, katika tafsiri yetu ya kawaida juu ya shaksia yake, yeye alikuwa yule ambaye alikuwa wakati wote akimuuliza baba yake kuhusu walipokuwa watu wote wa familia na wafuasi, sio yule Sajjad yule. Bali ni yule



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 120 4/25/2018 11:01:30 AM

Sajjad (a.s.) anayemwambia shangazi yake kwamba nimesikia ule wito wa ufukara, nimesikia du'a ya mtu fukara masikini aliyetengwa ambaye anaomba msaada, hivyo niletee upanga wangu kwani nataka nitoke nje nikamsaidie. Na katika alfajiri ile ya Ashura kila jicho lilikuwa linashuhudia mandhari hii; kwamba mtu mgonjwa na mkono wake mmoja juu ya bega la mwanamke na upanga kwenye mkono mwingine alitoka nje kwenye uwanja wa vita. Lakini Imam Husein (a.s) alimrudisha ndani kwa kumthibitishia kwamba kizazi cha haki kinapaswa kuhifadhiwa kupitia kizazi chake. Safu ya wafuasi wa haki na uadilifu inapasa kuhifadhiwa. Ingawa madhalimu waliamua kuumaliza uzao wa wafuasi wa haki, lakini Imam Husein (a.s.) alimwambia Sajjad (a.s.) kwamba ni lazima kiokolewe. Hakusema kwamba huhitaji kuuliwa kishahidi, lakini Imam Husein (a.s.) alichoambiwa Sajjad (a.s.) ni kwamba nimeazisha na kuinua hisia za ufahamu hadi alfajiri hii ya Ashura, na sasa wewe unahitaji kuubeba ujumbe huu mbele kwa watu wasio na fahamu wa huko Shaam na Kufa ili kuwaamsha..

Kwa hiyo, wafuasi wa kwanza wa Imam Husein (a.s.) katika jangwa lile hame la Karbala walikuwa ni Sajjad (a.s.) na bibi Zainab (s.a.), hadi leo hii wito wa kudai kuungwa mkono Husein (a.s.) ungalipo. Husein



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 121 4/25/2018 11:01:30 AM

anahitaji wafuasi wa waunga mkono ambao wanaweza kubadilisha mazingira ya uwenda wazimu. Wafuasi hawa wasije wakawa wanasoma mashairi tu kwa jina la Karbala na wakawafanya watu wakakoroma na kulala, wanahitaji kuwaita watu kwenye haki na uadilifu.

Kwa nini Imam Khomein (r.a.) alisema. "Mimi sina chochote kilicho pamoja nami isipokuwa Karbala.?" Imam Khomein (r.a.) anasema kama leo unaliona taifa hili kama la kiadilifu, leo kama dunia inatuona sisi kama wachocheaji wa haki, leo hii kama unaniona mimi sio mzembe kwenye masuala ya haki, si mpumbavu kwenye kweli, kwa nini sifanani na wengine, ningeweza pia kukaa ndani ya nyumba yangu na kwenye madrasa nikitoka mihadhara, nikiendesha utafiti wangu na kutojihusisha na udhalimu unaofanyika katika jamii. Kwa nini mimi nimekubali kutupwa nje ya mipaka, kwa nini nimekubali kuwa muathirika wa lawama na kukubali kuishi maisha ya ukimbizi? Mmeona ni miaka mingapi ambayo nimekaa chini ya maroketi na mabomu. Ni nani aliyetwaa amani hii na utulivu kutoka nafsi yangu? Imam Khomein (r.a.) anasema. "Yote haya ni kutoka Karbala." "Nimechukua uhangaikaji huu kutoka kwa Husein (a.s.), (a.s.), nimejifunza uadilifu huu kutoka kwa Husein kwa sababu Husein (a.s.) ni mhadhiri wa haki".



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 122 4/25/2018 11:01:30 AM

Haiwezekani kwamba mtu anabakia kuwa mzembe kwenye haki na bado achukuliwe kuwa mfuasi wa Husein (a.s.). Mpaka Siku ya Kiyama, kama mtu anataka kufuata njia ya haki, basi somo la haki ni yale mapambano ya Karbala.

Tumuombe Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Husein, atufanye sisi sote kuwa watu wa haki na auondoe huu ujinga kuhusu haki. Ewe Mola! Namna Maula wetu Ali (a.s.) alivyosema kwamba kwenye kichuguu na mchwa, siko tayari kufanya hivyo, kwa namna hiyo hiyo tumuombe Mwenyezi Mungu asitupe sisi uwezo wa kupora haki ya mtu yoyote na kuikanyaga haki. Ewe Allah! kama tumekuwa wazembe na wajinga kuhusu haki, basi tunakuomba ubadilishe uzembe huo wa nyuma yetu kuwa hisia ya haki leo hii. Tujaalie fursa ya kufuata tabia na mwenendo wa Husein (a.s.) na umfanye yeye kuwa kigezo chetu cha mfano (Uswah). Tujaalie fursa ya kuelewa na kuufikia moyo wa Karbala. Tujaalie fursa ya kuelewa uhalisia wa mapambano ya Husein (a.s.). Ewe Mola Wetu! Kwa jina la ile damu tukufu ya Husein (a.s.) tufanye sisi tuwe ni wenye kuitikia wito wa msaada kutoka kwa Imam Husein (a.s.). Kwa namna Mashahidi wetu wapenzi walivyoitikia kwenye wito wa Husein (a.s.) na kupata shahada, tujaalie na sisi kifo cha namna ile ile. Ewe Mola Wetu! Kila mmoja wetu atakufa, lakini pale kifo chetu kitakapodaiwa, kifo



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 123 4/25/2018 11:01:30 AM

chetu nakiwe kama kinachofanana na kile cha Husein (a.s.). Tujaalie kifo cha Kishahidi.

## NI MWANZO NA WALA SIO MWISHO

Kuna mada nyingi kama hizi za kujadili ambamo tuna matarajio kwamba mkusanyiko mpana wa elimu utahamishiwa kwetu katika mstari mmoja au miwili. Katika zama hizi matarajio yetu ni kukusanya elimu yote katika maneno: ndio au hapana. Sijajaribu kamwe na kukamilisha mada yoyote ile, wala sina uwezo wa kufanya hivyo, na kamwe sijawa na nia ya kukamilisha mada, hata kutoa taarifa za msingi kuhusu mada fulani ni vigumu sana.

Mada za namna hiyo kamwe huwa hazifikii ukamilifu wake na wala hata ile nia ya kuzichukua kuelekea kwenye ukamilifu wake na wala hata ile nia ya kuzichukua kuelekea kwenye ukamilifu wake. Nia na juhudi zangu ni kiasi cha kuanza tu mada kama hizo ambazo hazijaanzwa bado. Wala hata sijui kama nimefanikiwa katika hii pia, kwa sababu kuna mada nyingi sana ambazo zimefungwa kabisa, zimo katika mabano yaliyofungwa na zinahitaji kufunguliwa. Mambo haya yamelala kwenye madonge ya kapsuli na masanduku yaliyofungwa na sisi tunajihisi kama kwamba



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 124 4/25/2018 11:01:30 AM

tunajua mengi kuhusu mada hizi, na hili ni kosa letu dogo kwamba mada nyingi ambazo zinategemea kuchokonolewa ndani ya Majalisi na kutoka kwenye mimbari wala hazijafunguliwa bado. Hivyo faida ninayoipata kutokana na fursa kama hizo ni kujaribu kuzichokonoa mada hizi, kisha wale wenye uwezo watazichukua wenyewe kuelekea kwenye kuzikamilisha. Wale wenye kustahili,wenye uwezo, wenye nguvu, wale wanaoweza kuchanganua na kufikiri juu ya mada mbalimbali, watu kama hao Mwenyezi Mungu akipenda watazichukua mada hizi hadi kwenye mahitimisho na vile vile watazitekeleza mada hizi katika maisha yao.

Hivyo ilikuwa ni lazima kuthibitisha hili kwamba hakuna mada ambayo imewahi kukamilisha kamwe. Najihisi furaha wakati baadhi ya amasa zinapoanzishwa na watu mwishoni wanatoa maoni yao na mawazo. Kumekuwa na baadhi ya mada ambazo zimewahi kujadiliwa kwa muda wa siku 15, lakini baada ya hapo pale washiriki wanapokuja kusema kwamba kiu ya mada hii bado haijakatwa, kwa kweli nasikia furaha sana kwa kauli kama hizo. Mungu aepushilie mbali kwamba washiriki hawa wasije wakahisi kwamba kila kitu kimetajwa na kwamba mada fulani imekamilishwa, hivyo najihisi utulivu pale ninaposikia kauli kama hizo, na hii ndio sababu mimi ninaeleza kwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 125 4/25/2018 11:01:31 AM

uwazi kabisa hili pia mara nyingi sana kwamba mada hiyo ilikuwa mwanzoni tu na sio mwishoni. Lengo sio kuzima ile kiu tu, kwa kweli nina omba kwa Mwenyezi Mungu akufanyeni muwe na kiu zaidi, na kwamba siku isije ikafika ambapo tukawa hatuhitaji kitu chochote, na tukawa tunasema kwamba sasa kiu zetu zimezimwa. Kazi yangu sio kukata kiu zenu, bali ni kuwaongezea kiu hizo. Wakati mwingi watu hawahisi njaa ama kiu, wanapoteza hisia zao za njaa na kiu, halafu wazazi hawampeleki mtoto kama huyo kwenye mgahawa kwenda kuondoa njaa yake, wanampeleka hospitali ili aweze kuhisi njaa, hamu yake ya chakula ichangamke tena. Wanamwambia daktari kwamba mtoto huyo hasikii njaa. Wakati kwenye nyanja ya elimu na Utambuzi tukiwa hatuhisi kiu, basi tusiende kwenye mgahawa bali tupaswe kwenda hospitalini. Nenda kamwambie daktari kwamba mimi sijihisi ile haja ya kiu ya elimu. Pale ninaposikiliza maneno machache tu najihisi nimepata elimu ya kila kitu. Hii sio hali nzuri na inahitaji matibabu.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hata baada ya kufikia hadhi ya kiwango cha elimu ambacho kwamba Mwenyezi Mungu swt. amesema kwamba yeye (s.a.w.w.) ni kielezi cha juu kabisa cha elimu ya kimbinguni, bado yeye (s.a.w.w.) anasema kwamba: رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 126 4/25/2018 11:01:31 AM

**“Mola Wangu niongezee elimu.”** (Surat-Taha aya ya 114). Nifanye niwe na kiu zaidi. Kuna hadith moja zaidi hapa. “Ewe Mola Wangu niongezee mishangao yangu (hairat),” nifanya nishangae zaidi, kwa sababu siku mwanadamu anapohisi kutosheka na akawa hahisi mshangao wowote, huu ni uzembe na upumbavu kuhusu nafsi zetu wenyewe. Kwa sababu Nyanja hii iko kwa namna ambavyo jinsi mtu anavyozidi kusonga mbele katika kutafuta na kupata elimu ya mbinguni, mishangao yake na mahitaji kwa ajili ya elimu zaidi na maarifa inaongezeka. Kama tukimchukulia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama kigezo chetu cha mfano, halafu yeye baada ya kufikia hadhi kama hiyo anaomba mishangao zaidi kwa ajili ya elimu ya Mwenyezi Mungu. Kujua maneno machache hakumaanishi kwamba tumeelimika, hivyo mwanadamu anapaswa kamwe kuzima utambuzi wake juu ya kiu ya elimu.

Fursa hii imekuja kufikia mwisho na sio lile somo lenyewe. Sijui kama hata hilo somo lenyewe limeanzishwa kamwe au hapana katika siku chache hizi. Juhudi hazikuwa ni kuligusa somo lenyewe ili kwamba wasomi waweze kuanza kulichunguza. Ni lazima kufungua mada kama hizo ndani ya watu nao waanze kufikiri kuhusu mada hizo. Hivyo siwezi hata kuhakikisha kwamba nimefanikiwa katika kuianzisha mada hii ama hapana.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 127 4/25/2018 11:01:31 AM

## MASWALI NA MAJIBU

**Swali la Kwanza: Kwa nini Imam Husein (a.s.) ambaye alikuwa akiyatambua yale yote ambayo yalikuwa yatokee, akawachukua pamoja naye wanawake na watoto?**

**Jibu la Kwanza:** Sasa kama sababu halisi ya Karbala ilikuwa inaeleweka, basi hili lisingekuwa ndilo swali bali kwa kweli swali lingekuwa ni kwa nini wale walioachwa nyuma walibakia nyuma? Sio kama Imam Husein (a.s.) alimlazimisha yeyote yule. Hata hivyo alitoa mwaliko kwa wote, lakini bado aliacha mwanya wa kuamua kufuatana naye, iwe kama ni ndugu zake wa karibu au hapana. Ndio maana tunaona kwamba hata wale ndugu wa damu hawakuandamana naye, hata ndugu yake Muhammad ibn Hanafiyya hakufanya hivyo au shemeji yake, na walikuwepo wale ambao hawana udugu naye ambao walifuatana naye. Halafu pia walikuwepo wale walioingia kuwa Waislamu hapo Karbala na kisha wakauliwa kishahidi hapo hapo. Huu ndio umaridadi wa kadhia hii ya Karbala, na hivyo tunahitaji kutafakari kwa makini kabisa juu ya kadhia hii ili kuielewa ile njia inayotuonyesha sisi ili kuifuata.

Hapo Karbala, baadhi ya wauaji pia walikuwa ni ndugu, kama vile Umar bin Saad au Shimr. Kipimo



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 128 4/25/2018 11:01:31 AM

cha kuwa na mtu sio udugu. Historia ya Maimam ni ya kushangaza sana na moja ya sababu kwamba tunaishi kwa furaha na hatusumbuliwi na somo hili ni kwa sababu hatuielewi historia hii. Hatuitambui hata ile historia ya Karbala au Imam Ali (a.s.) au Imam Ridha (a.s.). Imam Ali ar-Ridha (a.s.) alikabiliana na matatizo mengi sana kutoka kwa watu mbalimbali kama Bani Abbasi pale mwanzoni tu alipokuwa Imam. Tatizo la kwanza alilokabiliana nalo, katika siku ile ile alipokuwa Imam, lilikuwa ni kutoka kwa ndugu yake halisi na kutoka kwa mmoja wa wawakilishi wa Baba yake (a.s.) Imam Musa Kadhim alikuwa yuko jela na huko ndiko alikouliwa kishahidi vile vile, kwa kuwa gerezani aliweka majukumu kadhaa juu ya wawakilishi wake na baadhi yao walikuwa waaminifu lakini pia walikuwepo baadhi ambao walikuwa Imam aliwataka wawakilishi hawa kutoa mahesabu ya hazina, pesa zote walizokuwa wamekusanya kwa niaba ya Khums na sadaka, wao walitakiwa kuyaeleza hayo. Tusije tukadhani kwamba hakuna mtu wa kuuliza huo uwajibikaji juu ya Khums iwe ni kipindi cha ghaibu au wakati wa kipindi cha Imam (a.s.). Kwa vile ilikuwa ni vigumu kutoa majibu juu ya hili kwa hiyo walijibu ndani ya barua wakisema kwamba: sisi wala hatukuamini wewe kuwa ndiye Imam. Madhehebu ya Waqfiya ilianzia kutokea hapa kwa sababu



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 129 4/25/2018 11:01:31 AM

tu kiasi Fulani cha pesa walichokuwa wamekusanya kisingeweza kuchukuliwa kutoka kwao. Wala haikuwa ni mali yao binafsi, ilikuwa ni pesa za Khums na kwa sababu pesa hizi, wao waliukataa Uimamu wa Imam.

Leo hii wanakataa tu Wilayat ya Faqihi, lakini wakati ule waliukataa hata Uimam. Hivi ndivyo fedha ilivyo, kwamba inaweza kuwa ndio chanzo cha ukataaji wa Imam na Wali. Tatizo la pili liliibuka kutoka kwa ndugu yake mwenyewe, Zaid, ambaye Imam (a.s.) alimwita "Zaid un Naar", (Naar ikimaanisha Jahannam, hivyo alipewa jina hili na Imam kwa kumaanisha kwamba yeye atakwenda Jahannam). Yeye huyu alidai kwamba yeye ndiye Imam, (inawezekana alikuwa ni mkubwa kuliko Imam mwenyewe). Hebu sasa ione tofauti, kwa upande mmoja ndugu halisi kwa upande mwingine mtu mzee ndani ya Madina anapata hadhi ya Salman mina Ahlul-Bayt). Hivyo ndugu wa kweli anatajwa kuwa ni wa Jahannam na mtu mgeni anatajwa kuwa miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), hiki ni kiwango cha ukaribu. Hili lilikuwepo huko Karbala vile vile, wale walioandamana na Imam walikuja kuwa sehemu ya Ahlul-Bayt, ambapo wale waliokuwa ni watazamaji hawakuwemo.

Aliyekwenda ni nani, hilo sio swali kwa sababu ka-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 130 4/25/2018 11:01:31 AM

nuni ni kwamba walipaswa kwenda kwa sababu pale Imam au Wali anapoanzisha mapambano ya mageuzi basi sheria ni kumfuata, wanawake, watoto, wazee, vijana na wengine kutofuatana naye. Wanapaswa kuulizwa, lakini sisi tunauliza kuhusu wale ambao walifanya kile walichopaswa kufanya. Hili linatokea leo hii vile vile kama mtu anasema jambo la sawasawa basi kila mtu anamuuliza kwa nini amesema hivyo ambapo kwa kweli wanapaswa kuwauliza wale ambao walikaa kimya. Dunia hii iko kinyume. Watu ambao hawachukui hongo au rushwa wanaulizwa kwa nini hawachukui.

Hivyo, kama Karbala ikiangaliwa kwa mtazamo huu wa kinyume basi swali hili litaibuka la kwa nini wanawake na watoto walichukuliwa? Hivyo wasiulizwe ni akina nani waliokamilisha lengo lao, wakati kunapokuwa na wasaa, ambapo Hujjat wa Mwenyezi Mungu anapokuiteni, basi inakatazwa kutokufuatana naye.

Wakati Mapinduzi ya Kiislam ya Iran yalipotokea mnamo tarehe 11 ya Februari kisha Raisi Shah Bakhtiar alikuwa ameweka amri ya kutotembea na alikuwa ameamuru kuuliwa kwa mtu yoyote ambaye angekuwa ametoka Nyumbani kwake. Baadhi ya wanachuoni, pamoja na Ayatullah Taleqani ambaye alikuwa mmoja



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 131 4/25/2018 11:01:31 AM

wa viongozi wa mapinduzi alisema kwamba kuna amri ya kutotembea na ninasikia harufu ya damu kama matokeo ya amri hii ya kutotembea. Hivyo alisema kwamba mtu yoyote asitoke nje, aliyasema haya vilevile kwa Imam Khomeini (r.a.) awazuie watu wasitoke nje.

Hata hivyo, Imam Khomeini (r.a.) alisema kwamba ni Haramu kwenu nyinyi kukaa majumbani kwenu leo hii. Kila mtu anapaswa atoke nje ya nyumba yake ikiwa ni pamoja na wanawake na watoto wao. Hawa ni watu wanaojifunza juu ya Karbala. Hampati tu Khums kutoka kwa Bwana wa Mashahidi bali pia mnapata na moyo huu, hii hali ya ufuasi wa Husein (Husainiyat) kutoka kwake, hawa ndio watu wenye uelewa wa wazi wa moyo wa Karbala. Hatuadhimishi kumbukumbu ya Karbala, tunaisimamisha upya Karbala. Hii ndio sababu ya kwa nini Imam Khomeini (r.a.) alijivunia wafuasi wake; alikuwa akitumia kusema kwamba ni haramu kwa watu kubakia wamekaa majumbani mwao, halafu watu wakatoka nje, wanawake, watoto na imeandikwa pia kwamba wale waliozaliwa kwenye usiku ule, akina mama pia waliwaleta watoto wao wale. Hivi ndivyo tunavyopaswa kuchukua somo kutoka Karbala.

Hata hivyo, ni lazima izingatiwe akilini kwamba baadhi yao hawakutoka. Hivyo, ni akina nani wa-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 132 4/25/2018 11:01:31 AM

naopaswa kuulizwa? Kanuni iwe ni ipi? Wakati kila mtu alitakiwa atoke nje, ilitarajiwa kuwa ni mandhari ya maangamizi kwa vifo kila mahali,wakati kila Kiongozi kama Marhum Taleqani alisema kwamba anasikia harufu ya damu, lakini wakati kila mmoja alipoitwa atoke nje, yeye pia alitoka nje. Hakusema kwamba nadhani hili sio sahihi, yeye mwenyewe alitoka nje vile vile. Imeelezwa kwamba wakati alipomuomba Imam Khomeini kufikiri upya, hapo ndipo Imam Khomeini (r.a.) alisema jambo Fulani kwenye simu kwamba aliiliacha hilo na ameanza kulia machozi kwani alikuwa amehakikishiwa kwamba walikuwa watoke nje na ulikuwa ni wito wa kimungu. Wale waliopata kujifunza somo kutoka Karbala, hivi ndio vitendo vyao. Hivyo, wale ambao waliandamana walipaswa kufanya hivi.

**Swali la Pili: Kama tukiangalia nyuma, tangu kifo cha Hadhrat Muhammad (s.a.w.w.), zama za Makhalifa tofauti, kumekuwa na udhalimu mwingi lakini hakukuwa na mapinduzi,kwa kiasi kwamba Haruun Rashid alikuwa katika serikali na aliwakandamiza Masaadati kikatili kabisa, na hili liliendela hadi kwenye kuingia ghaibuni kwa Al-Hujjat (a.t.f.s). Kwa nini hapakutokea mapinduzi kutoka kwa Maimam kama yale ya Imam Khomeini (r.a.), ambamo alianzisha utawala katika uhalisia na am-**



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 133 4/25/2018 11:01:31 AM

**bapo ulimwengu ulitambua kwamba haya yalikuwa ni mapinduzi. Ni nini sababu ya hili?**

Kama ukiangalia kwenye historia basi unaweza kuuliza swali hili kwamba tangu Karbala au hata kabla ya hapo, kwa nini Maimam hawakuanzisha mapambano yoyote yale, hata kama ukimwangalia Mtume, kutokana na kile Qur'ani inachokisema, kwa nini na Mitume nao walikaa kimya? Hili ni swali muhimu sana. Hii ndio falsafa ya historia. Kuna majibu ya kina juu ya hili, kwa nini hapakuwa na mapinduzi kama hayo. Matukio haya yanayotokea yanaibuka kutokana na sababu zao. Allah swt. amemuumba mwanadamu na katika muda ambapo dunia hii inadumu, iwe ni wakati na kutoweka kwa Imam (ghaibat), kipindi cha Mitume au cha Maimam vyovyote iwavyo, kuna sheria fulani ambazo zinahitaji kufuatwa. Mabadiliko ya kijamii yanaweza kutokea tu kwa kutimiza sheria hizi. Moja ya sheria ambayo Qur'ani inataja ni ile ya kwamba:

إِنِ اللهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْم حَتى يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo katika nafsi zao.." (Qur'ani Tukufu ar-Ra'd; 13:11).**

Hili ni jambo ambalo lilikuwa limetengwa kwa watu wenyewe ili kuleta mabadiliko, ambapo kama ingeku-



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 134 4/25/2018 11:01:31 AM

wa ni kubadilishwa kwa nguvu basi iko kwenye maumbile ya Mwenyezi Mungu swt. Yeye Ndiye muumba wa ulimwengu unaoshangaza kama huu, hivyo kwa nini asiweze kuleta mabadiliko hayo Yeye Mwenyewe? Lakini hivyo sivyo lengo lilivyokuwa, kumlazimisha mtu kuleta mabadiliko, au kupitia miujiza. Unaweza kuona kwamba Nabii Musa (a.s.) ambaye alibadilisha fimbo yake kuwa nyoka vile vile hakumuua Firauni kwa muujiza. Nabii Nuh (a.s.) angeweza kumuongoza kila mtu kupitia muujiza kuliko kuvumilia matatizo ya tufani ile. Kama leo hii, polisi wanaweza kupata ungamo la uhalifu kutoka kwa mtu kwa kumpiga hata kama hakufanya uhalifu huo. Kama Mitume wangetumia mbinu hii basi ingekuwa rahisi sana. Kama Imam Husein (a.s.) angetumia miujiza basi Karbala isingetokea kama ilivyokuwa. Hivyo miujiza haiwezi kutumika kwa ajili ya muongozo, inaweza kutumika kwa kuonyesha uhalisia wao wenyewe kwamba wao ni Mitume.

Wakati Imam Al-Hujjat (a.t.f.s.) atakapo kuja, hata hivyo pia haitakuwa muujiza kwamba kutakuwa na uadilifu kila mahali kwa mpulizo mmoja wa tarumbeta. Kama hili lingekuwa litokee basi lingeweza kutokea hapo kabla. Hapana, yeye atatumia njia za kawaida-atatoa mwaliko na kuamsha wito wa. "Je, kuna yeyote wa kunisaidia mimi?" Na kisha mtapaswa kujitokeza



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 135 4/25/2018 11:01:31 AM

mbele na halafu yeye atawatakeni kusimamia shughuli zilizoko kwenye eneo lenu. Kila kitu kimo mikononi mwenu. Mwenyezi Mungu swat. ameliweka hili katika mikono ya watu, badilisheni hali zenu. Kwa hakika kuna uongozi kupitia Uimam na Wilayat lakini kwa kuwasili tu kwa Imam au Mtume kwamba mabadiliko yataanza kutokea hiyo siyo kweli, mwisho muhimu wa kuangaliwa ni Ummah.

Uongozi wa Kiislam unaojulikana kwenye madhehebu nyingine kama ukhalifa unajulikana miongoni mwetu kama Uimam (Imamat) na Ummat pia unaojulikana kijumla kama Wilayat. Wote, Imam na Ummah wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja; mmoja hawezi kuwepo bila ya mwingine. Kama kuna Uimam lakini hakuna Ummah basi Imam huyo atabakia kimya. Wakati Ummah unapokuwepo, lakini ukawa haukujiandaa, na Imam akawa hayupo basi hicho ni kipindi cha ghaib. Kwa nini hili litokee? Wakati Ummah unapomuacha Imam akiwa ametengwa basi Mwenyezi Mungu naye humuondoa huyo Imam. Sisi hatukutimiza ahadi zetu, Mwenyezi Mungu swt. aliwatuma hao, lakini nini kilichotokea? Wengine walikuwa kwenye magereza kadhaa, wengine walikuwa uhamishoni na waliotekwa nyara. Kwa nini hamkuwa Ummah mmoja? Mnaweza kulalamika kwa



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 136 4/25/2018 11:01:31 AM

Mwenyezi Mungu swt. lakini kulalamika peke yake hakutoshi kuamua lolote, mpaka pale mtakapokuwa Ummah mmoja kwa ajili ya Imam, tatizo hilo haliwezi kukomeshwa.

Mlitakiwa kuwa Ummah lakini mlikwenda kuwa kitu kingine kabisa, mlikuwa wafuasi, lakini wafuasi wa nani? Mliukubali tu Uimam wao lakini huo ni mwanzo ambao haujakuwa Ummah. Kuwa mfuasi (muqallid) ndio hatua ya kwanza kuwa Ummah, lakini sio ya mwisho. Mtafuteni Imam ili muweze kuwa Ummah wake.

Kuna mzaha, uchukulie kama mzaha, kwamba kulikuwa na muuza madawa ambaye jina lake lilikuwa Ibrahim na alikuwa akisimulia tukio fulani kwa watu. Alisema kwamba: nilikuwa nimelala wakati wa usiku wakati mtu mmoja alipobisha hodi. Nilifungua mlango na kumuuliza alikuwa ni nani. Jibu lilikuwa mimi ni Jibril. Yeye Ibrahim alimtaka aondoke na akamuuliza kwa nini alikuja. Jibril alijibu kwamba Allah amekuita. Yeye akasema kwa nini Allah ameniita mimi? Yeye hajaniuliza mimi kamwe hapo kabla. Yeye akasema kwamba mimi sijui lakini nimetumwa nije kukuita wewe. Yeye akasema, vyema, kama fursa imetolewa basi nitakwenda kuona.

Halafu Ibrahim akafuatana na Jibril na wakati pale Jibril alipomfikisha kwa Mwenyezi Mungu, Yeye aliuliza huyo alikuwa ni nani. Jibril alijibu kwamba huyu ni Ibrahim, lakini jibu la Mwenyezi Mungu lilikuwa kwamba nilimtaka Ibrahim Khaliilullah, huyu uliyemleta ni nani? Sasa kuna akina Ibrahim wengi lakini tunahitaji kumfuata yule wa kweli, yule ambaye anavunja masanamu. Mtafuteni huyo. Huu ni mzaha wa dhahiri, Jibriil ni ma'asum na anatambua ni yupi Ibrahim halisi.

Lakini mnahitaji kuangalia ni nani mnayemfuata ili kuwa Umma, na kuuelewa mfumo wenyewe. Huu ni mfumo mmoja mzuri sana ambao kama ukiangalia utaona jinsi ulivyo msafi.

Mwanafunzi wa Ayatullah Tabatabai ambaye amefariki na ambaye ndiye aliyewatambulisha Mashi'ah huko Ulaya anasema. "Kila kitu ambacho nimejifunza kutoka kwao nimekiwasilisha hicho kwenye vyuo

vikuu vya huko na wanafalsafa ambao walikuwa wamesikia kuwepo kwake lakini wakauhusisha Ulaya, niliwaambia kwamba Ushi'ah pia ni dini, (aliuwasilisha kwa wanachuoni na Hadith chache tu). Nilipowawasilishia dhana ya Imamat walishangazwa na hiki kiungo cha jinsi Shi'ah walivyomshushia Allah swt. na ulimwengu huu. Yeye mwenyewe ni mwanachuoni na



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 138 4/25/2018 11:01:31 AM

pale nilipowasilisha sababu hii ya kutoweka kwa Imam (Ghaibat) walibaki kushangaa. Huu ni mfumo mzuri sana kama utawasilishwa kwa namna inayofaa, huu mfumo wa Uimam, hii Karbala na hii Qur'ani.

Kama uongozi wa Kiislam unawasilishwa basi demokrasia inakuwa haina thamani tena, lakini Uislamu umo ndani ya mchafuko na balaa na hii ni kwamba, kabla hatuja uwasilisha kwa wengine kwanza tunahitaji kuusafisha sisi wenyewe. Tutawezaje kuuwasilisha kwa wengine? Tunaposoma Qur'ani ni nzuri sana wao wanasema kwa nini hamuifuati? Ni mfumo kamilifu na safi sana. Wote ni mwanga mtupu. Wilayat ni jina la kuondoa giza na kuingia kwenye nuru. Shi'ah ni dini ya Wilayat, na Wilayat maana yake ni kuondoa dhulma na kuelekea kwenye nuru. Utaelekeaje kwenye nuru? Kupitia mifumo hii ya kisiasa ya kilimwengu? Umeona kwamba demokrasia imeshindwa. Mnamchagua mtu fulani na mtu mwingine ndiye anayekuwa raisi, halafu inaamuliwa na mfumo wa kisheria na kuimarishwa na mawakala, halafu mnaushutumu mfumo wa Wilayat? Huu ni mfumo wa mwanga na nuru; tumevaa miwani za kiza kutuzuia tusiione nuru na tumewataka wataalamu kuizuia nuru hii kwetu sisi na kuwa kama giza. Ni dhahiri kwamba kama hii ndio hali yenyewe



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 139 4/25/2018 11:01:31 AM

hivyo swali lilikuwa ni kwa nini mapinduzi hayajibiwi ambayo mabadiliko yanayohitajiwa na ummah hayakutokea na ambapo mabadiliko haya yangeweza kutekelezwa.



04_18_(4-75 x 7) Falsafa ya Mageuzi ya Imam husein _ 25 April_2018 .indd 140 4/25/2018 11:01:31 AM